# *MAKUSUDI*

# *Ya*

# *Jana!*

MSHESHE R. RASHID

# MAKUSUDI YA JANA!

Kimechapishwa kwa mara ya kwanza 2022.

Haki zote zimehifadhiwa. Ni marufuku na hatia kwa wenye silika za kugushi, kuiga, kubadili, kuchapisha, kutafsiri, kuigiza au kutumia mbinu zozote bila idhini ya Mtu yeyote atakayefanya kitendo chochote kinyume cha sheria atashtakiwa

**ISBN 978-9914-748-98-7**

Kimechapishwa na;

**Elong'o Publishers**

**Nairobi, Kenya.**

Simu : **+254742433826**

*Baruapepe*: info@elongopublishers.co.ke

# YALIOMO

SURA YA KWANZA....................................................................................4

SURA YA PILI.........................................................................................13

SURA YA TATU.......................................................................................17

SURA YA NNE .......................................................................................30

SURA YA TANO .....................................................................................35

SURA YA SITA .......................................................................................42

SURA YA SABA......................................................................................58

SURA YA NANE .....................................................................................62

SURA YA TISA .......................................................................................67

SURA YA KUMI .....................................................................................72

SURA YA KUMI NA MOJA.........................................................................84

SURA YA KUMI NA MBILI ........................................................................90

SURA YA KUMI NA TATU.........................................................................95

SURA YA KUMI NA NNE.........................................................................102

SURA YA KUMI NA TANO .......................................................................106

SHEREHE ...........................................................................................116

# SURA YA KWANZA

*"AKili zikutue na zikukae sawa. Usiwe na gambizi kutokana hadaa za malimwengu. Wewe sadiki. Amini sana. Amini kuwa maisha si umri tu bali pia ni uhai na dunia yako. Tena ndiyo abadi kubwa unayoishi nayo. sasa iwe vipi hivyo? iweje huna ukumbukalo. hata ukoko wa wali wa jana huwezi kuutambua! Mbona tena unao mchezo huo wa kujiuliza kama kwamba maisha ni mtihani wa kwako pekee? kila kiumbe ana yake. Hujajua hivyo hata sasa! Jamani! Maisha hayana mzaha. Hayachezi ngoma goya na mlimwengu. Kama wewe wapenda mzaha na utani, basi ujihadhari nayo ndugu yangu.*

*Siku zote, kuna kupandana na kuporomoka kama yapo mabonde ya mlima. Kuna kucheka na kulia kama mtoto alipozaliwa na mkongwe anapoleta ukiwa. Kuna muda wa kutenda sabili ya wema na wakati wa kujipa hongera mwenyewe. Upo muda wa kujutia mdomo juu. Wewe mwenyewe, umejigundua kuwa upo kwenye jahazi la fahari linaloselelea safarini. Sasa wasafiri na fusra zilizo azali. Wasafiri kwenye bahari ya kuishi kwema walau wafahamu kwamba mambo mengi katika safari hii ni ya kujibahatishia; bahati nasibu tu. si haramu ni nyota yako halali kabisa.*

*Hata hivyo. Nakuona haupo makini. Siwezi kukuita bundi, bado ukomavu haujakushika mkono vizuri. kuna hatua zinakungoja uzipigie misamba imara ili uwe sawa na shwari. Nitakufaa sasa. Naomba tusafiri pamoja ingawa hujanipa ruhusa wala mwaliko siku hii. Si sikio haliwezi kulala njaa. Tena haya yako hayajafa. Nisikie mwandani.*

*Maisha ni mwendo wa kila mtu na njia yake. Tafauti na kwenda peponi. Maisha ni mtatago wa chuma kati ya nafsi na maazimio ya mtu wa Mungu.Yaani, hakika ya kuishi ni huku kula tabu na kuwahi tabia ili uvue ruwaza njema baadaye. Bila hayo upo nunge!*

*Si mara moja, umejipata ukiulizwa.*

*'Ee mwafulani, umeyatambua malengo ya maisha yako?'*

*Si jawabu unalo hapo? kimoyomoyo wajibu ama wajibizana. Na Zaidi ya aghalabu, umejiliwaza kuwa, kuishi hakuhitaji malengo wala kapu kubwa la bidii na uchu tu. Aha. Lazima kuwepo fundo la siri kuhusu chombo hiki tunachosafiria sasa – maisha.*

*Hewala, nafahamu kwamba wajua namna usafiri wako ulivyo. Waelewa fika kwamba safari yako ya kuwa mtu makini ilishang'oa nanga kwenye bandari ya Ulimwengu wa sayari ya tatu. Mumu humu kwenye maisha ninayokuelezea kinaganaga kuyahusu. Huna budi kuwa dede na mtu tayari. Ujiandae ipasavyo. Binafsi yapo unayoyahitaji. yapo unayoyakisia masikioni ila yapo pia yale usioyatarajia usoni.*

*Kutoka sasa, wahitaji maadili mema, tabasuri na hekima kando na ucha Mungu kukabiliana dhidi ya mawingu ya misukosuko ya maisha. Maisha yetu yapenda hupiga selo pasi na tahadhari; si mchana si usiku. Yana mashakafundo na uvundo wa kila aina. Uzuri na urembo wake pia upo papo hapo. Yana ukili wa miwa. Upo ubavu wa shida na ubavu wa afueni. Huna budi kung'ata sehemu yako kati ya hayo. Ufanisi wake... Utafute!*

*Toka zamani, ulidhania kwamba maisha ni kipaji cha kujielewa tu. Ndivyo ulivyousiwa ukiwa mwanafunzi asomaye. Huwenda hawajakosea. lakini ni wajibu wako sasa kujiimarisha na kufikiria vinginevyo. Tofauti na awali, hautavavagaa huku na kule bure. Kumbuka uliko toka. Kumbuka, Sarabi si maji. Usiamini kila ukitiliacho macho. Fungua macho wakati mwingine. Ona........Ona sasa... Haya fanya hima."*

Sauti asi ilininenea. Sauti hii ilikuwa ya kupekuapekua na kujaa maneno mazito, ilinijia na kuninyemelea taratibu pale nilipokuwa

nimekaa kimya. Ilikuwa na shauri mbaraka kwangu ingawa ilipeketekea utulivu nilioutafuta kwa masumbuko mengi. Hata nawakwepa baadhi ya watu kwa kusudi hilo. Sauti ilikuja na uradidi wake kama i ukaidi. Ikanipa mpasho wa thamani. Maneno ambayo yalinitahadharisha na kunipanua ubongo kiasi cha haja.

Dukuduku zikajisozasoza taratibu katika chumba cha akili yangu. Nikatoneshwa na kutononeshwa. Si uwongo. Si ukweli. Hata nafsi ikaamua kunishauri kwa utulivu na busara yake. nami nikakunga mkono. Sikujua ni kwa nini walau niliupokea ujumbe huo kama kwamba ni jambo sijambo tu!

Licha ya sauti hii kunigongea hodi asubuhi kama ya leo, mimi mwenyewe nina mazoea na tabia ya kuchanga bongo wakati kama huu. Hasa ni kama mazoea ya kupapia kwa kijoko. Napenda sana kudurusu mambo mbalimbali ya siku yenyewe kabla ya kwenda nje juani. Muda huu ndio wangu wa kupanga mikakati ya hapa na pale. Napanga nikipangua mpaka ‘njama za asira na asiria’ zinagalana sawasawa. Bila hivyo, mambo mengi hayatatazamika wala kuafikiwa. Wazungu husema, *if you dont plan, you plan to fail and dead men don't make shadows! "* Kwa hakika, sipendi mambo yanayovurugika. Eti yawe tamathali ya mihogo chapachapa. Niitwe mtu ovyo, tena bure bwerere!

Staghafiru, Mwenyezi nitangulie na uikubali fatiha yangu kwani la kushangaza ni kwamba siku hii, nimeshindwa kutekeleza ukawaida wangu. Nimeshindwa kufikiria mipango yoyote. Mabongo yamelala kimya kama pono. nimenaswa na kufumbwa kwenye nasaha za sauti ile iliokuja ghafla kama mwanga wa kijijini. Nikawa mfano wa msukule. Naam, sauti hii iliniiba sana, mimi na nafsi yangu, zaidi ya mno, nafasi yangu binafsi. Ilinipokonya uhuru wangu wa kuifikiria leo na jana yake. Kumbe sauti ya nafsi ina nguvu kiasi hiki?

Yakini ni kuwa ndani ya sauti ile, niliona wazi kuwa leo si jana wala si majuma ya majuzi. Leo, kumebadilika na yamebadilika mengi.

Mathalani nilijua ati, '*mwanzo wa ngoma ni lele*'. Picha nilizoziona zilikuwa kama mwanzo mpya kwangu. Ni hatua chache tu nimeshazipiga kwenye uzima wangu hadi sasa. Niliona hivyo.

Kila kitu kimebadilika juu chini seuze kuchukua mikondo tofauti. Hata mimi nimebadilika mno. Mabadiliko yangu si ya kitambo mno ila yamekuwa kama kumbukumbu safi zaidi ya pamba za usufi. Ninabadilika polepole japo mwendo wa dunia una kasi sana.

Siwezi abadani kuikata kiu ya kuyatanabahi yaliofanyika katika maisha yangu ya kisogoni. Kuyasahau ni sawa na kukataa mlo! Hivi, nani hapendi kula? Nani? Nani! Lahaula! Anaenzi njaa! Ama tena niitwe mso mila, mtumwa. mtu hatoroki ngozi yake. Hata vipodozi vyafahamu hilo. Atajiumbua tu. Hashamkum si matusi, kama mshenzi akipata ngou husahau na kwao. Mwenzenu nina asili. Naijua alifu kwa kijiti. Siwezi kuisaliti. Kujikumbuka ndiko sitara yangu.

Sadiki Wasuka – jina nilililoliwahi siku ya kuzaliwa. Isitoshe, limekuwa kama baraka kutoka kwa babu yangu Mzee Wasuka Sadiki.Sikiri mengi zaidi ya hapo, kwani mambo ya milango yetu huwa mengi hata kuyaelezea wazi huwa tabu wakati mwingine. Kwa sasa nina bahati ya kazi. Kazi ile ile iliokuwa ndotoni mwangu tangu ukembeni. Ni dhahiri tena wazi. Ipo mikononi na viganjani mwangu. Naipakata na kuieleka kila siku kama mwana na mlezi wake. Mimi Sadiki, Nimefaulu kuwa mwanasheria wa hadhi na haiba tele kwenye taifa letu. jamhuri ya Mfumoni.

Takribani mwongo mzima umekamilika tangu nihitimishe masomo yangu kule chuoni Bongonyota. Baada ya kuhitimia uzamili wa uanasheria na kufanya sherehe za mahafali. Nimekuwa fahali tosha kwenye uwanja mpana wa kupanua utendakazi nchini. Hali yangu ya maisha imenivusha kwenye mirija na mabomba ya kuchuma riziki tumbi kwa tumbi. Tena kwa uhalali wa tajiriba yangu. Kila siku hunigongea hodi kwa ufanisi na neema zake. Mara si moja. Tabasamu

hunijaa usoni nikiwazia haya. Naishi kwenye nyota ya jaha. Nyota iliyoiotea mwenyewe. Hata kidogo haijaiatiliwa na mtu. Ni ndoto ile ile halisi toka zamani.

Ndoto niliyoiota kila mara kwenye malepe ya usingizi wangu ilitimia na kufana wazi kama vivunga vya nywele kichwani. Maisha yalinitekenya na kunikumbatia falau ya mtoto mchanga. Nala shibe ya tumbo na kujivisha fasheni za kisasa asiria. Naishi kimamboleo kando na hawaa zile zilizomzika fisi angali hai – tamaa na mauti. Ningali namshukuru Mungu kwa uteuzi wa kuishi hivyo. Raha ilioje kutimiza ndoto ya masiha. Mashallah!

Kando na kuishi ndani ya utamu wa maisha. Nimesifika kwa upekee wa kazi. nasifiwa kwa ujuvi wa kuichenga nyundo ya hakimu. Si kwa uhalifu wala shere. Nilifanya hivyo kwa kutumia hadhari na busara aliyonitunukia Mterehemezi kando na uwazi wa elimu yangu pana. Nilipiga dua kila siku kuwa mbusarifu. Nilifanya hivyo, kuepuka dhihaka zenye majira yake. Dunia mzigo wa mengi, kuubeba ni stahamala pia.

Kazi yangu ilinikubali toka ukucha wa guuni hadi unywele wa utosini. Kila niteteapo hoja zangu dhabiti - za kesi ninayowakilisha kortini, jaji huona haya kuwashika kombo ninaowatetea. kwa kuwa ushahidi wangu huwa shadidi. Siyumbiyumbi wala sitapitapi. Nipo mahiri na imara sawa na chuma ya pua. Haya ni zamani kidogo, sasa hivi nimebadilika tena. Nimeimarika katika kazi hii. Nina makadara makubwa haswa! Hakimu mkuu. sikuwahi kutarajia nafasi hii ila ndio hivyo. Silalamiki.Mtu hujengewa kwa fitoze.

Maisha haya si nyota ya jaha tu. Ni nasibu ya Mungu mwenyewe. Nishikapo jambo, duduvule huniheshimu. Natenda kutenda. Nafanya kutekeleza. Hata kwa siku kadha wa kadha hivi, nimekuwa mtetezi kama wa wasonacho na kikwazo kwa wale wajiwezao – wenye mabavu na mabega seuze vifua! Yafikapo mahitaji

ya mahakama, nisingekosa kuwa jembe, nililima suluhu na kuyatufua magugu ya dhuluma. Kukosekana kwangu mahakamani kukawa kosa kubwa kama la jinai. jengo zima la kesi zima lingetumbika macho popote kunitafuta nilipojibanza. Nilihitajika huko sawa na nira kwa maksai walimao shamba. Kisa? Kinolewacho hupata.

Kando na kuwa mfanyakazi mwanasheria mwenye kutambua kazi *ni kanzi*, asubuhi hii ya leo niliamua kujipa nafasi niwe peke yangu kidogo. Ni muda wangu ule wa kupumzika kabla ya shughuli kunipigia tari tena.Nimetulia tuli kitini kwenye afisi yangu ingawa akili zangu zimetumbikia mahali nilimokuwa kisogoni.Zamani sana.

Vilevile, kuna kesi zinanisubiri jino kwa jino kule mahakamani saa chache zijazo ilhali nahisi nimechoka. Ni kama nimetwekwa nyara. Sio ya kwamba ninaogopa kutoa hukumu. La hasha! Mara hii nimejihisi tofauti kabisa.

Bila kusapasapa kitoweo mbali na kinywa, kazi yangu hii ya uanasheria, niifanyayo kwa uzoefu na welekevu, leo imenikumbusha kisa kimoja cha zamani sana. imenitumia sauti pevu mawazoni. nikawazawaza. haya na yale yote yakaja na kumwagika wa! dakika zikashika hesabu. moja hadi sitini. wazo baada ya wazo. mwisho uchovu ukajilaza kichwa kizima.

Kwa uhakika, hisia za kuchoka kwangu na kule kuwazawaza kwangu kulikuwa na nia moja. Kulikuwa kumoja. Visa hivi viwili viliingiana sana shilingi kwa ya pili. Ni ajabu kubwa hata kwangu mwenyewe Sadiki.Sijaweza kusadiki.

Kwa kuyafikiria mambo yalivyokuwa zamani, ninaona yale yale mabadiliko niyasemayo. lakini kuna kiza kinachomea na kunawiri kando. Naona peupe mambo mengine yakiwa makavu mno mbele ya macho yangu kuyatazama hata mara mbili. Hayakupendeza hata kidogo. Yalitisha na kuvunja magoti. Nilijiruhusu kutafuta majibu ya mbona kukawa hivyo. Niliizungumzia mwenyewe kwa upana sauti ile

iliofika pasi na mwaliko. mawanda yalipwa kama bahari chafu.

Macho yangu ya mshabaha wa kifuniko cha chupa yakiwa yananoanoa hivi na vile kwenye mwangaza uliopo dirishani, mkono wangu wa kulia ulijiweka pacha na uzito wa kichwa changu chenye komo dogo mno. Ungenitolea macho kwenye mkao huu wangu ungenifananisha na ngole waliojianika kwenye mawe uani. Nilisisimka tu bure kama ndege aliyepigwa na mawaga.

Damu ya mwili wangu – niliihisi ikichezacheza na kukimbia kwa kasi yake mwilini, huku ikitulia ghafula na kwa kichea. Nywele za mwili wangu zilisisimka hadidi japo sina wasiwasi kwa lolote lile. Hali ya joto wala baridi haikuwapo jengoni pale kutokana na juhudi zilizotimizwa na viyoyozi vya teknolojia ya kisasa.

Mkono wangu wa shimali ulifurahia kuchezesha kalamu iliyonyiririka vidoleni. Mkabala wa bega langu la mkono uo huo, kuna rungoya ya kisasa. Mwangwi wa nyimbo za sasa uliakisika masikioni bila kero. Nadhani nilikuwa nikitegea sikio nyimbo za taarabu kama sijakosea.

Midundo ya moyo wangu ilikuwa ikisakatia lele za nyimbo hizo. Hii haikuwa kama ada yake. Huenda ni mbwembwe tu za siku kama hii. Mwili mzima ulijisawazisha kwenye kochi lililoyumbayumba mbele nyuma kama bembea. kimya mawazoni.

Sijui mbona ninajihisi hivi. Sijui mbona nilipata tahafifu mapema hivi. Sijui mbona mawazo haya na dhana zile zilinijia akilini. Fikira zangu zilikuwa zinakwenda chakachaka. Akili yangu ilipata miguu ya kutembea mbali. Labda ni kutokana na hisia za sauti ile.

Tuligeuziana mawazo kwa kila sekunde ya muda. Tukabishana vilivyo. hata hivyo, kwa aghalabu, niliipa nafasi inifafanulie mambo yake kama nifanyavyo kwa mgeni yeyote yule ajaye pale afisini. Tuliulizana mengi sana. Niliuliza swali na maswali. Nilitaka kujua.

‘*Mbona unanionesha mambo tofauti na makusudio yangu?*’ niliiuliza sauti.

*"Kila kitu hufanyika kwa kusudi. Nafanya hivi, upate nafasi kuwarekebisha hao wengine! Sauti ilinipa jawabu.*

*"Hao kina nani? Hawana hata hiari zao? Kwani mtu hana hiari ya kufanya mambo yake? Mtu hufanya atakavyo." Ningejibu vile.*

*"Mtu ana hiari mbili tu. Kutenda kusudi nzuri ama kushika kusudi mbaya. Kila kusudi huwa na matokeo yake." Sauti ingejibu kijasiri sana.*

*Sasa.Kwa nini basi umemchagua huyo rafiki yangu kuwa haya? Nijibu? Mbona yeye?"*

Nilikaza maswali huku nikitutuma. Hamaki nazo (ndani kwa ndani) zilikuwa zichanganyikana na huzuni nilipouliza hivyo.

Sauti haikunijibu. Ilisimama kimya mlangoni pa afisi yangu. Niliitazama hoi ikibenua midomo yake na kutikisa kichwa kana kwamba inanihurumia mimi na nafsi yangu. Ghafla ikatoweka kama ruhani. Nikabaki pweke nikijisaili mwenyewe maswali yale niliyoyauliza mara kadha wa kadha minghairi ya majibu. Binafsi, nilikosa kauli kuhusu hayo. Hatimaye nikaungama kwamba ‘*Mungu humwongoza amtakaye*.’

Sauti iliniwacha nikichimba fikira zangu. Nilikuwa ninawaza mambo yanayonihusu mimi mtu wa Mungu pamoja na waliokuwa karibu nami. Hivi sasa, nimezama kwenye lindi zito la fikra. Nimedhuruku na kukumbuka ya nyuma yangu. Muda huu wote pale afisini mwangu, nilitia na kutoa mawaidha mawili matatu ya zama zile. Jambo lililotendeka udogoni kumbe laweza kujirudia!

Huruma na simanzi. Simanzi na majonzi. Yote yalininyemelea kama paka aliyemwona panya aliyeenda chechele chumbani.

Namhurumia sana rafiki yangu. Nina hawafu kubwa kwa yaliompata na kumsonga mwandani wangu wa zamani. Hata la zaidi ni kwamba, nazidiwa kuwa na kiwewe kwa yale yanayomteka bakunja siku hizi.

Ningekuwa na uwezo kitambo hicho ningempa mkono dhabiti. Wakati ule sikuwa mtu wa jina kama sasa. Kitambo kile, nilikuwa mtu wa utu kando na uchu wangu wa kutafuta ya kesho. Sikuwa na nguvu mikononi wala kinywani.

Hekaya hizi zangu za kumsaidia mwenzangu zilibaki kuwa malindi na miamba telezi. Miamba na malindi yale. Hayakuwezekana kamwe. Jinsi alivyo siku za leo. Nimetonesheka si haba hata nimeshindwa kusadiki kwamba kuna vitu haviwezi kubalidika hata kwa hiari. Ndivyo alivyo Makusudi sasa.

## SURA YA PILI

"Mtaa wa Mapona ndipo familia yetu ya Mzee Mlafani na mkewe Rehema ilipopiga kambi. Huku ndiko makazi yetu yalipojifaa zaidi tangu nilipokuwa na ushuo wa kuyakumbuka maisha haya ya udogo wangu. Yaani, tangu na tangu. Tangu nilipopata hatua ya kutii amri za wazazi na walezi wangu.

Kwa mapana na marefu, Mapona ni kiunga kilichokuwa mfano tosha cha kusimulia vyema jinsi maisha huwakubali wachache na kuwakataa halaiki! Akina wana wa panopano kama mimi na wengine walio humu, tuliusadikia ujadikubeli wa Mapano.

Tulikuishi kwa kupiga gae starehe mustarehe si mchana si majio. Kulikuwa ni dunia ya aina yake. Pahala pa kujivunia. Mapandikizi ya majumba ya mabwenyenye yalipata starehe na naima huku. Yalikuwa yamejengwa na washi waliotoka ng'ambo hasa Ujerumani.Wajenzi hawa walikuwa ni kamusi za ujenzi. Walifahamu fika matakwa ya kujenga makazi ya kuvutia na asa za kubembeleza nafsi.

Majipaa ya majumbausi yale, hayakuezekwa makuti wala mabati. Kulikuwa na vigae spesheli vilivyotulia kwenye paa hizo kama kofia jekundu. Kila jumba lilikuwa na nyua pamoja na lango kuu.

Mabango ya '*mbwa mkali*' yalining'inia kwenye vibanda vya mabawabu vilivyokuwa mkabala na malango makuu. Mara nyingi, kimya kilitembea peke yake mtaani Mapona.

Kila mtu huwa kwake na shughuli zake. Hata kucheza, watoto walicheza kwenye nyua zilizokuwa binafsi. Ndandalo na magogo ya umeme yalipenya njia chache zilizokula lami kupindukia. Si shani kupata mangazimbwe majira ya jua mti kati.

Usiku taa za usalama zilimweka na kumulika. Mwangaza wa taa hizo ziliwabari wenye ila kutenda yao maeneo haya. Isitoshe, majibwa

makali yalikuwa yamefunguliwa muda huo. “Bwe! Bwe! Bwe!” Yangebweka – Ujumbe uliotosha kwa masikio ya yeyote aliyepanga mambo tenge. Waliokuwa na bahati mbaya, waliparuzwa na chengo za majibwa yaya haya. Kwani, mdharau mbiu hubiuka!

Mapona ni Ulimwengu wa ukwasi ambao tayari uliweka himaya yake si kwenye upeo wa macho tu bali pia katika hali ya siha na afya kati ya wenyeji. Utajiri huu tulitulaki na kutudaka kwa mikono miwili. Tena kwa yakini, ulodi ulitukaa nasi tukauvaa. Mapona kukawa sitaha ya kutamaniwa na wengi walio kando.

Kadhalika, kando na ulimbwende wa mazingira, uchapasi wa majengo na vijana wenye mavazi sheshe. Vitu vyote vya kutajika na hata kutofahamika, vilikuwamo mzomzo kwenye maduka makuu mumu humu. Vitu vyenye thamani ya taanasi na vitu vyenye thamani sawa na dhahabu vilishamiri maduka ya Mapona na mbavu zake.

Hata nikidhania, vijana wengi waliopo humu waliponea chupuchupu kuzikumbatia tabasamu za dhiki kila uchao. Vijulanga wa Mapona hawakuwa gora moja na wale walio Masazoni wala Kichakamkwaju wala kwingine kule isipokuwa jiji la Mashombo.

Uzuri na ubaya wa maeneo haya kidogo ulikubali kutiliwa shaka asa kwa sisi wenyeji wadogo. Hatukujua kucheka na njaa. ‘*Ku namna gani*?’ Swali lilikuwa fumbo kwa kila mmoja wetu wa Mapona.Kisa na maana, kutarazaki kuliwakubali wazazi wetu kwa kila nafasi walioipata kutukimia mahitaji yetu.

Wengi wetu tulijishanua kwa madaha kuliko tausi nusura ya kujisahau na kuwakengeza wengine wasio mizani sawa kwetu kwa mabezo yetu. Baadhi yetu, walianza kutembea mwendo wa bata huku wakiyatenda yao huku wakinai wale wana wa pangu pakavu tia mchuzi. Hawa walikuwa pua na mdomo nasi. Kwa hakika ni majirani wetu wa sehemu hizi. Kwa waliokutamani kulibaki mithili ya simulizi kupata

jamvi la kuishi Mapona.

Mathalani, shida na changamoto mchafukoge zilisalia kwa wakazi majirani kama mambo yasio shani wala bina. Hata yalipotajwa hawakushikwa na kicho seuze woga wa kunguru kufukuza mbawa zake! Wameshayazoea.Waliyaona kuwa halali labda kwa wengine kama sisi yangekuwa haramu ila si kwao. Hakika kinyume cha mtaa wa Mapona ni hapa Masazoni ama kule Kichakamkwanju kama si Mtemanyuki.

Vichochoro vya sehemu hizo vilizidi wingi wa kunguni kwenye kitanda kichafu. Majengo ya mitomo iliokosa mbavu za kujihimili vyema yalitazamana kwa huruma ya kumwangukia mwenzie wakati wowote.

Mitaro mikubwa ilipitisha maji ya taka badala ya maji safi kama yale ya mto Marambo.Mifuko za sandarusi ilipepea kila pahala. Hata kuku na bata walijifunga nailoni hizi kwenye vipi vyao kwa bahati mbaya wanapochakura pipa za takataka.

Mapaa ya kila nyumba hujinyoosha kwa vilio wakati wa jua kali la mchana. Hakuna anayehimili kuwa ndani ya himaya yake muda huo. Ni tabu juu ya taabu.

Kwa kweli, tukilinganisha sehemu hizi, ilikuwa dhahiri shahiri kuwa, wenyeji wa Mapona, tumepiga mbizi kwenye uki wa maisha ilhali tukasahau kuwa mawimbi ya shubiri – shida, huwa na huja.

Kuwa Mashombo au Mapona kulikuwa sawa na kuishi Masazoni au Mtemanyuki.Sababu ni kwamba, watu wote walihitajika kujituma sana ili kuyafikia waliotunukiwa na Mkawini mbingu. Wakazi hawa walibaini kuwa ili kuota mleli kwenye fanaka ni lazima kujituma na kutia nira maishani.

Watoto wa sehemu hizi zote pamoja na Mapona walijumuika katika safari moja. Safari ya kupata elimu. Walienda katika shule

zilizokuwa na mvuto wao. Wazazi wa huku walitutakia heri njema ya siku zijazo.

Sisi watoto wao hatukuwa na jamvi tofauti na wavyele wetu. Tulisubiria kwa hamu kuu. Maisha ya kesho yalitusubiri sana kama kinywa kinachotaka kutaka kiu kwa maji baridi shadidi.

Kwa udogo na utoto, wengi wetu walizembea kujitendea haki. Mimi na wenzangu nyakaa hizo, tuliishi kujisahau mara kwa mara ingawa dalili za kesho zilitusubiria wenyewe tuzipe amri. Taraa, ubwabwa ulikuwa ungali umekolea kwetu. Kwani, dalili ya mvua ni nini?

Juu ya hayo, tulifaa kujiundia kesho yetu kwa makini mno. La sivyo, tungejutia shida zitakazokuja usoni petu kana kwamba ni bamvua na tufani. Kujiuma ulimi kinywani kulikuwa sako na bako nasi.

Tope la majuto lilijilegeza ovyo kama ulimi wa kinyonga kutunasa. Atakayeteleza topeni, ni basi. Majuto makuu. Si twafahamu eti si uwongo kuwa, majuto ni mjukuu na huja kinyume. Tulisalia na jukumu la kujichunga kando na kujitafuta katika nafsi zetu.

# SURA YA TATU

Takribani kilomita sita hivi kutoka hapa Mapona, kuna kivuko. Sehemu hii ina umbo la pembetatu. Hili ni daraja la zamani sana. Tena, ndipo njia ya pekee ya kupiga charo na kuvuka kuja mtaa wa Mapona au kwenda kwengine kule.

Wenyeji wa ng'ambo ya pili walipaita ***'Daraja la Marambo'***. Inasemekana kuwa, kivuko hicho kimestahimili mengi. Si ya kushangaza tu hata tutaje ya kutamausha moyo yangali yamesalia visa vya kutajwa vinywa wazi pale darajani.

Si ajabu wala shani kabisa kwamba, hapakosekani kisanga na kiroja wakati wowote ule. Si kuteleza na kusakamwa miguu kwa wapitanjia. Si kubomoka kwa vidato vya mtatago huo. Si kutamalakiwa kwa mvo mzito wa mvua ya bojo ilionyesha kila uchao. Si kugeuka kitenda cha mamba waliowandawanda kuliko nguruwe. Si hili si lile. Iwe kwa kiza cha usiku, iwe kweupe kwa mchana. Yalitendeka yakutendeka.

Jambo kwenda mrama pale darajani – ilikuwa kawaida kama sheria kwetu wapita njia. Kila aliyetarajia kuvuka, alishika roho mkononi pamwe na nia njema mdomoni. Tulijipigia fatiha kwa hadudi na hadidu. Apenadaye mkasa ni nani?

Licha ya hayo kuwa, *daraja la Marambo*, lilibakia kuwa mpaka wa ng'ambo yetu na viunga vingine vya Mashombo kama vile; Kichakamkwaju, Kijutoni, Masazoni, Mtemanyuki na kwetu Mapona.Viunga hivi, viliundwa kwa miundomsingi dhaifu sana. Barabara ndefu zilizosheheni mabonde na matuta ya mashimo. Mashombo na Mapona ndiko kulikokuwa tofauti na maeneo mengine.

Upitapo huko, macho yako yangeona vazi kubwa la mararuraru limejitandika ovyo na ungegundua baadaye kuwa ilikuwa ni njia tuliojengewa na Gavana wetu Bwana Mwamba! Wakumpigia debe wangemshauri aiboreshe barabara hii ila walimwogopa kama bundi.

Mavumbi hayakukosa kutuonyesha umahiri wa kujisiteri kila yalipojitifuatifua kuunda tufani. Vilevile, kulikuwa na misururu ya vyumba vya mitomo pachapacha, vichochoro vilivyokata kona haraka pamwe na upeo wa umati wa watu majira ya macheleo na jio. Watu hawa walifurika sawa na mchwa kwenye shughuli zao za kutafuta jasho la siku.

Watu wa wali deni mchuzi karadha, walitapakaa na kupayapaya huko kama vikembe vya panyabuku. Hawa ndio wajuao ya kwamba,'shibe na raha mustarehe za mwana Sultani si mchezo mwema kwa msaka tonge mchochole!’.

Usumbufu na ugumu wa masiha uliwashikia mbio za swara nusura yakuwamwaga kuzimuni. Kutafuta mali kupita himila za tumbo na koo zao kuligongesha meli mwambani. Wachache wao walifaulu kupua nguo za ufukara huu. Mfano mwema ni wazazi wangu.

Kwa waliosalia, shibe ya kucheka na mlo wa leo hakukutajirika wala kukutwa. Bali kulimithilishwa na hali ya kuwapapasa nyuki na nyigu masegani mwao! Ilikuwa vigumu kushabikia milo bwerere hata kwa kuibembeleza. Kupata kulikuwa shida na kukosa kulizidisha shida. Hatari ilioje hii!

Abadani kataani. Wenzetu hawa. Hawakupikika na utamu wa maisha chungu kimoja. Walipata makombo ya ukavu wake tu. Kila jambo lilikuwa kisirasni kama si chira. Nyuso ziliwavuka kila uchao kwa kutabiria mashakafundo kugonga hodi. Nuksi za siku zilikaidi kuwageuzia mgongo kabisa. Upo wakati walingedhani wametendwa!

Sio kosa la kutoa doa kusadiki kuwa, wote walikuwa sehemu hizi, wamefunga ndoa ya paka na mbwa kwa uhawinde uliowatua na kuwatulia tuli. Huu ni umasikini wa kukinaisha macho na moyo, nao ulijitandikia misala si Kichakamkwaju, Kijutoni, Mtemanyuki wala Masazoni –mitaa wa mburu matari.

Waling’ang’ana kujibandua alakulihali kujiondoa shabukani. Waliyakinisha ya kwamba, wali wa kushibia huonekana siniani tu. Hivyo, watia bidii za duduvule kugota msonabari kila siku. Wazazi wangu walikuwa kielelezo chema kwako. Walijua ipo siku.

***

Upande wa kaskazini mwa Mapona na Masazoni, kuna shule ya msingi ya Chumio.Shule hii ni ya kipekee huku bila shaka. Imewatangamanisha walalahoi kwa walalaheri seuze wanafunzi kwa walimu. Hawa wote wakiwa wa tabaka na dini zisizo sawa kwa mizani moja. Shule hii ilituleta sote kuwa fauwa. Shule ya Chumio na walimu wake ikawa kiini cha elimu Mapona na Masazoni.

Mimi na Makusudi, rafiki yangu wa mafiga na vinga-tulisomea hapa Chumio.Ushababi wetu ni wa tangu na tangu ulianzia kushika mizizi Chumio na baadaye kunawirisha shina na matawi. Tangu madarasa ya chekechea hata sasa, tumekuwa mti mmoja mkubwa mithili ya mbuyu. Urafiki wetu ulikuwa unanawiri kila siku kama uyoga.

Japo hali zetu za kila siku zilikuwa kama ardhi na mbingu. Usena wetu wa nia safi nyeupe kama maziwa na tui haukukatika kamwe. Tuligandana kwa kila jambo mfano wa utomvu na mti wake. Tulishirikiana kwa mengi sawa na kinu na mche wake. Undani wetu huu ulikuwa alifu kwa kijiti tulipoanza kwenda shuleni. Pindi tu tulipoanza kusomea shule ya msingi ya Chumio.

Utajiri wa kwetu na ufukara wa kwao haukuwa kizingiti wala mkingamo tosha kuvunjia mbali urafiki wetu. Mawili hayo.

Tuliyafumbia macho kila tulipokutana ana kwa ana. Tukafaana kwa mengi kuliko kufanana kwa uchache wa maisha yetu. Si nyumbani si shuleni. Usena wetu ulitupigia goe sisi wenyewe.

Daima, tulipiga dua na kushika nia kwake Mungu ili usahibu wetu usifikwe na masaibu yalomfika mtaka jamvi katika baraza la wakongwe wenye ghadhabu – kujitia matatani bila mwao. Kukosana kwetu kungekuwa hasara si kidogo. Kivyovyote vile, hatukutaka kuvurugana wala kukosana kwa lolote lile, tuliepuka kuwa sawa na mafuta na maji.

Mara si moja, muda uliponikubali, niliweza kutoa mkono wa heri kwake. Nilimpokeza mavazi sheshe yaliyokataa kunikaa pima. Naye aliyavaa kwa buraha iliozidi kifani pamoja na mziwanda wao aliyeitwa Chachania.

Siku zijazo, sikukosa bashasha na furaha kila waliponialika karamu ya kuramba vidole nusura kucha kuchanika huko huko makwao. Siku ya siku inapotia guu, hawakusita kunialika kando na marafiki wengine. Hivi, urafiki na usena wetu tayari ulikuwa waramba asali ya kupendana bila kumpwekesha mwengine.

Wenye usuli na asili ya lugha waliwahi kusema kuwa, “*Mwana akibebwa hutazama kisogo cha ninaye*.” Naam.Wazazi wetu pia walichanga bia pakubwa huu uhusiano wetu uliokuwa mithili ya meno ya mbwa. Ukuruba wao ulikuwa umekomaa na kupea ushirika zaidi ya damu na maji.

Si tetesi wala si tuhuma, wazazi wetu walijuliana hali kwa kupashana jambo sijambo kila walipopata wasaa wa salamu. Waliinuana migongo pindi maisha yalipowapindisha ovyo mitheli ya liundi angani. Walijengana kwa hili na lile. Ama kweli, walikuwa vioo maridadi kwetu kujiremba na kujipamba navyo. Kama si wao tungewaiga kina nani?

Walezi wetu walituchukulia kuwa wana watiifu kama watoto wa

bata. Kando na utoto wetu wa kuchupachupa kama tumbili, daima tuliwapa faraja ya uzazi wao. Tulibakia ange kwenye maagizo na miongozo yao siku zote. Tulijitahidi kuwa kwenye maelekezo yao. Wasemavyo Waswahili, '*mwana msikivu haonywi mchana kutwa*.'

Makusudi kando na kuwa mwandani wangu wa siri na dhahiri, alikuwa danga asiyetabirika kwa urahisi vile. Kando na kujitanua kifua kila mara, alikuwa mwingi wa sarakasi tena mwenye ucheshi kama chale jukwaani. Hakika ni mterehemeshi wa burudani.

Mathalani, baadhi ya matendo yake niliyakisia kwa kisebusebu na kila wakati, niliweza kuyatilia shaka bali si shauku. Sababu bora huwenda nisiwe nayo kwa sasa. Kwani usilolijua ni sawa usiku wa giza.

Alifahamika sana kama podo la mishale ya kuvunja mbavu. Wanafunzi na marafiki wenzake kama mimi, tulimtambua kuwa ziaka la ucheshi darasani na hata mitaani. Ufundi wake wa maneno mdomoni ulilitoa nje joka lolote pangoni.

Si Mapona si Masazoni si Mtemanyuki wala si kule kwengine.*"Tashi"*– jina lake la utweshi na utani, lilitawala anga ungedhani yu nyota au mbalamwezi pekee kwenye sayari hai. Kati ya wakubwa kwa wadogo na wazee kwa vijana, nani aliyekosa kumtambua apitapo au azungumzapo?

Bila shaka hakuwa mojawapo wa watu wa mazingira yetu. Utuvu wa ucheshi wake ulizaa taji kuu la kusifika kote kama sarafu za shaba. Alijulikana kwa vishindo radidi vya kumwachia ganzi tausi sembuse mimi na wewe. Hata majitu yasiyojua kutabasamu yangecheka mbavu kuvunjikia majifua yao seuze kuanguka sakafuni pu!

Alipozungumza tu, wengi wetu tulihesabu magego na masegego yetu vinywani huku mbavu zikituomba msamaha wa kupumzika. Tulicheka sana hata mara nyingine, tulidhani tumegeuzwa wehu kwa utani wake.

Hakuwa mkataa wengi kama mchawi. Hivyo, alikaribia umaarufu wa ngwenje za taifa lolote shupavu. Hulka hiyo ya kuziwacha mbavu za wenyewe bila salama, ilimpeperushia ufanisi wake hata zaidi licha ya kuwa angali mwana wa uchochole. Ulimi wake ulikuwa mwepesi kuchangamsha watu wa watu. Ninakubali ya kuwa, alishikika vyema kwenye talanta ya uchekeshaji na upevu wa akili shuleni. Kweli, Mungu *akikunyima hiki kakupa kile*.

Kando na hayo, tabia yake ya kupekuapekua mageni ilichangia pakubwa jinsi alivyo sasa. Alipenda kwenda na usasa ulioibuka mitaani mwetu. Alitangamana chanya na yeyote yule amjiaye bila ya kumpiga msasa kando na kujipiga darubini.

Mimi na ndugu mziwanda wake, tukawa kweli kinyume cha sifa zake. Unyamavu wa baibui kwenye utulivu wa utando ulikuwa bahari kubwa kwetu. Ulituteka nyara mara kwa mara. Tukawa wanyamavu kama shanga shingoni. Kutokana na hali hiyo, tulihofia kuwa nje ya nyumba mara kwa mara.

Mimi na Chachania.Tulijifunga nira kudurusu vitabu kila tupatapo mwia angalau tuwe wembe tamathali yake Makusudi.Vitabu vya hadithi havikuwa mbali na macho yetu. Majarida na magazeti. Vitabu vya kaida shulenu na vile shughuli za ziada, tulivipitia na kuvidurusu kwa muda na nafasi zetu. Matopa ya mabuku maktabani yakawa ghera machoni petu seuze moyoni mwetu. Isitoshe, tulienzi kusoma na kujiburudisha kwa kusikiliza vipindi vya elimu rungoyani na runingani.

Shuleni.Tulijitosa himahima michezoni kama njia mojawapo ya kupumzisha akili. Mchezo wa kandanda pamwe na mbio za riadha, zilituvulia boshori tuingiapo ugani. Miongoni mwa wachezaji nguli shuleni mwetu. Hatukukosekana kwenye dimba lolote lile la kuchabangana mabao faridi. Tukose tuchekwe! Abadani kataani! Sisi na michezo hii, si leo si kesho, tulibaki kuwa mamoja utadhania tumekuwa mapacha.

Tulipata ushabiki shakiki kati ya wanafunzi na walimu wa shule nyingi za viungani. Walitushangilia kwa vifijo na nderemo tele bimithili ya nyuki mauani. Ni furaha iliyoje kutajwa kama sifa kwenye vinywa vya watu. Tulihisi hisia nuzri. Bila shaka huko ndiko kulikuwa kwetu sudi na bahati. Isipokuwa kwake Makusudi, mtu na dunia yake mwenyewe. Alikuwa na ushawishi kuliko sisi wenzake.

Sio kwamba tulimchukia wala kumwonea gere sifa zake. La hasha! Tulimpenda jinsi alivyo. Kwani ni nani asiyegundua kuwa hakuna aliye kamili kuliko mwingine? Wasemavyo waswahili; *afadhali dooteni kuliko ambari kutanda.* Sote tulikuwa kama akilili angani. Tulimetameta kwa nyota zetu za kipekee. Ingawaje nyota ni nyota tu kama nyingine. Nyota ya Makusudi ilikuwa tafauti na zetu.

***

Majira ya macheo moja, Ijumaa, nikiwa darasa la nane mwaka huo. Chachania alifika shuleni akiwa mchovu na mwenye homa kama ng'ombe aliyesedeka kimeta. Kama sivyo, alionekana sawa na ng'ombe mwenye ndigana. Alikuwa ametamauka ajabu. Uso wake wa tufaha aliushusha chini na kujitundikia hijabu ya simanzi tele. nilipomtupia macho vyema, niliona ameshikwa na shake la kulia lililokuwa karibu kumbomoa kando na upole wake wa kila siku.

Mwendo wake wa kusuasua kama lumbwi vitagaani, uliniongeza shaka na wahaka chungu nzima. Alitembea kana kwamba alitaka kunyatanyata tu. Miguu ilimpitapita huku na kule mithili ya mtu aliyevurugika akili. Nusura nimdhaniye ameshikwa na akili sakarani.

Alikuwa hajijui wala hajitambui. Sababu yake kuwa vile sikuwa na mwao nayo abadani. Nilikisiakisia mambo tu. Niliona si kawaida kama sheria kwake kuja shuleni pweke.

" *Makusudi yu wapi? Mbona Chachania amepooza moyo vile Leo hii? Hakuandamana guu kwa guu na kaka yake Makusudi. Kulikoni*?"

Haya ni baadhi ya maswali yaliojijenga akilini pindi tu nilipomwangalia usoni ndugu ya rafiki yangu. Maskini, huzuni ilimtawala vibaya. Ningefanya nini jamani?

Mwaka huo huo, Chahania alikuwa ncha kali na hatari katika masomo ya darasa la daraja ya nyuma yetu. Haikuwa kosa wala dosari, hata si jambo la kushangaza mtu, shuleni kote, tukimshabihisha na wembe mpya uliotolewa kwenye kikasha kipya. Ilidhihirika wazi kuwa mtoto wa Simba ni Simba tu! Yeye na Makusudi walikuwa mashoka ya kuogofya daftarini na vitabuni. elimu iliwanata na kugandamana akilini mwao sawa na gundi. hawa ndio mwfano mwema wa wanafunzi waleteo tabasamu mbelel ya nyuso za walimu wanaotaabika kusomesha kwenye mavumbi ya chaki.

Kando na hayo. Nilijongeajongea karibu na mlango wao wa darasa la ***7A***. Darasa hili pia lilijulikana kwa jina la ***SABA AMBOSELI***. Nilipiga hatua chache hadi hapo. Nikamtazama Chachania kwa makini na wingi wa udadisi. Kisha, nikampa utweshi wa siku angalau kumjulia jambo na hali mwenzangu. hata nikamtania kwa jina lake la utani ili nimguse mishipa.

"*Chachania, Chewa ndugu yangu*!" Nilimsalimia kwa ustarabu huku nikivunjilia mbali kimya kilichoshiba kati yetu pindi tulipokutana uso kwa macho.

"*Chewa, Sadiki.U hali gani*?"Alinijibu kwa sauti ya kugunaguna na kugitagita.

" *Njema.Hivi mbona umesononeka usubuhi?*" Niliamua kumjulia hali kwa undani hata zaidi.

Chachania alitamka polepole tena kwa sauti iliyopasuka kati ya kuchuchua huzuni na kuhimili hisia zake. Akasema:

"*Sadiki, rafiki wa dhati, sijui nikwambie nini, lakini, Lisilo dawa halianguliki.... Maskini ndugu yangu mkubwa! Makusudi ameshikwa*

*na matata. Si yale yale tuyajuayo. Mara hii.... sijui… sijuii....siiijuuuii… sii.......*"

"*Sijui kama yu salama! Kha! Lini atakoma vitimbi vyake vya kujipalia makaa mwenyewe*? Hivi amefanya nini mara hii?"
Niliikatiza kauli ya yake huku nikiwa na Chachaniawizo nzito za kujenga picha ya hali ilivyompata Makusudi.

Hususan pale alipo kwa sasa. Dua na sala tu. Kwani sote tulimjua 'Tashi' (yuyu huyu Maksudi) kama ngisi. Hana mwelekeo dhabiti wa kupigiwa mfano kando na uhodari wake masomoni. Usalama wake ulitugawa moyo kati ya kulia kilio na kujishikia hofu. Hasara ilioje?

Kama rafiki wa mifupani, nilielewa fika kuwa pale alipo sasa Makusudi anahitaji si mkono wa usaidizi tu bali pia uvusho wa busara kuelekezwa kwema. Nilimgeukia Chachania ili kumsaili jambo fulani lililonifikia akilini ghafla kwenye msitu wa fikira zangu zilizofumukana muda huo.

Nilipomtazama na kumtupia macho, nilibutaa kiasi cha haja. Mwenzangu alikuwa anadondokwa na kukokomokwa na machozi bila kipimo. Alilia kwi! kwi! kwi!

Sikujua ya kwamba nimemchubua mbingu za machozi ya simanzi. Yale yale aliyokuwa ameyanyaria kwa muda mrefu. Chachania alichiririkwa na kububujikwa michirizi ya machozi huku akijikaza kisabuni kutolia. Alijikaza sana kilio chake kisijemtoka kwa nguvu kinywani mwake.'*Damu ni nzito kuliko maji'.*

Alishikwa na kwikwi wala usidhani ni utani. Nilijitahidi kwa kadri kubwa kumbembeleza na kumtuliza hisia. Jambo ambalo lilifua dafu baada ya nusu dakika za saa moja hivi.

Alipotulia.Alinichania soga waziwazi ya kisa kilichojiri jana. Alinieleza yaliokuwa hali tulipotoka shuleni siku hiyo jioni. Yale yaliofanyika darajani nilipobakia nyuma shuleni.

Aliyoyasema yaliniacha kinywa wazi kama changu aliyevuliwa kwa nyavu usiku wa manane. Nilibakia gogo la jiti bovu. Kimya cha

ububu kilinishika na kunitikisa mwili mzima. Hisia zangu zikavurugika kama maji yanayotokota mekoni. Mwishowe, nilikufa ganzi kwa kukosa kalima mudomoni.

Nilikuwa kimya, kimya sana. Nikitega sikio ndi! Maelezo ya kina yalimtelezeka kinywani ndugu yake mtu wa watu. Alinifafanuliwa bayana yaliomsibu Makusudi. Kama mjuavyo: *kilio huanza mfiwa, ndipo na wa mbali wakaingia*. ilibidi nijitadi kuwa makini.

Chachania alishika kasi ya kuyapakua ya paukwa na pakawa. Alinielezea bila ya kimuyemuye chochote. Kisa chote na masimulizi yote. Aliyamwaga mwa! Niliyotamani kuyasikia kutoka kwake kwa uhakika, yalinikaribia masikioni na akilini.

Nilimtegea sikio Chachania kwa makini sana. Hata wa leo nayakumbuka masimulizi aliyoyatamka kinywani na maneno yake ya ujanani ungedhania ni jana tu tulikuwa na kikao naye! Ninakumbuka alivyonisimulia;

'Muda wa kupambazuka, ulikuwa umegonga hodi na kongole. Hivyo, majira ya kucha yalianza kumea kucha kwa ukangaichi mwema. Siku hiyo, alivyonieleza mwenyewe. Chachania aliamka mapema kama ada yake. Alifanya hivyo kwa minajili ya kujiandaa ipasavyo kuja shuelni mapema.

Kama mtu mwongofu, alipiga bismillahi kwa dua nyerezi za shukrani kwake Dayani.Alimshukuru tena na tena kwa uhai, rihi na siha njema aliyoipokea siku hiyo kama jana na juzi. Chachania alijua eti, kutomjua Mola ni jambo baya sana katika maisha ya mtu. Alisema kuwa mcha Mungu si kafiri.

Ilikuwa siku ya kawaida ya kuenda shule kwa wanafunzi kama mimi na yeye. Pale nyumbani, alijikokota sana kuondoka sawa na mtu wa hirimu tawili. Kama hulka na silika yake, Chachania si mkimwa kama nduguye mkubwa. Vitendo vyake vya kobe havikumweka mbali na kuchelewa skuli kil siku. Sio uwongo kuwa, muda haukumsubiri ajitambue kuwa ameshachelea kung'oa nanga ama kufanya jambo fulani.

Vilivile, nguvu za kushuku ndege mbaya kutokea hapo kwao zilimwandama kila alipokuwa akitenda mambo yake. Hakujua hasa

maana ya hali hiyo. Ila siku hiyo, moyoni. Sauti ilimnong'onezea siri ya kuwa, "*lisemwalo lipo na kama halipo li njiani laja*. Si kwema leo... Sauti ilimwambia,

"Mzuie*! Mzuie! Fanya haraka wewe! Kimbia.Makusudi ana.... hana* ……!" sauti ya moyo wake Chachania ilimweleza na kusemesha kwa taharuki.

Kwa hakika hakujua adadisi wapi kukithiri kwa woga huu uliompata macheo hii. Hakuwa mtu wa kuupuza moyo wake. Alirudi tekani kumwangalia kakaye.

Alipofika alimpata kaka yake amejiandaa tayari kuondoka. Akamtazama kwa kina huku akiikumbuka sauti ile ya moyoni wake. Hakupata uwezo wa kutabiri chochote. Hakuona kasoro yoyote aliyonayo ndugu mtu. Aliendelea kumtupia macho kwa kina. pengine apate dalili chembe moja.

Macho yao yaligongana kwenye anga ya kuonana. Makusudi hakupenda jinsi alivyotazamwa na mdogo wake asubuhi hivyo. Macho ya Chachania yalimfanya ajishuku kuwa kuna jambo limemtumbukia nyongo. Akamkaripia.

"Wewe *Chachania! Unajua sipendi tabia hiyo*!" Makusudi alimfokea nduguye.

"Nimefanya *nini sasa! Nakutazama tu. Hivi hupendi kuangaliwa*? *Hutaki niseme u mtanashati leo? Hahaha*!" ndugu alimweleza mwenzake kwa utani huku akicheka kwa mzaha wa kumchezea kindugu.

Punde si punde, mama yao aliingia kutoka jikoni. Aliwaharakisha kuondoka pale nyumbani. Muda ulikuwa umeyoyoma na kutotoma. Akrabu za saa zilitoa taarifa hiyo.

"Haya*! Shuleni mara moja! Mkichelewa mtaona cha mtema kuni. Nikiitwa na mwalimu wenu.si mwajua? Haya mbiombio…Shuleni…Nendeni haraka*" mama mzazi –Bi Tumaini aliwaelezea wanawe. Mtu na ndugu yake waliondoka kuelekea Chumio. kijiji kidogo kilichositiri shule kubwa ya msingi iitwayo Chumio.

***

Siku ya fadhila zake huwa na asubuhi kunjufu. Laimba ya jua la matlai. Muda wa jua linapotoa jicho jekundu, wekundu maridadi kwa uhai wa siku nzima! Sawa na asemavyo mkongwe Ken Walibora,

kwenye kitabu chake; SIKU NJEMA.Siku hii kwa ndugu hawa ni kama mfano huo. Safari ya kuenda shule iliwapa mwao mtu na nduguye kuwa mazuri yenye chudi na sudi yalikuwa yanawasubiri shuleni Chumio.

Mipapatiko ya mbawa za ndege pamoja na mikorokocho yao kwenye vitagaa vya miti na majumba, kulikuwa ishara tosha kwamba kilichosubiriwa na kutamanika kuwa, kimekubali kuwatandikia mkeka juma hilo.

Kila waliompita njiani, alivaa tabasamu ya aina yake. Siku hii walijihisi wepesi. Walipiga gumzo la utani huku miguu ikiwasongeza hatua moja na kumalizia nyingine. taratibu mwendo wa kobe milimani. hata walikuwa wakicheka kila neno lililowaponyoka kinywani. Furaha iliwabembeleza hakika.

Baada ya mwendo mfupi wa bak bandika bak bandua, walikaribia kivuto cha ng'ambo yao. Walijiunga na makundi ya wanagenzi wa shule tafauti tofauti pale darajani. Mimi pia nilijiunga nao kutoka upande ule mwingine wa mbavu zao za kulia. Kiasha kuingia hapo kwenye mwendo wa tunga na tao hadi kule shuleni. Tulivuka kuelekea kwenye jumba la uhai wa elimu na nyota zetu za kesho – Chumio.

Njiani, msururu wa wanafunzi walioelekea shuleni ulizidi kumiminika na kuongezeka sawa na siafu waliochokozwa kwa maji moto. Halaiki ya watu waliowahi kazi zao lilipitana nao majira hayo kama kawaida ya siku nyingine ile.

Kengele ya kwanza kuingia shuleni iligongwa, ngo! ngo! ngo! Ikasikika mpaka kitalifa cha mbali. Si kwenye mabonde ya Masazoni si maghorofani kule Mapona. Mimi, Tashi, nduguye na wanafunzi wengi tuliharakisha mwendo wetu kufika shuleni. Binafsi sikuwa mbali na mwendo wao wa kuelekea shule. Kwa masafa macache, kila mwanafunzi alionekana akikimbia kuwahi darasa lake.

Siku hii ilikuwa ya kipekee hata kwangu. Nilivutwa na hisia za furaha kuliko majuma waliopita hapo awali. Nilijua wazi na kwa jahara kuwa, mambo furufu yatagonga hodi. Niliamini mengi ya siku yenyewe yatakuwa mema hivyo hivyo. shule ya Chumio ilijaa mihemko ya furaha wakati mwingine na siku hii imekaa nakutulia kama mojawapo. huenda roho zetu hazikukisia buraha bure. lipo jambo litapaua mbarika. roho zetu zilijaa raha isiyoelezeka lakini miili yetu ishikwa na hofu. tulikuwa tayari tumechelewa. mwalimu wa zamu hakuwa mtu wa kututolea meno hasa tusipozingatia saa inavyokwenda. adhabu yake ni

tanuri. ukiipata utashinda ukiiota hata usiku kama jinamizi. ole wetu tuliochelewa tena.

Macho yote yalipupia lango la shule la mabati makuukuu. masikio yalikita kutarajia ukali wa sauti ya mtu mzima. kimya. utulivu. tena ukimya mpana ukazidi. roho mikononi, tulipenyapenya hadi madarasani mwetu. kwa kimya kile kile tulichoingia nacho ndivyo tulivyojiweka sawa vitini na kuzamia kazi. tulishukuru Mungu kuepuka ghadhabu za bwana Kadiri. lakini tulifahamu kuwa si kawaida. mwalimu huyu amewashinda hata majasusi. hupeleleza hata asipokuwa karibu. machoyake yalitosha, akikutazama vizuri utajitoa kama umetenda mambo yako. siku ya leo hakuonekana. shughuli zilimbana pahali. Aha, kalenda ya shule ilinukuu kuwa leo ni siku ya tamasha ya muziki.

## SURA YA NNE

Ni mawio yale yale kangaichi. Asubuhi ya siku ya ndovu kumla mwanawe. Siku ambayo wengi wetu husema hivyo eti. Walakini mimi nitakiri kuwa ni siku na ukuu wake. Siku hii ilikuwa imetukaribisha sote meza moja, wakubwa kwa wadogo, vijana kwa wazee, jinsia kwa jinsia tena kwa furaha na mahanjamu bila kifani. Walimu wetu wote walikuwa mbioni huku na kule kutupiga msasa vilivyo. Tulikariri na kuimba. Si mashairi si nyimbo za kitamaduni pamoja na densi za kukosha macho. Tulijipa ari za jihadi na sabili kabla ya kujiwakilisha jukwaani.

Kwa hakika na yukini, juma hili la tano lilikuwa tayari kutumwekea njota za jaha. Huu ni muda tuliousubiri utuvutie heri angalau tuwe na tabasamu na kumbukizi kwa siku zijazo.

Kila mwanafunzi alijiwekea ari na ujasiri wa ushindi na matumaini ya kuwapiku wapinzani wengine kwenye tamasha la muziki. Ninakumbuka tulivyoyavulia nguo maandalizi hayo kwa bashasha na ghera ya ajabu. Hatukutaka kubaki nyuma kama chura wa kuchupia ovyo mafuta moto. La hasha!

Basi la shule lilingurumishwa na dereva wetu, Bwana Msafa.Shule nzima ilikuwa na upeo wa buraha kama maarusi wanaotia ngosho siku yao ya kufunga ndoa. Wanafunzi wa madarasa ya chekechea walionekana kila mara wakichupachupa huku na kule kwa furaha ungewadhania wamegeuka ndegere chaani. Kumbe ni raha na bashasha tu.

Wengine walijipa majukumu ya kulipakia basi kwa masanduku ya maleba na mabodi ya kugiza. Kwingine, kikoa cha waimbaji wetu kilikuwa kingali uwanjani kilituhakikishia ushindi bali si ushinde.

Kila mmoja wetu alijua wazi tutakuwa tembo wa nyikani mara hii. kiboko yao. Kwani haikuwa mara yetu ya kwanza kujitosa himahima tamashani. Hapana. Ulingo wa tamasha hizi ulitufahamu vyema kama sarafu za chuma. Sisi na midundo yetu. Tulielewa fika ushindani uliopo na tulikuwa tayari kupambana jino kwa ukucha.

Waama kwa waima, sisi kwa sisi, ungetuuliza namna vyumba vya mioyo yetu vinavyojenga hamasa na kujijusuru ungetupa itikio la 'msasi haogopi miba. Mazoezi ya kupiga jaramba yalitukolea kama shira ya vitumbua. jasho la majijasho lilimwegika na kutitirika miili ya vijana wa damu changa. Damu ilio na uwezo wa kususuma milima na majabari, alakulihali. Iwe vipi shindano la siku moja litubabaishe.

Tulifahamu kabisa ya kwamba lazima tutakumbana na wanafunzi wengi kama sisi ambao ni simba wa majukwaa kama sisi. Ilitupasa tujizatiti kudhihirisha kwamba tupo mahiri zaidi ya chui.

Kengele ya mgambo shuleni ilipogongwa, kila mmoja wetu alinyambua nyayo zake hadi gwarideni. Hii ilikuwa ishara tosha kuwa kuna mbiu ya mgambo.

Mwalimu mkuu, Bi. Sonia alisimama kititi kadamnasi yetu. Tabasamu iliomvaa usoni, ilimpunguzia kunyanzi za uzee ulikuwa ange kumpokonya ucheshi wake. Ijapokuwa ana hirimu ya makamo, alipenda kukaa kama mtu mwenye ujana na usasa. Si kwa mavazi. Si hivi wala vile. hata maongezi yake mara nyingi yalikuwa na ujana ndani yake.

Alikuwa ameshiba furaha iso na kifani. Sisi tuliomtazama kwa kina, tulikadiria kwa umbali maana ya furaha yake. Tulijisemea tu kimoymoyo.

"*Leo kuna mazuri! Labda tumeshawapiku mahasimu wetu wa toka jadi! Yamkini, shule ya Kidoa huwenda wasihudhurie kigoda cha kuchunana ngozi ya umahiri tamashani! Mambo yatakuwa rahisi kama….*"

Mawazo yetu yalikatika ghafula pindi sauti ya Bi Sonia ilipojitokeza hewani.

"Wanafunzi *wa Chumio, mpo? Nawapa salamu zangu za dhati, Hamjambo? Naam, namshukuru Mungu kwa mengi aliyotufungulia na kutujaalia sisi sote. Si ukakamavu na ujasiri si busara na ukarimu. Hata kuifikia leo na kuiondokea jana ni kudura zake. Sote tusadiki – Amina!*

*Ahaa, siku ya kiu kuramba asali, kwetu imefika kwa nehema kuu. Tumekuwa tukiisubiri kwa unyenyekevu mno. Ama siyo? Nami naungama kuwa hayawi hayawi huwa.*

*Leo, tunatarajia vitu vya taanasa na azizi kwelikweli. Kwanza, ni tunzo bora ya muziki na pili ni ushindi wa kishujaa. Je, mna ashiki kwa vitu hivyo viwili? Mtavileta papa hapa gwarideni? Hakika. Sote tuna matumaini kuwa mtafanya hivyo*

*hivyo. Inshaallah.*

*Isitoshe, fungu kubwa la wanfunzi wetu watakuwa kwenye michuano bambam kule Bomamali.Bomamali ipo jijini Mashombo. Watapambana jino kwa jino, watajitahidi vilivyo pamwe na wenzao kuko huko ukumbini. Ninachukua fursa na satua hii, kuwatakia mema na ushindi wa mizani.*

*Kando na hayo, hatukuvishwa kilemba cha ukoka na walezi wa zamani waliponena kuwa; alimaye mtama havuni kunde. Sio? Mtahadhari sana. Hamna faida! Hatutapata hata riba ya tunu tukitenda yasiofaa wanangu. Hususani, kuvunja sura nzuri ya tabia na maadili. Hapana, tusifanye hivyo. Muwe watu na heshima zao popote pale.*

*Mara nyingi, sisi wenyewe hujisababishia mambo yanayoishia kutudhuru tena. Tunavunja sheria, tunakataa kutii, tunatia hamsini zetu katika ilani na maagizo ya kutusaidia sisi wenyewe. Tunawashawishi wenzetu kutenda kasoro. Kwa nini? Baadaye tutamlaumu nani?*

*Ebu mtazame aliye kando yako. Si nyote mu mamoja. Sare yetu ni moja. Basi mtu asikuongeze kitu kibovu wala usimpunguzie maadili mema. Hivi, tunasahau kuwa aliyemfunza chui kula watu ni binadamu? Ndiposa ninawaeleza bayana, akili kali si akili akali! Jijue wewe ni nani.*

*Tafadhali msiwe wana harashi wala wenye vitimbi kokote mliko. Nawasihi jamani. Daima majuto ni mjukuu na huja ……Sihitaji wanafunzi wenye vishungi vinavyokaidi maji! Mkumbuke ninyi ni vioo wa shule na jamii yetu. Nidhamu na*

*taadhima ndio msingi wetu hapa.*

*Usidanganyike kuwa mtundu kama mkia wa mbuzi ukaishia kuwa mgwisho matopeni tu! Utatuchafua sisi na usafi wetu wa pamba! Kila mmoja wenu ana jukumu la kujitunza. Nitafurahi nikiwaona watunzi wenye busara. Kumbuka sana kwamba maadili ni msingi kwenu.*

*Hewala, mnapofika huko, muiwambe ngoma ya kushinda bila wahaka wala woga. Si mnajua kuwa mbwa wa msasi mkali ni wakali pia? Mungu awe nanyi. Asanteni sana.*"

Bi. Sonia alimaliza kauli yake. Hotuba yake isiotumia kejeli wala mzaha ilitukaa na kututulia tuli akilini na kupenyeza masikioni bila nta wala komango kuibari. Yalikuwa mazoea yake Siti Sonia kutumia lugha ya Kiswahili kwa ufasaha na ufasili wake kila anapozungumza. Kimombo alikitumia sana wakati hasira zimemkaa vibaya kooni.

Ingawa mara nyingi alitufumbata na kutufumba kila alipotuhutubia, kila mmoja kati yetu alishika kwenye kolezo za bongo kuwa jungu kuu halikosi ukoko. Kwani tulipojirudi na kuzitafakaria kauli zake, tuliona busara yake.

Baada ya kuhutubiwa gwarideni, tulijiandaa kwa kuliabiri basi lilokuwa likitusubiri karibu na lango la shule. Tuliingia kwa utaratibu. Mmoja baada ya mwingine.

Tulipoingia sote ndani na kutulia, Bwana kadiri alituongoza kupiga dua kwa minajili ya safari hii iwe ya saada na sudi kwetu sote. Mola wetu atuondolee nuksi na nakama alakulihali. Alipomaliza.Mzee Msafa aliushika usikani.

Aling'oa nanga kwa ustadi wa kipekee. Basi letu likachanua lami kwa madeko na maringo.Kufumba na kufumbua,chombo chetu kilikubali tweto na tuto za mwendo.Kitalifa na masafa  yalipungua polepole.

Safari ya kwenda Bomamali imepamba moto. Bomamali ni maeneo mojawapo kati ya mengi yaliomo jijini Mashombo.Ilikuwa mara yetu ya kwanza kufika Bomamali na viunga vingine vya Mashombo.Kwa muda mrefu, tulizoea matamasha haya ya Muziki

kufanyika Mapona, Kichakamkwaju au hara ya Masazoni pekee.

# SURA YA TANO

Cheba! Tulipofika na kuwasili ukumbini, tuliweza kujumuika na wanafunzi wenzetu wengine waliotutangulia kupiga kikao cha kusana almasi kama si dhahabu. Mkururo wa bashasha na buraha hazikuadimika kati yetu wakati huu. Tuliwaza na kuwazia hatima yetu siku hii. Nikikisia, kila mmoja wetu alififikiria wazo lenye thamani kubwa bimithili ya senti za shaba – kupata hadia pamwe na ushindi.

Ukumbi ulikuwa umejaa chordo kwa watu walioiva sura za pashawa na ujasiri huku mazingira yote yakionekana ya kupendeza na kuvutia mnaso wa macho na moyo sawa na ming`ao ya vilimia angani.

Shamrashamra za siku ziliendelea kujipasha moto. Jukwaa lilikuwa ange kuwapokea wanafunzi wenye vipaji vyao. Ushindani mkali sawa na vita vya nyati ulianza rasmi baada ya kikao kifupi kati ya wanafunzi, walimu na washirikishi wa tamasha lile.

Upo wakati Makusudi alianza kuwa lumbwi wa vitagaani. Alibadilika na kuwa mwingine kulingana na muda ulivyozidi kuyoyoma na kuchimba idadi ya saa. Tulikuwa tumejibarizi ugani angaa tukisubiri muda wetu ufike kiungia kwenye mimbari.

Alifanya vitendo tusivyovielewa azali yake. Kuna muda alichangamka na kukaramka sana mithili ya mhalifu sugu aliyejipata huru ghalfa. Akabubujwa na maneno tumbi nzima.

Mengine yakihitaji huduma za wafasiri na wakalimani mahiri! Hatukumweleza kamwe. Tulibaki kusadiki kwamba, ‘*usilolijua ni sawa na usiku wa kiza kaniki*’.

***

Upande mwingine, sisi wanafunzi wenzake, alituchukulia kama wafumbatia moshi; watu wakupumbazwa tu hivi hivi. Alichangia soga

letu kwa nafasi yake japo kulikuwa na shughuli nyingine alizozipa kipaumbele. Shughuli hizo zilikuwa siri ya wachache.

La kutustaajabisha na kutuvua midomo hata zaidi ni kuwa, hakuwa peke yake katika hali ile. Takribani wanafunzi ishirini na wawili hivi walikuwa kwenye kikaango kimoja naye. Walipitapita vijia vyao vya siri. Huku na huko walizingazinga kwa shughuli zao.

Walipayukapayuka maneno bora kwao kutamka. Kundi waliloliunda chini ya mti ulio mkabala wa ua ya bwalo, lilizua maswali mengi kila tulipowatazama. Waliyoyafanya pia yalitufumbata mwao kabisa. Sherehe na vifijo vyao havikueleweka. Ilikuwa ni kupokezana vitu faraghani na kisha kuanza kucheka vicheko vya fisi kumkejeli tembo nyikani.

Kumbe kivuli hakionekani usiku! Hatukuwahi kugundua yaliojiri kati yao. Sisi wengine tulibakia mashabiki tu wa miamo na vicheko vyao vya mastaajabu makubwa walivyovichanga ovyo ovyo kila walipopishana nasi. Labda kwao walikuwa wanashangilia michemko ya jukwaani ila kwetu tuliwaona wenye kasoro si katiti. Tulikuwa mbali mno na jukwaa iweje wanacheka yanayojiri huko!

Mpaka sasa, hatujui walikuwa wakishangilia nini hasa. Kwani sote hatukuwa makini wala ange kufuatilia matokeo ya hadhira na wawasilishaji.

Kando na hayo, Makusudi alijigeuza kuwa mwana wa kambo, mkaidi zaidi kati yetu pamoja na wale wafuasi wake. Kila baada ya mida isio mirefu, alijibari faraghani pamwe na vijana hao hao tusiowajua wala kuwafahamu kwa asili na usuli.

Pengine walikuwa wanafunzi wa shule zilizo majirani na Chumio.Wachache tulioweza kutambua sare zao ni wanafunzi wa shule ya msingi ya Kerodonda iliopo Kichakamkwajuni.

Kwa upeo wa macho yeyu, tulitathmini kuwa, huwenda

wanapokezana lawalawa mbili tatu kwa njia ya uchoyo tu. Mbona basi atusahau sisi marafiki wa toka nitoke?

Pengine alifanya hivyo kutunyima sisi. Labda alitaka tushikwe na gere ama tumshikie kinyongo. Hayo, yalisalia kwetu kama mkeka uliokunjwa zamani na kikao kuvunjika bila habari. Hatukuyalia maanani kabisa.

Vijana hawa – mabanati na maghulamu, walizidi kupishana njiani kwenda pale alipoketi Makusudi.Walifanya hivyo kwa nyakaa za saa tatu hivi.

Hadi sasa, alikuwa ameketi chini ya mti wa mkawini. Wote tuliowatazama kama sinema, walionekana kuwa na ngozi ya utundu kama tandu na cheche. Walishiba shibe ya utukutu mithili ya wana wachuro.

Kwa udadisi na upekuzi wetu mdogo, tulikosa kifua cha kuwauliza hayo yao. Kama tujuavyo; '*pilipili ya shambani yakuwashiani*'. Hili lingekuwa pigo lao kwetu bila shaka. Waama tuliafikiana sisi kwa sisi kwamba, '*aliyekaza uta mwondokee'*.

Tulijitia hamnazo japo kimoyomoyo tuliungulia ashiki ya kutaka kujua weupe wa pamba kati ya tano ya chokaa nyeusi tititi. Ni ukweli kuwa hatukuweza kuchunguza kilichofichika kati ya vijana wale na Makusudi.Hivyo, tulikubali eti wamekuwa wajanja wa kila jambo walitendalo. Waligeuka wasiri kama makaburi ya mabaniani.

Ghafla bin kichea, jina la shule yetu lilitajwa na kuangaa hewani kutoka kwenye kipazasauti. Mshereheshi alikuwa akipiga mbiu kama ada yake. Wito huo ulitugutusha kuwa tunahitajika mara moja kwenye jukwaa pasi na kulegeza ratiba ya siku.

Sauti hiyo ilikuwa mojawapo ya kanuni za kumbini ambazo hatukuwa na budi kutii alakulihali. Tulijikusanya kama vichala vya

zabibu. Tuliitana mmoja mmoja ili tuelekee ukumbini.

Vilevile, mwalimu wetu – Bwana Kadiri kama kawaida yake hakosi kutuchunga kama wachungwa. Alikuwa tayari anatusubiri kando ya mlango tarabe wa ukumbi huo. Alikuwa hapo akitupungia mikono himahima. Alifanya hivyo kutuashiria na kutuelekeza twende pale alipo bila kusitasita wala kugitagita. Nasi tulimwarifu mwenzetu mwenye shughuli nyingi –kuwa tunahitajika mara moja. Kisha sote tukaelekea kwa mwalimu wetu chapuchapu bila kunyatua miguu kwingine.

Tulipomkaribia, tulisimama dede kama kigaro cha wanajeshi kwenye gwaride. Tulikuwa pacha kwa walinda nchi wanaosubiri amri ya jemedari wao. Hatukufaa kuwa kitalifa kama kile. Tulikuwa tumevunja amri moja ya Bwana Kadiri ambaye tulifahamu uwezo wake wakuturudi popote aonapo panafaa marudio!

Kwa uhakika wa kukisia kwetu, Bwana Kadiri alikuwa karibu kuungua sura kulinganga na jinsi alivyotutazama. Tuliona miale ya mori na hasira zikitunyooshea vidole. Mishipa ya wahiji ilitamani kuwa viboko! Tulijua wazi kwamba kichapo cha mwana mtundu kinaweza ibuka muda mchache kama bomu la atomu na kulipuka ‘*Buum*!’.

Hapa ndipo nafikiri sote tulijishusha kwenye sala na dua za kila namna bila kikomo. Tulimwelewa sana Bwana Kadiri kama mtu asiyependa mzaha katika jambo lolote lile hata kula.

***

Kwenye Afisi ya Walimu, mara nyingi tulimwona akila bila kutabasamu seuze kucheka au kuchangia mazungumzo ya wenzake wakati huo. Hata alipokuwa akisahihisha na kuzipitia insha zetu hulka na silika yake ilibakia ile ile – Mzaha kando.

Haya tuliyajua na kuyabaini kila tulipopata nafasi ya kuingia huko. Sote tulijua yatakayojiri muda si mrefu. Na sasa, alitutazama

kidogo kisha akafungua kinywa kuzungumza ili atueleze yake.

“Mbona *mnachukua muda mwingi sana kuja hapa? Mwajisahau sivyo? Ni kawadia tu kama sheria kutii amri. Sasa…. Mlikuwa huko mbali mkifanya nini? Wewe Makusudi na wenzako, mna nini leo*?” Bwana Kadiri alitukaripia.

Alifoka kwa ghadhabu na kero tawili huku ametukazia macho ya bundi. Hata hivyo, alikuwa angali hajakasirika sawa na mkizi kama tulivyodhania awali. Tungaliona tanuri la moto nyikani.

Sote tulikuwa tumenywea kwa hofu na shakawa ya kuonjeshwa adhabu. Hakuna aliyethubutu kunyanyua hata macho kumtazama Mwalimu Kadiri.Kwa bahati nzuri, tulipata uwezo wa kumshawishi kidogo.

“*Samahani Mwalimu, Bwana Kadiri.Tuwie radhi. Kule tulikuwa tunaitana ili…ili…*” ndivyo kauli yetu ilivyotoka na hatimaye ikatizwa ghafla.

“*Ili jambo gani lifanyike? Ebu jiandaeni haraka. Hayo yenu mtanijibu baadaye. Shuleni. Kwa sasa makinika mna kazi kubwa. Sawa*?” Alituamuru kwa sauti ya radidi kama samba.

“*Naam*!” “*Labeka*!” Tulijibu huku tukifumukana kwa utaratibu kuelekea kwenye vyumba vya mabadilisho, ambako tungelivaa maleva kabla ya kuingia jukwaani. kauli yake ya mwisho, ilitutia ari sana. Ilitufufua na kututuliza. Moyoni, tuliamua kumtendea haki. Lazima tuutafute ushindi.

Tuliingia kwenye ulingo wa mapambano bila woga. Tulijiwakilisha kwa utausi naushoerewanda wote tulifundishwa almuradi kinyang’anyiro kitupatie haki ya ushindi. Matunda ya mbwembwe zetu zilidondoka kama matone ya asali.

Waandalizi wa tamasha walikubali ubabe wetu. Waliona ufundi

wa kazi tulizozileta kadamnasi yao. Hadhira haikubakia kuwa mfuko wa kanzu, walishangilia kwa shangwe na vifijo kila mara tulipotia ondo jukwaani. Kwa yukini, siku ilikuwa yetu kujitaja wafalme.

Bwana Kadiri alifurahi sana nusura ya tabasamu kugeuza mwehu. Alirukaruka kwa nderemo tele. Huu ndio wakati Makusudi alibahatika kuwa mtende wa siku.

Alipewa tuzo yetu na alijipata amebebwa hobelahobela huku vicheko vya kwa! kwa! kwa! na sherehe vilipasha moto ukumbi mzima. Hadi sasa mahasimu wetu walikuwa wametulia kando. Ushinde wao waliukubali japo kuna mara nyingine ya kuwania.

***

Tulirudi shuleni na ushindi wetu. Shangwe na nderemo seuze vigelegele vilitanda pembe zote za Chumio.Bi Sonia alijumuika kushangilia nasi. Uzee wake aliutupa kando akashika miondoko yetu ya ujana. Tuliimba nyimbo za majigambo na ushindi wakati Bwana Kadiri alikuwa anamkabidhi mkuu wake tunzo ya Tamasha la Muziki.

"Chumio *ee Chumio haa! Chumio kiboko yao!*

*Hawakuwezi hao! Chumio kiboko yao!*

*Chumio ee Chumio haa! Chumio kiboko yao!*

*Kiboko ee! Kiboko haa! kiboko yao!*"

Tuliimba kwa sauti kubwa na yakujishanua nusurakujitifua kama mavumbi ugani. Maeneno jirani na shule yetu, yalikaribia kutupa pongezi zetu. Wanafunzi na jamii nzima ya Chumio walimeza mate ya kulegeza furaha iliwashiba miili yao. Wakucheka walicheka. Wakuimba waliimba. Wakuruka walirukaruka kwa urefu na ufupi wao. Shule ya Chumio ilibaki kuwa mwamba kote hadi jiji la Mashombo.

Bwana Mwamba – Gavana wetu, hakuchelea kutupa mkono wa

tahania. Alikuja kwa mbwembwe tosha kama mwamba kweli. Hidaya za kukosha macho na mtima alizokuwa nazo siku hiyo, zilituacha hoi wa shakiri na bashasha tumbi nzima.

Kifani cha uterehemeshi kilifika kilele majira yale ya jio. Ingawa tulitamani kuendelea na sherehe yetu. Kama wanafunzi walioshiriki ushindi ule, tulipepea kwa raha kujua kwamba tumewabwaga mahasimu wetu wa jadi –shule ya Kidoa.Tuliwashida wote hata wale wa shule ya msingi ya Kerodonda waliopenda kujigamba kama mamba wa mto Marambo!

Bwana Kadiri alibembea na walimu wenzake kwenye ufahari wa kuipandisha shule yetu katika hadhi kuu mkoani mwetu Mapona.Ushindi huu, ulidhirisha dhahiri shahiri kwamba shule ya Chumio ni ngazi bora kihali na mali. Daima tuliipenda kwa dhati shule yetu kando na ushindi wetu wa siku hiyo. Siku ilikuwa siku, hata bwana Kadiri alitusahau! Alisahau kuwa tunafaa kumpa majibu ya kisa cha utundu wetu kule Bomamali.

## SURA YA SITA

Maisha ya shuleni yaliendelea kwa kasi na kwa ukawaida wake. Kudamka kila siku kulikuwa ni ada ya kila mwanafunzi wa enzi zetu. Walijipiga msasa masomoni. Kila mmoja akijitahidi na kujizatiti kupiku alama bora. Walimu wetu walikuwa mbioni kutufundisha yaliomo kwenye silabasi. Mambo yalisonga hivyo kila uchao.

Kando na siku kugeuka kuwa miezi, Makusudi alikuwa mwingi wa kugeuka mambo, si kitabia tu bali kimazingira pia. Kuwa kwake kinyonga halisi haikuwa taabu wala janaa. Upo wakati aliaanza kuwa mtoro asiyefika shuleni kwa visingizio vyake visivyo na mbele wala nyuma.

Hasa siku za Jumanne, Alhamisi, Ijumaa kando na wikendi. Aliadimika ipasavyo skulini. Yeye na ndururu – sarafu za jadi walikuwa sawa na siku kama hizi. Tulio karibu naye, tulimkubali kama mtu wa misimu. Waswahili hawakunena yaliokwenda upogo kuwa, mtu huadimika kama wali wa daku. Sidhani kama waliweka msondo kauli hii. Walituchemsha bongo sawasawa.

Kuondoka kwake ovyo shuleni, kulifumbiwa macho na wengi. Si walimu si wazazi na hata si sisi kwa sisi – wanafunzi wenzake. Madhali tulidhani anaenda kwa matibabu kule zahanatini. Mara kadhaa amekuwa akishadidia kama si kusingizia vile macho yake yalimpa kero si haba.

Sababu kuu ya sisi kutotilia maanani sana kuwapo kwake shuleni ni kwamba, alikuwa na ubora wa kutahinika kuliko sote. Hata aliporudi siku kesho, alama zake kwenye mijarabu zilituonyesha kisongo chake.

Makusudi ni gwiji wa mambo mengine mengi kando na masomo. Bila kusahau, yeye ndiye chale aliyeiletea shule yetu tuzo la kitaifa! Tuzo la mwigizaji bora lilikuwa lake siku ile ya mashindano. Tunzo ya mwanafunzi mshairi halikumkinai kamwe, pia alilizoa ile ile siku. Bila kusahau hiba na adia ya mwigizaji stadi. Tangu awe

mwanagenzi mbichi kule chekechea, amekuwa mvuto wa fanaka katika shule yetu.

Alitupofusha kwa mapovu ya uzuri wake ilhali alikuwa ana makovu ya tabia pia. Walimu wetu walikosa kumpiga darubini kwa kina kuhusu jambo hilo. Kila mwalimu alimshangilia kuwa johari wa mtihani na michezo. Hakuna hata siku moja, walimu wa Chumio walifaulu kugundua madoa yaliojipachika kwake. Sababu? Alizoa maksi moto moto hata kwenye mitihani iliokuwa mawe.

Kila aliporudi na kuukalia mtihani, tuliliona wingu lake la ufanisi. Alitupiku kwa alama mzomzo hata tukakosa la kusema wakati mwingine. Alitifua alama za ushindi hadidi kwenye mitihani yote tuliowahi kuifanya. Aligeuka shoka lisilohofu gogo lolote la mijarabu. Yote angeyachanja vigae vigae na kuyabandua bandu bandu.

Kando na yeye mwenyewe na mambo yake, kulikuwa na wanafunzi wengine walioiga hulka yake ya kutoroka shule. waliyumbayumba na kumfuata kama bendera kwenye tufani. Kila muda wa shule ulipowalegezea kamba. Walinyatuanyatua nyayo hadi msalani. Huko, walizivua sare na kuvalia mavazi mavulia kisha kurudi mitaani bila tahadhari ya walinzi wa shule, walimu sembuse wazazi wao. Walipenya huku na kule kwenda kutenda waliofundishwa na mwenzetu –Makusudi.

Kata zote za Mashombo zilimvulia kofia Makusudi, mwana wa famila duni. Aliyebobea kwa ufasiri unaohitajika kwa kila mwanafunzi aliye shuleni. Nusura tumshawishi Rahmani kwa dua atugeuze tuwe kama Makusudi! Ila hayo hayakutimia katu. Tulishinda mbali ashiki za nyoyo zetu. Tulijikubali jinsi tulivyo. Laiti wengi wangalijua ukweli usiofichika kati ya ngozi yake huyu mwenzetu, sijui wangalisema nini!

Ungewauliza washika dau na wahisani wa maeneo yoyote yale, wangekwambia kwamba Makusudi ni nehema kubwa. Watakueleza kinaganaga kuwa anafaa ajizatiti zaidi masomoni ili awe kielelezo

chema kwa vijana walio nyuma yake. Asa kwa ndugu yake Chachania pamoja na walioishi kwenye nyavu za uchochole kule Masazoni, Mtemanyuki na Kichakmkwaju.

Kila mtu alikuwa na imani naye. Walezi wengi aghalabu walipata mtu wakuzungumzia na kuwausia wana wao. Si mitaani si majumbani. Alikuwa fahari kote na kwa kila mtu.Lakini hata sisi hatukusahaulika.Tulihimizwa kujitia nira kumfikia rafiki yangu.Mawazo ambayo tuliyafanyia kazi kila siku ijapo kwa umakinifu mwingi.

Upo wakati Bwana Kadiri aliniita Afisini pake. Nakumbuka alikuwa mkuu wa idara ya Kiswahili.Alinipa mshawasha wa kung'ata si bidii peke yake bali aliniongoza kupata mwongozo wa maisha yangu ya sasa. Alinipasha maarifa yalionifaa na kunikaa hadi leo. Hakika yalikuwa moto wa vifuu vya nazi.

Kuchemka kwangu kwa ari, kulifungulia mwanya wa kumwonyesha Makusudi kuwa hata papa wapo. Somo la Kiswahili na Hisabati tulishika alama sawa kwa mithani yote ilifuata. Kwake haikuwa jambo la kushangaza kwani masomo hayakuwa moyoni mwake. Dira yake ya macho ilichunguza kwengine. Kule ambako sisi tulikuwa kama vipofu tu. Huenda tulikufungia macho tu.

Hata mimi nilianza kugundua ya kwamba nimepoteza rafiki wa zamani. Mwandani Makusudi hakuwa yule wa zamani tena. Amebadilika na kuwa mchachu kama maji ya bahari. Nilibaini kwamba hata yeye hana shughuli na urafiki uliokuwa kati yetu. Hatukuwa na malengo sawa tena maishani. Kila mmoja na yake.

Haidhuru kwa hayo, lipo lililonifuta chozi la moyo, Chachania alichukua njia yangu. Alizidi kung'aa zaidi kuliko nduguye. Kwa sababu ya upole wake, ilikuwa vigumu ajulikane na umahiri wake kama Makusudi.

Nilipotambua ukaribu huu, nilijipiga moyo konde kuachana na Makusudi aliyeshikwa na yake. Niliupangua urafiki na kuuendeleza usena upya kati yangu na Chachania.

Siku zilipozidi kwenda mbio. Muda ulijipeperusha kama mchanga ulio kwenye shisha. Rafiki Makusudi alionekana kusumbulia na mengi akilini mwake japo hatupakulia kwenye sahani sisi wandani wake.

Labda ni kwa vile hatukuweza kumtabiri vyema kama majira. Labda siri zake hazikumruhusu afanye hivyo hata ikiwa alitaka kutupusulia waziwazi yaliomchoma kama miiba. Vitimbi vyake vilijieneza polepole. tulipoanza kuuona mkondo wake. Tulichukua muda wetu kumshauri mawili matatu ijapo alipuuza na kuutupilia mbali.

Makusudi alisahau kabisa kuwa *mchezea zuri na baya humfika*. Ama ajuayekutafuna nyama ajifunze kugegeda fupa. Uhodari wake masomni ulianza kushika masizi mazito ya kuzembea kutokana na ushawishi wa marika. Ari ya kukinai shule ilianza kumkoloea mwili mzima. Hakuwa tena na ari na nia ya masomo. Tayari alikuwa ametekwa na tusioyaelewa. Yaliomshika hakika yalikuwa kama mizimu. Yalimpeleka mbio kama kichaa.

Aidha, wosia tuliompa kila mara ulimgeuza kuwa Masito mwenye usito mzito wa kipekee. Alitusikiliza kwa kina kando na umakini ingawa hakuyabebea shoka tuliyomwelekezea kama nasaha.

Aliyapuuzilia mbali. Nasi tulibaini kuwa ameshajipa kilemba cha mgema aliyesifiwa na tembo kulitia maji kitambo. Mara nyingine, tulipojaribu kumpa akili zetu, alikasirika sana nusura kuzua zahama ya kuchunana ngozi.

Mimi na Chachania tukaamua kumwachia njia yake ajisafirie mwenyewe ili kuepuka ugomvi huo. Kwani sote tulijua ya kwamba,

*rasharasha ni mwanzo wa mvua*. Ipo siku. Ipo siku mambo yatachimbika na kufumbuka wazi hadharani.

Mama yake hakukosa nasaha mbashara. Alimjuvya peupe mara kadhaa. Makusudi na kusudi zake alitanabahishwa kuwa makosa yake yatamshutumu yeye bali si mwingine. Kila alipoteleza kwa tabia alikumbushwa hivyo. Kuwa mtenda lake lijapo kooni hulimeza mwenyewe.

Hawakuchelelea kumrudi palipomfaa bila kumpa ya kumshaa. Bila shaka, walimaizi kauli ya zamani isemayo, mchelea mwana kulia hulia yeye. Mathalani, mtoto akibebwa hutazama kisogo cha ninaye. Mama mtu alijitahidi kumkanya na kumnyoshea kidole. Mama mtu alimkanya sana.

"Mwanetu. Makusudi*. Nakuona wabadilika kila uchao. Muda mwingine hausikii lolote uambiwalo; mbwa nambwa kafiri wa nyani! Ipo siku utakosa pa kupiga magoti. Ebu jichunge. jichunguze vyema mwanangu. Usimfanye baba yako kuwa mwehu, kichaa kasorobo. Atakumaliza kwa vituko vyako hivyo. Nafikiri wamfahamu na yake*?" Mama mzazi alimweleza kwa utu licha ya kumkaripia.

Makusudi alikuwa mkono wa kulia. Hivyo, wazazi wake walimpenda ukomo wa upendo wao ingawa mwana wa mifupani alikuwepo pia. Kitindamimba alibaki kuwa Chachania.Wavyele wao walitia juhudi kukimu mahitaji yao ya msingi.

Walifanya hivyo kwa kudura na uwezo wa Mungu wa kufuta vumbi msala wa ufukara uliokubali kuishi nao milele.

Shuleni.Si mara moja ya kuhesabika. Tulipata kinywa cha nasaha kutoka kwa Mwalimu Kadiri.

"*Pele haligeuzwi jupi, kila binadamu ana udhaifu wake kila mmoja wenu ajaribu kuujenga uduni wake kuwa bora. Najua mwaweza.*

*Tafadhali maisha yasiwaangushe kingalingali. Shika tahadhari yako!*”.

Alipenda kutunasihi hivyo ijapokuwa hatukujua ni kwa nini alitueleza sote ilhali ni mmoja wetu aliyekuwa tenge. Ndivyo nilivyodhani. Mimi na akili zangu wakati ule.

Kando na dua tulizotia mimi na Chachania, tulijipa moyo kwamba ipo siku ndugu yake atabadilika na kushika mema kama ilivyokuwa zama zake. Lakini wapi? Makusudi ni Makusudi tu. Alikuwa sawa na kovu zito lililokubali kurudia hali ya kuwa jeraha sugu. Hakuwa wa tiba seuze kafara.

Kwa sasa, aligeuka donda sugu lisilosikia dawa wala kafara. Kila kulipozidi kucha siku nyingine, ndivyo alivyonoga ghera ya vitendo vibovu zaidi. Aligeuka nzi asiyeogopa uchafu wowote ule. Tena tusisahau kuwa, kufa kwa nzi kidonani si ajabu!

Kimbarani! Hakujali chembe wala kubali chochote kijacho na kitokeacho kwake. Alifanya apendavyo kama fugo ijapo kwa siri kubwa. Alifanya yake kwa ufiche mkuu kwetu sisi na wazazi wake. Alitufungia pazia jeusi la kutotambua usaha wake. Huenda atendayo chemba yatatuacha bubu tukiyajua na kuyang’amua. Naye hakujua kuwa jipu huiva. Hadi siku moja.

Ilikuwa jioni ya Alhamisi, muda wa kipindi cha Magharibi kuvunja ungo. Mvua ya rasharasha ilichelea kujitojatoja angani. Pengine ilidhamiria kumwagika kwingine. (Wanafunzi wa Chumio) Sote tulianza kupiga milundi kuelekea makwetu. Tulitembea hatua za njiwa huku tukiwa katika makundi madogo madogo. Kila moja na soga lake. Miguu yetu ilibapababapa kwenye pambizo za barabara ya kuelekea darajani. Kule mtoni Marambo.Kivuko cha ngambo zote.

Hivi sasa, tulikuwa tumetoka shuleni na ilivyo ada yetu, tufikapo darajani, tunapokezana mikono ya kwaheri hadi tutakapokutana tena siku itakayofuata.

Siku hii sikuweza kuandamana na akina Makusudi.Nilikuwa nimesalia nyuma pamoja na kundi dogo la wanafunzi walioitwa kwa dharura kutoka darasa letu. Kikundi hiki kilikuwa na wanfanuzi karibu thenashara yaani kumi na wawili. Tuliokuwa hapa kundini, sote ni viranja wa shule. hivyo, nilikisia kuwa kuna ujumbe maalum unatusubiri pale nje ya Afisi ya Walimu.

Kulizuka tetesi mbovu juu yake rafiki yangu. Mbiu hii ya mgambo ilimfikia mwalimu wetu wa darasa Bwana Kadiri.Inafahamika kuwa baadhi ya wazazi wenye utu walimwarifu utovu huo. Utovu uliomwacha Makusudi kuwa totovu kila nilipomrudi kwa nia njema. Nilibakia kimya kwenye kundi lile la vinara wa shule.

Wengi wao wakiwa washirika kama si marafiki wake. Wote walikuwa kama mimi. Tulimfahamu sana. Ila mimi nilimjua zaidi yao ndiposa nikawa mwandani! Kila mmoja alipayuka yake bora asikike anajua jambo kumhusu. Punde, Bwana Kadiri alifika mlangoni na kututazama. Macho yake mekundu kama ngeu yalikuwa yameiva hasira kali. Huenda ndiyo yaliyomnyima haki ya kuongea nasi jioni ile. Alionekana kuwa na ustahimilivu wakiasi cha juu mno. Alijikaza kutulepukia sisi tusio na hatia kwa ghadhabu yake.

Nikiwa kiranja wa darasa lake, hakusita kuniita kando. Niliingia afisini mle nikiwa nyuma sanjari na mwalimu Kadiri.Nilikuwa ange kudadisika kumhusu Makusudi japo sikuwa na uhondo mwingi wala mtama wa kumwaga mara hii.

**MIMI (SADIKI)**: Shikamoo Mwalimu!

**BWANA KADIRI**: Marahaba mwanangu. Umeshindaje?

**MIMI (SADIKI)**: (*kwa uchangamfu na wingi wa kukaramka)* Nimeshinda vyema na salama. Hakika leo kipindi cha Kiswahili kilinoga kama halua.

**BWANA KADIRI**: Shabashi! Nashukuru sana kusikia hivyo.

Natumai ungali wajifunga kibwebwe masomoni. (*Akitabasamu na kuonyesha utani, hakuwa na chembechembe za mori kabisa*) Hivi bado wakumbuka ahadi yetu?

**MIMI(SADIKI)**: Naam, ningali natia bidii Mwalimu. (*Nikimtania pia*) Ahadi ni deni. Si dawa ya dawa ni kulipa!

**BWANA KADIRI**:(*acheka kidogo)* Vizuri. Kulipa deni ni tijara ya moyo. Madeni ni ugonjwa! Usikubali kuwa mdeni, Utaugua! *(Akitia mkazo*) Hata hivyo, nimekuita hapa. Nina jambo na nahitaji majibu uyaweke wazi tafadhali.

**MIMI (SADIKI):**(*nikitikisa kichwa kukubali*) Naam.

**BWANA KADIRI**: Makusudi akoje darasani siku hizi? Nimesikia anasumbua sana! Ni kweli amekuwa nzi huko?

**MIMI (SADIKI)**: (*kichwa nimekiinamisha*) La! Si ukweli. Lakini mara nyingi hayupo darasani. Hata mara nyingine haji kabisa shuleni. Ukiangalia sajili utagundua hivyo.

**BWANA KADIRI**: Enhe! Huwa nampa idhini kwenda kupata matibabu ya macho. Ruhusa yangu ni mara moja kwa juma! Si hivyo ndivyo tulikubaliana? Mimi na mamaye? Simwelewi mtoto huyu.

**MIMI (SADIKI)**: Ndio! (Nilijibu *bila kutarajia*)

**BWANA KADIRI**: Tumemsifu sana mgema sasa tembo kalitia maji! Hapana! Kuna jambo linaendelea na hujaniambia, Sadiki? (Sauti *ikipanda kidogo*)

**MIMI(SADIKI)**: Mwalimu, kwa kweli. Rafiki yangu amebadilika sana. Hata sisi wenzake hatujui anashiriki yapi. Tunafuunu kuwa amejiingiza kwenye lindi la uraibu. Uraibu wa dawa fulani…. Sina uhakika.

**BWANA KADIRI**: Ni hivyo! Habari hiyo imenifikia leo

kutoka wa wazazi wenu pamoja na chifu. Hata Inspetka wa polisi amepiga simu afisi ya Mwalimu mkuu. Si jambo la mzaha tena. Nitafanya uchunguzi wangu binafsi. Isiwe wewe pia upo kwenye mambo haya? (*alionya*)

**MIMI (SADIKI)**: Afanalek! Ni ahadi mwalimu hatupo kwenye mambo hayo! (*Nilijibu kwa taharuki)*

**BWANA KADIRI**: Ala! Wewe na nani tena?

**MIMI(SADIKI):** Mimi na Chachania.

**BWANA KADIRI**: Haya nenda nyumbani. Wasalimie wazazi ukifika. Alamsiki!

**MIMI (SADIKI):** Naam**!** Binuru**!** **(***Nilijibu nikiondoka kwa haraka*)

Kwa fajaa, kina Chachania walipokaribia daraja la Mirambo, shangingi la rangi ya kahawia, lenye namba za usajili - KCS 689V.Toyota Corolla hilo liliwafikia walipo. Mabarobaro wawili wenye misuli tinginya na mavunga ya nywele walishuka nje ya jigari hilo.

Kufumba na kufumbua, mmoja wao alikuwa ameshanyakuliwa marshimarshi hadi garini mle. Sauti iliowahi kumjia Chachania, ilirudi kumkirinzia kichwa wakati huo.

"Mzuie*! Mzuie. Fanya haraka wewe! Kimbia! Makusudi ......!*"

Chachania alikanganyikiwa na kuchanganyikiwa. Alitatanishwa na maana ya sauti ile nay ale yalikuwa yakitokea mbele ya macho yake. Hakuona hatua bora ya kushika mkononi muda ule. Aliduwaa tu pasi na kufanya jambo.

Akina Chachania walibaki wakitanabahi kwa hamaki na mshangao. Jigari lile lilishika lami vivyo hivyo kwa upesi wa umeme. Liliondoka kwa mbio za ajabu kiasi cha kuonyesha ujuzi na uhodari mkuu wa dereva wake.

Hali ilipowakaa na kuwarudia. Walijipekuapekua. Waligundua kuwa kinda mmoja kati yao hayupo. Naye si mwingine ila Makusudi!

Hapo ndipo walipojiona kama vifaranga vya kuku. Walirundika unyende mbaya hewani. Roho zikatikisika. Hata hivyo. Dua la kuku halimpati mwewe. Usaidizi haukuonekana kuja. Hawakuwa na jambo lingine la kutimiziwa kando na kulia kwa kite na shakawa.

Wasiwasi wa Mungu tuhurumie ukawateka nyara. Walitazama huku na kule. Hawakuona dalili wala ishara zozote za mwenzao. Akili zao ziliwashawishi wachane mbuga kutafuta nusura. Huo ndio uamuzi uliowasubiri viganjani mwao.

Mwisho walichana mbuga hadi makwao badala ya kurudi shuleni kwa walimu. Walikuwa wamechanganyikiwa na kuvurugika akili si haba. Kufika kwao nyumbani ndiko kulikuwa mwisho wa maelezo yake Chachania kuhusu siku hiyo."

Kumbe ndio maana asubuhi ile ya Ijumaa, Chachania aliwahi shule peke yake. Hadi mimi mwenyewe nilinyong'onyea kwa huzuni. Niliyokuwa nikiyakisia siku ile, hayakuwa mbali na udhahiri wa mambo yalivyo. Maswali niliowahi kujiuliza nilipomwona akija shuleni wakati ule wa asubuhi, yalikuwa na majibu yake tayari.

Niliingiwa na kizaazaa na mpapatiko mzito kama kuku mwoga. Wahaka huu ulikuwa sawa na jinsi Chachania mwenyewe alivyonibainishia mambo. Kumbe mambo hayakuwa mambo siku ya jana! Jamani rafiki yangu tuliyemsema sana jioni ya jana hiyo hayupo tena. Ameenda kudhirisha utundu wake! Kwa yamkini, sikuwa na maneno kinywani. Nilibakia bubu mwenye uwezo wa kusema angaa neno moja.

Kutoa neno kinywani kulinishinda kabisa. Ulimi wangu ulikuwa nanga iliotulia kwenye mgongo wa bahari. Nilishusha pumzi nzito nzito na kutumbua macho bure kama samaki. Kukaramka kwangu asubuhi hiyo, kukayayuka tamathali theluji kwenye nguu za mlima. Tulitazamana na Chachania hadi pale wakati wa mgongeo wa kengele kubwa ulipotugutusha kuingia madarasani. Kila mmoja alijivuta na

kujikazakaza kufikia darasa lake.

Vipindi vya kwanza viling’oa habta na kushika kasi. Milio ya kengele ilijivungumiza kwa ulegevu kana kwamba iliigiza vilio vyetu vya kumpoteza Makusudi shuleni pale. Haikuwa ibura kuwa kengele inaomboleza kupotea kwa mcheshi wetu. Wanafunzi walioipata habari hii, walionekana wakijiburutaburuta kuelekea madarasani mwao. habari iliwapitilizia ufahamu.

Kila kitu kilikosa maana. Kusoma kukawa taabu. Kuandika ni taabu. Kusikiliza kwa taabu. Mambo yote yalikuwa tabu na tabu tena. Kila mtu alikuwa tabu taabani kutaka kujituliza na kujiliwaza kwa kiasi cha haja ndio suluhu. Yaliomtokea mwenzetu yalikuwa kingwangwa. Mambo mazito ajabu. Sisi sote, yalituweka kwenye upweke na ukiwa tusioupenda. Hatukujua kama yu hai au ameshalazimishiwa idhini ya Izraili.Kweli, upweke ni uvundo.

***

Kutekwa nyara kwa Makusudi kulikuwa ni mtego wa kuwateka bakunja marafiki na familia yake. Yeyote atakayejaribu kumtafuta angetegwa kinywani kama samaki. Makusudi naye alikuwa chambo wa mengi yatakayojiri kwenye njama hii iliyopangwa kupangika. Hata walinda usalama walishikwa na hatihati kwa jambo hili. Vidole vya lawama vitawaelekea muda si mchache. Majukumu yao ya kutilia kila kitu machoo yaliambulia patupu. hawakuweza kumnasa Makusudi hata siku moja. hata kukwepa na kuhepa kwake shuleni kulikuwa kama kisa cha Abunuwasi.Muujiza mtupu.

Baada ya kuzuka kwa tukio hilo. Shuleni Chumio.Hali ya taharuki ilitanda na kuvangavanga kati ya walimu na wanafunzi. Hofu iligeuka mishipa yao ya damu! Sauti zao zilionyesha udhaifu

ulivyowakaa na huzuni ilivyowabeza. Shughuli za shule zilienda kwa kujiliwazaliwaza. habari ya kutoweka kwa Makusudi ikapepea angani, sikio moja hadi jingine. Si saa nyingi kabla hatujapata kujua kuwa hata redioni tangazo maalum ilitolewa. mukhtasari wa habari kwenye runinga uliangazia uhalifu huu. nchi nzima ya Mfumoni ikashika subira ya hatima yake Makusudi. Lau wangejua ni njama, sijui wangefanya nini.

Mitaa yote jirani ilipashiana habari hizi za ndege mbaya kujiri Mapona.Kila mmoja akichukua hatua na nafasi ya kuwachunga awapendao. Hususani wale wachanga na wadogo wao. michezo ya kutangatanga nje ukapigwa marufuku kwenye mitaa yote. Kila aliyepita njiani alitupiwa macho ya mwewe ili kubaini lengo lake la kupitia njia fulani. Watu walianza kujipipigia doria wenyewe. hasa kina mama na watoto wao. Hakika, tahadhari kabla ya hatari. Wasemavyo wenye kusema semi.

Huyu Makusudi, kama nilivyomshuku, sikufanya makusudi pia, shaka yangu ilianza kukata kiu yake. Nilikisia kuwa amejitia kwenye minyiri ya pweza mwenyewe. Kamwe hatajitoa hivi hivi bila kupoteza viungo. Nilikuwa nimemdokezea mwalimu wangu hali yake. Yatakayokea sasa, yalitutia homa kali.

Wiki mbili zilizopita, tulikuwa kiguu na njia – kituo cha Polisi kilichopo Kijutoni, hara ndogo iliopo Mapona.Kina Chachania na baadhi ya wanafunzi walikuwa naye siku ya mkasa wa kisa, walihitajika huko. Mahojiano ya kijasusi yaliwasubiri. Walitarajiwa kuelezea kinagaubaga ujio wa zahama iliowafika kule darajani – siku ya Alhamisi.

Mimi na Bwana Kadiri, tuliandamana nao sanjari chanjari hadi hatua za mwisho kituoni. Kulingana na ripoti ya inspekta wa polisi wa Kijutoni –Mzee Mzoa, alidai kuwa kupatikana kwa wahalifu pamoja na Makusudi, kulikuwa sawa na kutenganisha chai na sukari.

Inspekta Mzee Mzoa pia alitueleza kinaganaga kuwa anashuku kutekwa nyara huko kulikuwa kaga tu iliyoashiria uovu mwingi ulifichika mitaani mwetu. Akielezea haya, alikuwa akitazama picha fulani iliokuwa mezani pake. Alipokinaishwa nayo aliturudia tena kisha akatuzungumzia.

"*Juzi* tu, *baada ya kumwelezea Mwalimu wenu mkuu kuhusu huyu kijana. Nilitulia kwenye Kafeteria moja jijini Mashombo.Nilikuwa nikitazama runinga saa za jioni. Habari zilizoanguka machoni, zilinitemea mate! Zilinikejeli na kunizomea si haba. Kumbe mambo yana mambo yake. Taarifa hizo, zilinikumbusha kuwa nimesahau ukaidi wa mkia wa nguruwe. Haukomi kujikunja katu. Daima haunyooki. Kila kitu na kila mtu ni uhalifu tu! Mara kule wezi! Mara huku vijana waraibu! Mara wale mara hawa! Ni kweli, nimeshindwa kuwalinda vijana wetu kutotenda feli. Nitafanya nini*?"

Mzee Mzoa aliyasema haya akiwa amechoka tena kufikiria. Kichwa chake alikiinamisha chini kama mtawa. Hakuwa mtu wa kutamaushwa na lolote ila kisa cha Makusudi kilimpa tumbojoto. Mtoto amepotea kwenye eneo lake la kutoa huduma. ni majuma matatu tu tangu atie guu pale kituoni kwa minajili ya kuboresha usalama. hajakaa sawa na kituko chamkuta kifua wazi.

"*Sivyo! Bwana Inspekta.Unatulinda kama jihadi.*" Nilijaribu kumshawishi.

"*Utalizuia mkubwa wetu.* Matumizi *ya dawa za kulevya* ndio tatizo huku. *Zinatuweka tenge tahanani. Vijana wengi tumetepeta kama Pombo kwa kuzitumia kivoloya. Hatuwezi chochote wala lolote la kutufaa sisi na wengine tukibaki*

*mateka wa dawa hizi. Kuwa msamaria mwema kwetu. Unaweza kutusaidia. Nina imani kuwa unao uwezo.*" Chachania alichangia soga hili huku machozi yakimlengalenga machoni.

"*Nashukuru umegundua hivyo. Msikubali hata kidogo kutetereka kwa dawa hizo. Mjaribu kula kasama kupambana na tabia zozote za uraibu. Sawa?*" Mzee Mzoa aliyasema haya akitushika mabega na kututazama usoni.

Uso wake ulituonyesha uwezo wa kushinda uwoga tulikuwa nao kila mara. Ulituonesha ujasiri wa kukabiliana na hali yoyote ngumu maishani. Bila shaka, alitutia ari si tu ya kumtafuta mwenzetu bali pia ya kumbadilisha tabia, yeye na wengine miongoni mwetu. visa vya vijana kuingia shughuli kombo vilikuwa vikiongezeka kila siku. Kuna ripoti iliochapishwa gazetini yenye madai kuwa idadi kubwa ya mabinti wa shule nchini Mfumoni, wamechupia starehe. wanahepa masomo yao na kupuuza visomo wavipatavyo ili kujibanika vichochoroni kupata 'wafadhili-hai'. hela zao za kunuka ndizo ziliwavutia sana mpaka mabinti hao hao wapo radhi kujiuza. ujambazi sugu mara nyingi umehusishwa nao kando na kuwa mihadarati ni njia moja yao ya kuchuma pesa. isitoshe, gazeti ilinukuu kwamba, baadhi ya magonjwa ya zinaa na mengine ya kuchumbukia yalisambaa sana kwenye vitongoji duni kutokana na matumizi ya mihadarati. Taarifa kama hii ni ya kusikitisha na kuatua moyo.

Kidogo hivi, simu yake ikalia ghafla na kututarakanya mawazo yetu sote tuliokuwa afisini pale.

"Triiiiiii*! Triiiii! Triiiii! Triiiiii!*"

Mzee Mzoa Adili kama yalivyo majina yake kamili, aliitazama kwa kina simu yake kisha akaipokea taratibu kwenye sikio lake la

kushoto. Tulisaila tutwe bila kusongasonga wala kushikashika vitu pale afisini.

Taarifa alizozipata mara hii ni kwamba kuna watu wasiojulikana wametoa tara kwenye soko kuu la Mapona. Ilikuwa hali ya dharura kwani pia kulikuwa na kijana aliyetishia kujitia kitanzi katika roshani mojawapo huko huko Mapona. Inasemekana, uraibu wake wa dawa za kulevya ulimwekea makengeza!

Mzee Mzoa alituaga kwa haraka huku akitoka shoti sawa na mwanariadha. Miguu yake ya unju ilipita juu kwa juu kwenye sakafu yenye tarazo. Katika mwendo huo huo wa matiti alipiga mawasiliano fulani. Kisha akajitoma ndani ya gari lake ambalo lilitoka kituoni mbio pindi tu alipoingia ndani. Tulibaki macho pima.

Naye Bwana Kadiri alikuwa kule nje ya kituo akijuliana hali na askari wa doria waliokuwa naye pale. Tulipotokea mlangoni, wote waliturushia macho. Walitaka kujua kilichofumbuliwa na kumwacha mbio Inspekta wa Kijutoni.Kwa kupitia nyuso zako, tulijua wazi walichokitarajia kutoka kwetu ingawa majibu yao hayakuwa nasi pale bali Mzee Mzoa mwenyewe. Askari wale walitaka sana kujua kilichomtoa nyoka pangoni. Nao hawakusita kujitomasa kwenye stesheni yao ili kuchukua maagizo yaliowafikia hapo punde kwenye rukono zao. Wote waliondoka kwa spidi na kasi yao. Tulibaki tumesimama peke yetu kando ya mwalmu wetu Bwana Kadiri na askari wawili wa doria pale kituoni. Ilikuwa bayana kwamba kesi yetu ingengoja hadi keshoye. huenda ikawa hivyo.

“Haya, *njooni turudi shuleni sasa*.” Bwana Kadiri alitushawishi kuteremka vidato vya ngazi ili tufike pale walipokuwa wamesimama.

Tuliwafikia kwa utaratibu na unyenyekevu. Bwana Kadiri alitushika mikono na kuianzisha safari. Askari nao waliendelea na shughuli zao kama kawaida. Tulishukuru kwa hali hiyo.

Njiani, tulimsimulia mwalimu wetu yaliojiri na kutamba afisini mwake Inspekta.Naye alizidi kukariri ya kwamba dunia tambara bovu. Alitusihi mno tuweze kukubali kuwa watu wenye majina yasio na aibu mbele ya wengine. Tulimpa ahadi zetu kuwa tutajitahidi kufanya mema daima dawamu.

# SURA YA SABA

*Tamu ya mvua aijua mwonja*, ndivyo W aswahili walivyowahi kusema. Msena wangu alikuwa tayari ameuonja utamu huo kwa ulimi wake. Shughuli walizojiingiza kimasomaso, yeye na marafiki zake, ziliwahadaa sana.

Kina Makusudi walikuwa warina asali waliozoea kuchovya ovyo ulanguzi wa dawa za kulevya pasi na kutambua kwamba maisha yao kesho yatakuwaje. Heri punda na ngamia mara mia. Hawa, hawakuwa na masikio ya kubali chochote. Walizama ndani ya kiza kipana kwa vichwa na miguu.

Tena si ajabu walitenda mambo sawa na ubashiri wa gazetini, waligeuka wachuuzi hatari kwenye soko la maisha ya watu. Vijana wengi walioangukia jamvi lao hawakuwa na nusura kamwe. Walizidi kudidimia kwenye uteja wao wa uraibu.Walionunua bidhaa zao bila shaka,walibaki wateja wasio na bahati. Misukule yenye hamu na kiu ya kuharibu miili.

Tembe zikawa tembe tamu na dawa zikawapakia sumu miilini mwao! Laiti wangalijua giza walilonalo kwa sasa, wangalijisaidia kutafuta mwangaza mapema. Hivi karibuni, hali huwenda ikawa si hali tena.

Faida belele iliwagongea hodi kwa shangwe kila siku kina Makusudi.Hela walizozipata kwa haraka zilitokana na ununuzi wa sharubati, peremende na mifuko midogo midogo ya sandarusi iliyorundikizwa chembechembe za afyuni na madadi ya bangi.

Kwa bahati mbaya kama kukutana na bundi, Makusudi alijichimbia shimo jingine. Kulikuwa na kundi alilojiunga nalo. Genge hili lilishiba kasoro mchafukoge. Lilipanga na kupangua maasi mengi ya kuwaangamiza marika wenzao. Halikumjali mtu wala chake. kundi

hili lilishona kushonana makatili na mahayawani.

Naye alikubali kwa kila njia kuwa mwanachama kindakindaki. Kinara wa kundi hili alikuwa Kauzo – kijana mwenye hirimu *thalathashara* hivi. *Hakuna asiyemtambua, pengine serikali na mikono yake mirefu.*

Alikuwa chanzo kikuu cha kuenea kwa uuazi wa dawa za kulevya kati ya vijana wenzake. Alijiona mpevu wa akili kuliko walimu walioshinda wakimnyooshea vidole kila mara. Walimu walimkanya sana kuhusu hali yake ya kutumia dawa hizo. Kumbe ni sikio gutu. Hana apatalo hana linalomfaa kusikia.

Kauzo aliapa kutokanyaga tena lango lolote la shule baada ya kupokea zinduko kali kutoka kwa mwalimu wake mkuu. Hakupendezwa na hatua ya mwalimu wake huyo kule Kerodonda.

Kauzo, ambaye alikuwa yatima, alivunja ndoa yake na elimu miaka mitatu iliyopita. Alitoroka Kichakamkwajuni na kuguria jiji la Mashombo.Katika jiji hili, alipata fursa ya kukaa meza moja na walanguzi waliompa shughuli na kazi.

Alitafuta vijana waliozima mwanga wa maisha kama yeye ili kuunda kundi la kumsaidia kusambaza dawa zao kwa siri kote mitaani. Alifanikiwa kuunda kundi la vijana ishirini wa watano hivi. Wote walikuwa waasi wa shule zao. Mzungu husema, ***birds of the same feathers flock together.*** ama walijaribu kufikiria kuwa, '**Waswahili wa pemba hujuanakwa vilemba**?'

Kazi kuu ikiwa kuuza bidhaa zao. Waliwawindakama wanyamapori, wanafunzi wa shule za msingi sekondari na vyuoni. Walikuwa na wateja wengi. Miongoni mwao akiwa Makusudi.Makusudi aliwazoea na wao wakamzoea kama malaika na ngozi. Siku zilipozidi kuwapenda wote walitambua kuwa mazoea yana tabu.Hatimaye,walimsihi awaunge nao washirikiane ili wawe kinu na

mche.

Ingawa alikuwa kuku mgeni kwenye kundi hili, alipata nafasi yake ya kudhihirisha uhodari wake wa kuchezae watu shere. Hatua ya kwanza, alifaulu pindi alipokubali kutekwa nyara. Njama hii ilikuwa ya kumfanya Makusudi atekeleze mipango yao kwa siri kubwa hata zaidi. kundi lake lilihitaji hela nyingi kwa minajili ya kuendesha mambo vizuri. njama aliyokuja nayo Makusudi ilikusudia kufadhlisha shughuli zote. Alifu mpaka yeh.

Sisi wengine, hasa mimi na Chachania, tulibakia kwenye msala mmoja wa kujizatiti na kujitahidi tuwezavyo kwenye masomo yetu skulini. Tulivuta subira kwa magumu ambayo yangezuka shuleni na nyumbani. Muhula wa tatu ulikuwa karibu kumalizika. Likizo ya Desemba haikuwa mbali. Makusudi alishaanza likizo yake kitambo. Likizo ya kutenda masihara. Masihara alioyatenda na wenzake yalifuma hara. ingawa hara zenyewe bado hazijaanza kuwawasha ngozini. kumbuka njama na siri zao za ulanguzi zilikuwa siri kwao wenyewe.

***

Matendo mabaya huwa na ijara pia. Usiku mmoja, Inspekta Mzee Mzoa na kikosi chake walifaulu kuweka mtego uliopata kufanikiwa kumkwangura Kauzo kwenye vibanda vya Kichakamkwaju.Vijana wengi wenye tabia mbi walibambwa pia na kigora cha polisi wa Mzee Mzoa.

Japokuwa Kauzo alinusurika kifo na kukamatwa, wanachama wake hawakuwa na nguvu zozote. Wengi kwa idadi kubwa, waliojifanya wanajeshi walikumbatia marisau, roho zao wakazianika kwenye kamba za nguo zake mpenda roho. Mwisho wao haukuwa mwema hakika. Walisafiri jongomeo kwa hiari ya utundu wao. Uhalifu

haulipi inagawa hawatilii maani kauli kama hizi.

Kauzo na Makusudi hawakuerevuka kwa yaliowasibu wenzao ni funzo tosha bali walikoleza mawi. Wakawa chanda na pete. Walioyapanga kutoka hapa, walituacha raia wengi wa Mfumoni kufikiria mbona simba hafi kwa dhoruba moja.

Siku tatu zilizofuata, Kauzo alimpigia pambaja Makusudi ambaye alikuwa gwiji wa kazi yao. Alimpogeza kwa jitihada zake katika kundi lao. Makusudi alifaulu sana kuzieneza bidhaa zao ghushi katika shule nyingi za aina ainati. Alitumia ucheshi wake na talanta yake ya ucheshi kuwanasa wateja wake waliokuwa kama samaki wasiokinai chambo ziwani.

Kauzo alipanga kupeleka Makusudi akutane na jemedari wake. Mkubwa wa shughuli zao. Mkuu huyu alikuwa kule Mashombo ingawaje kina Makusudi na wengine hakufaulu kumtilia jicho hata siku moja. Kauzo alipanga kumpeleka mwenzake kwani kazi kubwa ilikuwa inaandaliwa. Bila shaka Makusudi atahitajika sana kama viungo vya pilau. juhudi zake kundi zilingaa kama nyota yake ya zamani, nyota aliyokuwa nayo masomoni.

## SURA YA NANE

*Hayawi hayawi, yasiokuwa yakawa*. Siku ya Kauzo na Makusudi kuunga miguu na safari ilifika. Siku hiyo, Makusudi alipata uwezo wa kuizima kiu yake ya kumjua kiongozi mkuu wa makundi yale yao. Ilikuwa siku yake kumjua jemedari wa genge lao kubwa lililoitwa ***'VIJA–KOMBO'***. Kana kwamba ni ada na kawaida yao, walipenya kwenye vijia vyao vya siri hadi mwisho wa safari yao kule Mashombo.

Siku hiyo, waliandamana sako kwa bako kama siafu jeshi. Walizidi kuwa wengi kadiri safari yao ilivyozidi kukata kamba. Vikosi vingine vilijiunga njiani. Wote walijuana kwa vilemba hata ilikuwa tabu kumtambua mgeni kati yao.

Genge la vijana sita u sitini lilitembea kikakakaka kuelekea eneo la mgambo. Kule Mashombo.Wote walikuwa wameitikia wito wa ile kazi kubwa ilioandaliwa kutekelezwa nao. Walipofika eneo la siri, kila mmoja alizama ndani ya jumba fulani lililokuwa kwenye mitaa ya kuunda magari. Hakika mipango ilianza kuiva mekoni kutoka hapo.

Makusudi na wenzake hawakuwa na mwao hata kidogo kuhusu mipango uliopangwa. Waliamua kumsaili kinara wao Kauzo ambaye aliwashibisha masikio yao. Aliwaeleza jinsi kiongozi wao alivyopanga kuipora Benki kuu ya Tabala iliopo kule Mashombo.

Taarifa hii kidogo ilimitia kiwewe cha ndani kwa ndani. Kupora Benki ni kama kujichimbia kaburi ungali hai. Hakujua arudi nyuma afuate maisha ya zamani au akae ajione yajayo. Alibaini wazi kwamba mambo huwa ni kangaja, huwenda yakaja.

Makusudi alikata kauli ya kusubiri yajayo. Hakuamini hata kidogo kwamba nyuma yake kuna uzuri uliomliliaaupokee. Uzuri wa kubadilika ulimlilia ila aliugeuzia mgongo na kuyafumbia hadi macho. Upande mwingine njama ilimfungulia mlango kuingia.

Njama yao ya kwenda kuipora benki kuu ya Tabala ilisalia tu

kutimizwa. Siku za kuhesabika kama leo na jana, tayari zilikuwa zimedondoka nje ya kalenda yao. Huwenda kesho –Ijumaa mwezi wa saba ikawa siku yenye mkesha wa hamu na ghera kwao iwapo lengo lao litatimia.

Makusudi na wenzake walijizamisha kwenye katara lililokuwa limeegeshwa na kuhifadhiwa kwa siri katika gereji la mwenzao aliyeitwa Bwana Mbisho Mango–aliyekuwa Mekanika bingwa jijini Mashombo.

Cheche za uhalifu zilivuta hamu ya kufanyika. Pale garini, Makusudi na vijana wenzake walimpata mwanamke mwenye umri wa makamo. Alijitambulisha kwao kama Bi. Santana Kigezo.

Bi. Kigezo ni mfanyabiashara mashuhuri jijini Mashombo. Alikuwa na biashara yake kwenye jengo mojawapo yalio pua na mdomo kwa jengo la Benki kuu.Bi. Kigezo alikuwa amepanga mengi ya kutendwa kwa yakini.

Ulikuwa wakati wa giza kuu, genge hili lilianza safari yao kuingia katika jiji la Mashombo.Jiji hili ni mkabala wa mtaa wetu. Walipanga na kuweka tayari vifaa vyao vya uvamizi hasa vya kubomoa vyumba vya hazina ya benki.

Vitu hivi vilizikwa kimyakimya kwenye mashanta yao ya kijivu. Majitu tambo mawili yalikuwa kando yakipanga vifurushi vya risasi kwenye bastola zao za G3 na bunduki nyingine za rasharasha. Silaha hizi walizikomboa kutoka kwa majangili fulani kule mpakani Tsavo Mashariki.Mikakati hii ilipangwa na Bwana Mbisho – Yule Mekanika...

Walipakia vifaa vyao kwenye buti la mashangingi mawili yalilokuwa maegeshoni upande wa pili wa jengo lao la maficho. Gari la kwanza lilikuwa aina ya *Nissan V8* lenye weusi wa kaniki. La pili lilikuwa *BMW V6*. Mpango wa kulitumia gari hilo la pili haukubainika

waziwazi. Kwani hata kina Makusudi hawakujua kuwa kuna kundi jingine pamoja nao kwenye harakati zao za wizi.

Waligundua hilo walipomaliza kujipanga na kurudia kikao chao jengoni ambamo walikuwa wamejificha humo kwa majuma yasiopungua kumi na mawili.Bi. Kigezo na Bwana Mbisho waliwaongoza wenzao kuelewa uzito wa kazi iliowasubiri usiku wa kesho.

Kwenye jumba lile la matongo, waliunda mduara huku wote wakitazama ramani ya Benki kuu ya Tabala.Wote waliaamini na kujiamini kwa imani zao. Kwa liwe liwalo, walichokipanga na kukiwekea ramani sharti kitimie.

Kila mmoja wao alipata jukumu la kushughulikia kwenye kikosi hicho. Wote walihitajika kutia juhudi zao ili nia yao ipate kufana. Makusudi na dereva wao Bi. Buye –walikuwa wabaki garini wakipiga darubini hali itakavyo kuwa pale nje ya benki. Kumi na sita waliosalia walifaa bila hali ya kiwe kuvamia benki bimithili ya mboza waonao mizoga.

Vijana waliobakia waliongozwa na Kauzo kwenda kuzurura maeneo ya Benki mchana wa uvamizi. Walifaa kudadidisi yote yanayotendeka bila kupitwa na lolote. Kauzo aliwaongoza mara moja baada ya maagizo ya Bi. Kigezo.Walipoondoka, kulibalikia na makundi mawili tu kwenye kikao chao.

Baada ya muda mchache wa ugono kuchuchumaa, wenzao kwenye kundi lile la pili, walielekea sanjari chanjari hadi kwenye gari la pili lililokuwa magharibi yao.Bi. Buye alishika usukani bila kusita wala kubabaika. Hata yeye alikuwa na azma ya kugotoa shughuli hii liwe liwalo.

Taa za gari zilipong‘aa na kumulika barabara,safari ilianzisha mwendo. Jigari lao lilipasua upepo kwenye giza totoro kwani halikuwa

butu kwa kuchubua lami. Lilikuwa dhabiti na mahiri si kwa kasi tu bali pia kwa kuepuka matuta na mabonde njiani. Kwa yakini litawatunuku sana siku hii wakilitumia vyema.

Isitoshe, gari hilo kilikarabatiwa na kukarabatika si mchezo. Umbo na muundo wake ungelitupiwa jicho na yeyote angelilidhania ni deraya bila shaka! *KAG 307E* – namba ya usajili wa gari hili ilibakia ikining‘inia hangahanga kwenye bodi ya nyuma kutokana na mbio zilizoibuka kati ya gari na safari iliojiri.Nyuma ya jigari la kwanza,lilifuata na gari jingine lililowabeba wanakundi wengine.

Kwa hakika, siku hii walijua kimoyomoyo, haikuwa na ndegembaya. Mipango yao ingetimia kwa wepesi wa dira. Hawakuona kizuizi chochote kati ya yale waliyoyapanga na kupangua majuma hayo yote yaliopita hapo mbeleni. Hadi sasa, kila kilichopangwa kilikuwa kimeshavumbikwa sawa na matunda mabichi na huwenda yameiva. Ama kweli, *dhamira ni dira*.

Mwendo wa saa nane u nusu hivi, walikuwa karibu na ghorofa iliokaribia eneo la tamaa na ashiki yao – *Benki ya Tabala*.Hapa ndipo kiongozi wao alikuwa amekodi afisi kwa minajili ya biashara yake ya kuuza mitumba na nguo nyingine cheche-sheshe za kutoka nchi za ng‘ambo kama vile Dubai,Amerika,Ufaransa,Uingereza na hata Uchina .

Kama jemedari wa kikosi chao. Siti Santana Kigezo–kama alivyopenda kujiita, alishuka kutoka kwenye gari la pili na aliwaashiria madereva pahali pa kuyasimamisha magari yao.

Magari yalipoegeshwa maegeshoni mkabala wa ghorofa. Walishuka kwa arubii na kujibebesha mizigo ya mashanta yao kisha wote wakamfuata nyuma Bi. Kigezo kuelekea ndani ya ghorofa ile. Walielekea kwenye chumba kimoja kati ya vingine vingi vilivyokuwa pale chini katika ghorofa ya kwanza ya jengo lile lenye upana sawa na

manowari kumi na saba kwenye foleni moja kwenda angani!

Chumba hiki ndicho kilikuwa duka la nguo za ng‘ambo. Waliingia himahima na kujifungia ndani baada ya kuchunguza iwapo kulikuwa na mtu aliyejaribu kufuata harufu yao hadi walipofikia. Makusudi aliwasha taa huku wenzake wakizirejesha chini pazia za madirisha kwenye chumba hicho. Mipango ya kuvamia Benki ikaiva kutoka hapo.

# SURA YA TISA

Kumbe *mchele haukosi ndume*. Uzuri wa Makusudi uliumbuka. Akajipata na ubaya mwingi. Si akilini tu bali pia moyoni. Ingawaje aliona uzito kuyafanya matendo ya njama zao, hakuwa na hali nyingine kando na kuwaunga mkono. Alijua dhahiri shahiri ya kwamba kuwasaliti wenzake kungemletea mengine. Waama kwa waima, *mganga mfichua mirimo ya wenziye huuliwa*!

Bi Kigezo aliwapanga vijana hawa kulingana na walivyoagizana kuvamia. Makusudi alifaa kubaki pamoja na madereva wakipiga darubini hali ya barabarani. Wakifaa zaidi kuwapasha wenzao hali yoyote ya hatari ikitokea.

Saa sita usiku ilitimia. Saa kuu ya barabara ilidhirisha hivyo kwa mishale yake ilio imara. Muda wa waja wenye mikono mirefu ilikuwa tayari kikaoni. Nao walio na yao ya mawi walijimwaga ugani bila woga. Wenzake Tashi walikuwa mbioni kumaliza shughuli yao.

Walifaulu kuingia ndani ya Banki.Bi Kigezo hakuwa mchache wa kung'oa vizuizi vya teknolojia vivyokuwa kwenye milango ya siri. Walifika karibu na lango la hazina. Hapa, walihitaji muda ili kuubomoa kwa vifaa walivyokuwa wamevibeba toka awali.

Ghafla bin kichea, kikosi cha polisi wakupiga doria kilitokea kule barabarani kama kifo na msena wake Izraili wafanyavyo. Makusudi na wenzake walishindwa kuamini wala kusadiki kuwa wanayoona ni meupe kama mchana wa jua.

Kila mmoja wao alitetemeka kwa hofu nyingi. Damu iliwakimbia kwa taharuki. Macho yao yalibaki yanagezageza huku na kule bila kuchukua hatua yoyote. Kabla wajifahamu, makaradinga ya polisi yalikuwa yamewakaribia sana sawa na hatua mbili tatu za miguu.

Kwa kuwa ukunguru ulikuwa tayari nao, walijiondoa kwenye magari yale wakiwa miguu niponye. Walizitafuna mbio za nyikani

kama panya walibumburushwa shimoni kwa miale ya moto.

Kila mtu njia yake. Wasilojua ni kwamba walikuwa wamezingirwa na askari walio siafu. Wote waliotoroka walijipata wamejisalimisha shingo upande kwa polisi walikuwa hima kuwaweka chini kivyovyote vile. Mchezo wa askari kumfukuza mhalifu ulipigiwa kipenga kitambo. Kina Makusudi hawakuwa na mwao hata.

Makusudi alifaulu kujibanza kwenye pipa la takataka. Alitwetatweta mithili ya ndege aliyenusurika kutengwa na uhai wake. Hakuamini kabisa. Eti anashikwa akiwa mwanafunzi aliye na yunifomu! Aibu ilioje kwake na kwa Familia.Marafiki. Walimu.Majirani. Watu wengine watamchukulia vipi mara hii? Na hakika, alijiuliza mwenyewe.

Bado usugu na kiburi ulikuwa ungali hai kwake. Aliamua kuwapigia simu kina Bi. Kigezo.Alibofya nambari na kutega sikio simu ikiita. Pindi tu ilipoingia kwenye mawasiliano, king'ora cha hatari kilijitokeza kule benkini. Askari wa benki walijitokeza kwa wingi kama wingu la panzi. Wakali kama nyigu na nduguze.

King'ora hicho hicho, kilimtoa hoihoi Makusudi alipojificha akidhani amegundulika. Lahaula! Alienda matiti miguu kushika misamba. Mwendo wake wa kujinusuru uligeuka gundi. Haukumfaa kamwe. Huwezi kimbia kama umevurugika akili. Alibambwa juu kwa juu na kikosi kilichokuwa papo hapo jaani! Alishikwa pap. Utadhani alikuwa shume lilosubiriwa litokee kwenye mapipa ya taka.

"Triiiiiii*! Triiiii! Triiiii! Triiiiii*! Simu yake Bi. Kigezo alikubali kulia kwa inadi na mikogo kana kwamba imetumwa kuwafichua walipo. Makusudi yupo tuli. Askari nayo vivyo hivyo, wanamtazama paka wao. Makusudi alishindwa kuipokea simu kwa kuwa alishasalimu amri. Bi Kigezo alipoona simu yake imelia kisha ikakatika ghafla, alitambua na kunusa hali mbaya ya shabuka na taklifu imewakaribia.

Aliwaarifu wenzake waweze kuchana mbuga.

‘*Siku za mwizi ni arobaini*’. Kwa kuhesabu, zao zilikuwa zimekamilisha hesabu hiyo. Walikimbia ovyo ovyo kwenye vyumba vya benki. Wengine walienda kule. Wengine walipita hivi. Waligeuka panya walioingia kwenye himaya ya paka koko. Kujuta kuliwasubiri sana.

Walipofaulu kutoka nje ya benki, waliirukia teksi moja ilikuwa imewasili kwa bahati nzuri. Teksi hii ilihitajika kumshusha mteja wake aliyekuwa anaelekea walikotoka kina Bi. Kigezi.Walivyojitupa ndani ya kijigari kile kulimithilika viazi vilivyofinyiliwa na kubonyezwa kuunda vipande vya chipsi mbichi. Walikuwa na haraka ya kutorok. Walitoroka kushikwa na kubambwa.

Abiria wale wasiotarajiwa walijibana bila kujali ada ya mishipi ya kujifunga seuze mteja wa teksi ile. Walikatalia humo. Wakamlazimisha dereva kuliondoa haraka. Kwa kuhofiya uhai wake wa kuiona kesho, dereva aliliondoa gari lake liliogeuka swara hatua chache za mwendo wake.

Dereva yule alichanganyishwa na umakini wake kutokana na vitisho vilivyowatoka kinywani wateja wake watundu. Alipoanza mwendo wa kasi, kisirani na chira zilimkinga kutofika mbali. Aligonga gari lililokuwa likija mbele yao sawa na risasi iliyopenya mtutu wa bunduki.

*‘BUUUM! TWAAA! KATAAA!’* Ajali ilicheka. Iliwacheka waliojigeuza kitoweo cha Izraili kwa hiari. Ajali hii haikuwa na huruma. Ilibingirisha magari yote bingiribingiri na kuyabondabonda kwa hasira. Haikutamanika wala kusemezeka. Ilitisha sana.

Magurudumu yenye pancha na mabamba ya gari ndio baadhi ya vitu vilivyosailia kama ushahidi wake Kifo kuwa katembea pale. Magari ya polisi yalipofika, yaliona yamechelewa kuokoa uhai na

kunasa uhalifu.

Waswahili hawakukosa mawazo walipodai kuwa ajali haina kinga. Watoro walikosa kinga kwa hakika. Manusura wala mansura hawakuwa na nafasi ya kutajika usiku huo. Makusudi pekee ndiye aliyesaila kulikabili jina na kuwa ‘mhalifu’. Mhalifu mwenye uzuri wa mkakasi ndani mabuu.

Katika eneo hilo, shughuli zikawa nyingi. kunusuru na kuwawahi walio na uhai. kuchunguza hapa na pale. Polisi walikuwa mbioni. Makusudi hakuta kushikwa vile. kwa kuwa alikuwa na mavazi ya shule na walinzi waliombamba walikaa walezi komba, aliamua kujinasua. Aliwageuzia hadithi na kisa.

" *Walinzi, mbona mnanishika jamani, Mimi ni mzalendo.*" Makusudi alijitetea.

"*Mzalendo wa wapi? wewe ni gaidi.*"Askari mmoja alimjibu.

"*Wewe ni mwanafunzi wa shule. Unafanya nini nje usiku huu mkubwa?*" Mwingine aliuliza.

" *Mimi nilikuwa nimetumwa dawa na nyanya mkuu. Anaugua sana. Sina budi kumsaidia*."Alijibu kijana mtu.

*"Mbona ulijificha kwenye Mapipa ya taka*?" Mwingine akauliza.

"*Nilikuwa na hofu kubwa sana. Nilikuwa nimewatia machoni wezi wale. Wangeniona si wangenimaliza pia*."Makusudi alijibu.

" *Umesema umekwenda kuleta dawa. ziko* wapi?" Makusudi akaulizwa.

"*Ndizo hizi hapa.*"

Makusudi alitoa tembe kadhaa za 'paracetamol' na zingine za

'asprin'.

Walinzi wale na ulevi wao wakamwashilia kijana mtu. Tena, walimpa amri ya kukimbilia nyumbani haraka awezavyo kabla hawajabali nia. Makusudi akala jasho la miguu yake. Akapotelea vichochoroni. Akapotea ndanikwa ndani, akawa kivuli cha kiza kama giza lenyewe.

# SURA YA KUMI

Miezi michache ya kukumbukwa kwa idadi ya siku zake, Makusudi alikosa kuwa mtu wala jitu kama zamani. Thamani yake ilipotea ghafla. Alianza kuchakaa, hulka na silika njema tulizozienzi akazivua kamagou chafu. Kulingana na utamu ule wa ulanguzi, alipokea mabunda ya fulusi nyingi, ajabu yake kusahau asali ya masomo shuleni! Pesa hizi zilikuwa zake kwa njia ya siri.

Hakuna aliyefahamu alipochimbia **maishilio** ila yeye mwenyewe na wenye giza wenzake. Kutoka hapo, aliamua kufuata mkondo wa uraibu na upofu mwingine katika jamii bila nadhari wala tahadhari. Makusudi amekuwa maji machafu kwenye karo.

Kundi alilojiunga nalo hapo awali, kabla ya kusambaratika, lilimpeperusha kama bendera. Alibobea kwenye magendo mbalimbali. Katika hali hiyo, alijipata amepepeapepea hadi kusikofaa kupeperukia kwa mikono wala miguu.

Anakumbuka vizuri, kwenye miezi ile michache ya awali, *Kauzo* alimtambulisha Makusudi kwenye genge jingine tena. Alitambulishwa kwao kabla ya kulijua genge la Bi. Kigezo.

Genge hili lilikuwa moto wa kuotea mbali katika kuvalia njuga anasa za dunia. Lilikuwa hatari mno. Hatari zaidi kuliko kikundi cha kwanza alichojiunga. Harubu ya genge hili haikumithilika. Si kwa kutajwa na kulaaniwa bali pia kwa kuonekana lilitambaa kama nyoka. Lilikuwa na uwezo wa kutupa sumu kali ya kuzima salama na amani popote lipitapo.

**‘*VIJA–KOMBO’***. Genge lenyewe lilijiita hivyo baada ya kufupisha maneno yaliokuwa kipaumbele kwao; ‘**Vija**na waliojaa mambo **kombo**’.

Kujiunga kwa Makusudi kwenye shimo la wendaziwamu wale ndiko kuliko mzika mzima kwenye kaburi la mawi. Ubeberu wa ukaidi

ukamwingia akawa kengeza wa mema asiyekuwa na kiwi kwa upwagu na upwaguzi.

Siku ziliposonga, Makusudi aliongeza weledi wa kutambua mizungu ya jiji kuu huku kwetu. Jiji la Mashombo. Huko, alipenya kila kichochoro na ushoroba akieneza injili yao ya uporaji.

Ipo siku walienda kumpora Bwana Bandura, paroko wa parokia kuu Mashombo.Makusudi anakumbuka siku hiyo kama asubuhi yoyote ya siku. Walimpata mja wa Mungu akiondoka kwake kuelekea parishi mojawapo ya waumini wake.

Alipanga safari hii kuwazima kiu wana kondoo kwa neno la Mungu.Alikuwa anaelekea basilika ya Mapona. Siku hiyo, Bwana Bandura, alikuwa angali anajiandaa taratibu nyumbani kwake kabla ya kuonoa miguu kuanza safari.

Akiwa mlangoni pa jumba lake, aking'ang'ana kubana kufuli lililompa kiwewe kidogo siku hiyo. Kina Makusudi alimpata akipambana kucha kuchanika pale mlango pake. Walipokutana soli na Padri Bandura aliwasalimia kwa furaha zisizo na bei wala gharama.

"Amani *iwe nanyi Wanangu!*"

"Iwe *nawe pia Askofu*!" Wenzake Makusudi walijibu kwa kejeli. Makusudi hakujua salamu hizo ingawa alileleka na kulelewa katika aila inayozingatia dini kama parange na ngao ya maisha yao.

Padre Bandura alipowapa mgongo wake. Walimtolea silaha zao butu ziliwahi kuwaparura waliowapinga. Wakampora mcha Mungu na jumba lake wakalikung'uta kubakia tupu kama bwalo la shule. Walipomaliza mirimo yao waliondoka wakijishanua na kujipiga vifua kwa vicheko kama bakaya mwitu.

Akiwa angali sakafuni amepiga magoti, Padri Bandura na kimo

chake cha nyundo, aliomba dua akiinua mikono yake juu angani.

*"Ewe Mwenyezi Mkawini Mbingu na Ardhi, nakuomba kwa unyenyekevu uondoe dhiki ya vijana hawa. Ni bayana hawajui watendayo.*" Padri Bandura aliomba huku amekukuta miguu yake chini.

Mungu Mwenyezi alikisikia kilio chake ila alimtakabalia siku nyingine. Kumpora mja huyu kulimchimba sana mawazo Makusudi.Aliogopa kushikwa pabaya na 'albadiri kali' iliyotamkwa na mja wa Mungu.Alijua fika kuwa makuu yanawasubiri mbele yao kama kioo. Ni siku na muda tu hakujua.

Aliwaza sana kama mlokole aliyetema chini ulokole wake kuwa mwasi. Aliwaza kama mhafidhina aliyeiritadi dini salama kwa kukosa ijaza. Wazo lake la mwisho kabla ya kushikwa na yaliyomshika leo, lilimpatia mzozo akilini mwake.

"*Ninafanya mazuri kweli? Nipo sawa! Nimevuka mipaka? Nielendelee ama niyawache haya*? *Sirudi nyuma hata. Potelea mbali*!"

Moyo wake ulipinga mawazo hayo kabisa kwa kumshauri. "Usiwache *mbachao kwa mswala upitao! Rudi nyuma kaka*." Hata hivyo, muda wa kukaa chini na kuusilikiza moyo wake haukuwapo wala haukupatikana.

Katika jiji la Mashombo, kila kitu kilikuwa kimejitwaa na kujituliza kwa sura ya kupendeza wageni. Jiji hili liliwafanya lukuki ya wageni kuwa na kamba miguuni–sawa na kuku. Kila ajaye Mashombo, hukutana uso kwa uso na majumba ya fahari yenye mapaa yanayotabasamia ufanisi kuliko Mapona.Kuna maduka ya kila aina. Si maduka ya jumla. Si maduka ya rejareja. Si maduka vibanda!

Huko, Makusudi na majizi wenzake waliendelea kujipachika laana migongoni mwao. Waliiba na kupora kila muda na nafasi yake, tabia hii iliwageuza nzige wa hasara katika mahashuo ya watu. Japo walitenda haya, Makusudi alitamani mwisho mwema hata kama

alikuwa anachezea zuri, hakutaka baya limfike.

Aliogelea hadi kufa maji kwenye utukutu huu hadi wa leo. Usiku wa leo ulikuja kwake kama mawimbi yenye tamaa ya kumeza mabaharia baharini. Usiku huu wa leo uliamua kumvua nguo na kumwanika peupe hadharani.

***

Siku zile za Jumanne, Alhamisi, Ijumaa pamoja na wikendi ni baadhi ya mida alioitumia sana Makusudi kutokuwa mwanafunzi. Upo wakati, alijipata ameondoka shuleni kupitia nyufa za nyua za shule. Akiwa na kisingizio kuwa yeye ni mwana wa nyuki maskini, lazima ajikomboe nafsi. Ati anajitafutia cha mdomo na mwili siku kama hizo.

Bila shaka, alikuwa mtu asiyejikubali jinsi alivyo. Alitaka kuwa zaidi ya watoto wengine walionekana kuramba kashata za maisha matamu kila kuchapo. Alitaka mno kuishi kama mimi –Sadiki mwana wa panopano. Aling'ang'ania fupa si lake tena kwa wakati mbaya. Hata hivyo, Mungu ana yake.

Kuna Ahamisi moja, alishiriki biashara zake za kuuza vigae vya vyuma na mabati huko Kichakamkwaju.Madhari ya Kichakamkwanju yalikubali na kupokea kwa mikono miwili kuwapo kwa viwanda vya '*Jua Kali'*. Ugomvi kati ya nyundo na mabamba ulienea katika anga za huko mchana kutwa.

Kando na kujituma huku, Makusudi alipanua mikono na akili zake kuliko tamaa iliomuua fisi. Akiongozwa na jamaa fulani aliyeitwa *Naafi*, alisambaza na kuuza dawa zao za kulevya kwenye uchochoro

wowote uliomkubalia kupita kwa siri na hombo. Madadi aliyouza sehemu hizo, zilikuwa zinaitwa 'gode’, hivyo ungewasikia wakisema 'wanafuta gode'. Huku nchini ni kawaida kusikia lugha zikiibukaibuka kama uyoga wa porini. Kila mtaa una lugha yake. Mwerevu wa lugha hana chake. Huwezi kutambua ujumbe wao. Pengine kuchanganyikiwa tu. Aksari na mzazi mtu mzima ajue vipi maana ya gode. Kwani gode ni nini?

Mara nyingi, wateja wake walikuwa na maficho yao yaliokuwa chini ya daraja la Mirambo na mabonde ya Masazoni kwenye misitu na vichaka iliotamalaki ujanikuwiti.

Ewaa! Mchezea zuri na baya hufika. Mchezo aliouzamia kuusakata ndugu Makusudi, ulianza kubadili mkondo wa lele. Aliikosa ari na ashiki ya kuwa darasani seuze kutia guu shuleni. Maswahiba wema, kama mimi na wengine, aliwatema kama si kuwatenga na uso wake. Hakutaka tena kuwa karibu na sisi.

*Mzaha mzaha hutumbua jibu*. Mambo yalizidi kuwa mvange. Makusudi alitumbukia kwenye matumizi ya dawa zile. Alitumia dawa hizo eti kujituliza kama wateja wake wafanyavyo. Zilimfanya mlevi na mwehu wa ajabu.

Maji yalipozidi unga. Alitumia kila aina ya tembe ambazo zilimwacha hoi bin tiki. Si kokeni si bangi si marijuana si gani nyingine ile! Alichovyachovya bila kutambua anajimaliza mwenyewe, dawa zile zilianza kumbandua bandu bandu kama gogo la mbuyu litemwapo na shoka kali.

Kila wakati alipokuwa shuleni, macho yalimwashawasha kama mtu aliyetiliwa wage mavazini, mwili ulimtetema na malaika za ngozi yake zilisimama wima akawa sawa na kidimu kizimbani. Yalipojiri haya, aliomba ruhusa ya kwenda matibabu katika zahanati ilikuwa pua na mdomo na shuleni.

Hakuna mwalimu aliyemnyima nafasi ya kutibiwa. Hasa kwake mwanafunzi wao aliyekuwa mjali wa taa ya elimu kwenye tamniri na mijarabu! Walakini kwa kasoro zake tu, anapotia miguu yake nje ya Chumio, hujiingiza chemba kujitibu kwa dawa asi. Kwa hali hii, aliona shule kama jela ndogo ya watoto!

"*Mbona nijiingize mzimamzima kwenye gereza la Chumio? kwa hiari! Eti masomo! masomo kitu gani! Mimi mwenyewe mwerevu! ProfesaAkilimaji! Mimi nikae siku nzimana kubongoa macho kwa kila ukurasa na kitabu. Ya nini? Maswali yakija nayabomoa kama kawaida. Siwezi na Sitaki tena ujinga kama huu!*" Ndivyo alivyojizungumzia kila alipojidunga uganga wake wa sirenji moja ya heroini. Aliendelea kuwa paka koko mwenye siri nyingi.

Baba yake alimshuku mwanaye kuwa na chembe za mambo mabaya ila muda na nafasi zilimkataza kumchunguza mtoto wake. Kwa umbali kama mzazi, aliona dalili za kijana wake kubadilika si kwa hulka si mwenendo si matendo.

Kabla ya kuwa mtu wa leo, Bwana Koja alikuwa na janga na jangwa lake. Alikuwa katika vumbi la kupambana na udhaifu wake uliowashika madume mengi ya Masazoni–ulevi chakari na ukata wa urithi.

Aila yake Bwana Koja iliweza kusadiki kuwa '*kichwa'* chao ni mlevi kupindukia. Bwana Koja alikuwa mnywaji hatari wa '*maji ya wazee*' hata asubuhi ni wa kubebwa ama kuzolewa msombe kama mkeka wa barazani.

Bahati yake Bwana Koja ni kwamba mkewe ni mcha Mungu.Bi. Tumaini alikesha usiku kucha. Alishinda mchana kutwa akiomba maombi ya kumnusuru aliyempa moyo wake. Kila siku alipiga fatiha aghalabu Maulana aliokoe familia yake kutokana na masumbufu ya ulevi, umasikini na utundu.

Dua na maombi ya kipenzi cha mtu yalijibiwa muda si mrefu. Mwezi ya kwanza mwaka huo, kabla ya sisi kuingia darasa la nane. Darasa la kazi ya kujikaza. Darasa la kuweka mipango na mipangilio ya kila jambo, kila swali, kila jibu na kila wakati nafasi yake. Kuwa darasa hili kulikuwa gora moja na mwanafunzi aliye macho kidato cha nne. Haya ninayoyasema anayafahamu na yamemfanya mtulivu vile alivyo. ana kazi.

Mwezi huo ndipo ombi la mama yake Chachania lilitimia. Yalikuwa majira ya kufungua mwaka. Yaani siku ya mwaka mpya. Bwana Koja kama kawaida yake alikuwa amekesha pamoja na jopo la werevu wenzake kwenye baraza la wazee. Walikuwa wakivuka mwaka kwenye banda lao la mgema mashuhuri Masazoni, Bi Chotagora.

Baada ya kupupia na kubugia makopo ya shibe yao, kila mmoja aliaanza safari ndefu ya kufika makwao. Tayari walikuwa wamemaliza saa zisizopungua kumi kwenye himaya yake Bi. Chotagora.

Njiani, Bwana Koja alisikika kama mnadi. Alisifia sana tembo la mgema wao. Ulevi wa kuuvuka mwaka ulimnoga kupita kiasi. Alijipata akitembea kinyumbe na mwendo wake wa kawaida. Alikuwa anaelekea kivukoni *–dajara la Marambo*!

Usiku ulikuwa mtulivu. Sauti za kereng'ende hazikuwapo. Waliotawala wakati huu ni paka na bundi waliobadilishana milio kana kwamba wanazozania kitu.

'*Miaaoo'*

*'Huhuuhuu'*

*'Mwiaauu!'*

*'Hu! Hu! h u! Huuu*!'

Sauti zao wenye usiku ule zilipishana angani. Bwana Koja

aliwatangazia hata hawa sifa belele za Bi. Chotagora.Hakusita kuwabainishia uhodari wa mgema hiyo wa pekee Masazoni.

Bwana Koja alianza kuvuka mvuko, safari yake kuvika huko haikuwa ndefu zaidi ya dunia na akhera. Wala naye hakuwazia wale mamba walio wafalme wa mto Marambo!

Kwa muda wa jicho kutazama dari na sakafu, mwenzetu alifika darajani. Guu mbele, guu nyuma. Matembezi yake aliyavuta kilevi hadi hapo. Mara kwa mara alipiga mbweu. Aliteuateua kana kwamba ameshiba kupita shibe yake na tumbo lake. Polepole aliingia kivukoni.

Kwa mbwembwe zake za kuwabari wezi njiani, alitumbukia majini baada ya kukanyaga vidato vivyooza kitambo. Ghafula kama fajaa, alikosa hatua. Safari ikasita na kukoma hapo.

*Chubwi*! *Tubwi*! Jitu tambo lilitumbukia mtoni. Aliingia ndani nusura kufikia kimo cha mwisho. Alijigundua kuwa hapumui hewa ya kawaida. Alihisi mwili wake ni mzito sana na anaenda mwendo wa kiajabuajabu sana.

Maji ya mto yaliiosha pombe ilimkolea hadi akilini. Akabaini kwamba anakufa maji! Akaanza kupiga mbizi kwa hofu kana kwamba amefikiwa na ngwena tayari. Ungemwona alivyoogelea, ungemmithilisha na nyumbu wa Maasai – Mara!

Ajabu ya shani. Mamba wote walikuwa nyanda za juu wa mto Marambo. Walisikia mipapatiko ya maji. Wakaelea aliko mzee wa watu aliyekuwa anang’ang’ana kuokoa maisha kwa kila njia.

Kila mtu Masazoni ni bata wa mto ule. Hivyo, Bwana Koja hakuwa na ulegevu wala ulelemama wa kutopiga mbizi. Alipokaribia kingo za mto, mamba mmoja alimfikia na kumtandika pigo kali kwa kia lake lenye ngozi ngumu iliosisimka.

" ***Twaa!***

***Uuwiii!***

***Waaii!***

***Saidia!***

***Nafa mie!***

***Watu! Watu!***

***Maji! Mamba!"***

Bwana Koja alipiga kamsa uliomfanya mamba yule kuona huruma. Ukemi wake haukusikia mbali kutokana na maji aliyoyameza kila alipokifungua kinywa chake.

Pigo alipopata lilimfikisha kwenye ukingo wa mto ule. Bila fahamu alilala hapo kimya kama maiti. Asubuhi ya siku ndipo aligunduliwa na kina mama walifika kuteka maji. Kelele zao za tafarani zilileta wenyeji wote wa Masazoni.Hata sisi wanafunzi tuliokuwa tukivuka daraja kwenda shuleni. Tulifika na kuwasili kujionea kwa macho yetu.

Kundi la wavuvi lifika pia. Wavuvi hawa pekee ndio walikuwa na ujasiri wa kumkaribia na kumgeuza bwana huyu aliyelala usingizi wa pono kwenye matete yaliomea na kushamiri pale mtoni. Kila mtu alijua kuwa mwenzetu huyu ameshakata kamba zamani. Kumbe sivyo. Alipogeuzwa, alishutuka kwa kukuru kakara. Aliinuka chapu chapu kana kwamba amewaona mizimu wa kale!

"Songa*! Ua! Toka! Mamba! Mamba*!"

Bwana Koja aligeuka chiriku. Alitulizwa na wavuvi wale. Kutoka siku hiyo aliamua kuyataliki ya wazee. Hakutaka tena kusikia ushawishi wa

Bi. Chotagora!

***

Upande mwingine, yule, Makusudi huwenda aliingiwa na ruhani mmoja aliyemtoroka baba mtu! Uanafunzi aliuvua na kuutupilia mbali. Yaliowahi kumpata babaye hayakuwa ithibati tosha ya kwamba maisha hayana mzaha!

Alijishughulisha na yake na kusahau kuwa kazi iso faida si ada kuitenda. Alichukua mkondo mpya. Mkondo wa kuwa alivyo sasa. Ila usiku wake wa kuwa jizi hukuwa mrefu. Usiku huu wa Ijumaa ulimtishia kumpa kichapo kitutu. Na ulifanya hivyo.

Baada ya kujipokeza dozi zake. Akili huwa zinamvuka naye huzivua na kuzitupilia mbali. Anakuwa mtu na nusu. Alhamisi, alijituma kwenye shamba na mjane mmoja aliyejenga makaziyake karibu na mbavu za shule yetu.

Alipenya kwenye tundu lililokuwa limeundwa na wanafunzi walipenda kuvamia maembe na mapera. Yeye hana hamu na matunda ya vitamini, Lengo lake lilimsukuma palipo kuku na bata. Alitambaa kama mjusi hadi akafikia kizimba cha ndege wale. Mkoba wake wa gunia akauweka chini na wazi. muda wa dakika ishirini. alikamilisha kazi ya kuwakamata na kuwa tumbukiza kwenye mkoba wake. akawa tayari kuenda kuwauza sokoni.

Nuksi huja na siku yake. Watumishi wake Mama Maimuna yule mjane, walimwona Makusudi na vitimbi vyake. Bila kusita

wakamtimua mbio. Alikwepa huyu na kumvuta doji mwingine. Hakuwa mzito wa mwili wala miguu. Watumishi walipambana naye kama kwaba wanamfukuza kuku. mwizi wa kuku amegeuka kuku kwao. chenga kwa chenga nyingine ndivyo alivyozidi kupambana Makusudi.Alipofikia tundu la uani, alijilaza chalichali ili ateleze hadi upande mwengine. lakini watumishi naowalikuwa na mawazo sawa naye. waliponyokea tundu wate na kukutana ana kwa ana. Bila kelele wala kamsa nyingi walimrudisha ndani huku wakimchunachuna. Mama Maimuna aliwachukia sana watoto wa Chumio na hasa waliotoka maeneo ya Mtemanyuki, Masazoni na Kichakamkwajuni. Adawa yake ilitokana na namna walivyoharibu mazao shambani mwake kando na kujisiteri njaa. aliponwana Makusudi, moyo wake ulivimba hasira hata zaidi.

Huyu ndiye mtoto aliyemkataza mpwa kwake kutotembea naye bila mafanikio yoyote ya kusikilizwa. Huyu ndiye aliyemfanya mpwa wake akaacha masomo na kutoroka bomani, alipotea mbali bila kujulikana aliko kuendea. Hadi sasa. mara moja, simu ilipigwa na askari wakafika kumchukua mwizi. Haja yake Mama Maimuna ilikuwa kijana huyu afungwe jela ili arekebike. Na alihakikisha hatua hiyo itafanyika bila msukosuko wotewote. Masikini Makusudi.Ukungu wa balaa ulimnyemelea polepole.

Ukungu wa kiza na balaa ulimfikia kama mawimbi ya bahari tayari kumwangamiza potela pote. Hakuwa na jingine la kufanya kando na kujisalimisha kwa walinzi wale waliomnyooshea mitutu ya bastola zao.

Askari waliomshika walimshurutisha asonge nao kulikokuwa na magari yao. Walitembea taratibu wakiangazia hali yoyote ya dharura inayoweza kujitokeza. Makusudi alijuta na kusaga meno siku hiyo. Hakuwa na ujanja wowote wa kumnasua. Alijihurumia kama sungura anayezama matopeni.

Aliwaona wale askari polisi waliomkamata kama ule usiku wa Ijumaa.Usiku alioshiriki kuiba Benki.Alijionea yeye mwenyewe kuwa matendo yake wamekuwa mawimbi ya dharuba yaliyotaka kumwangamiza. Alitazama sare yake ya shule kwa jakamoyo kuu. Alijua ujanja wake umefika ukingoni. Ruhusa na idhini aliomba imegeuka kuwa nafasi ya kuiba na kunaswa. Ama kweli,ivumayo haidumu nazo mbio za sakafuni huishia ukingoni.

## SURA YA KUMI NA MOJA

Ukweli, Makusudi alikuwa hajui kufa hata alipolifumbiajicho hatari. Hatima yake sasa anaitazama kaburi. Mkia wa utundu wake ulikuwa tayari wakatika. Machozi ya majuto yalianza kumlengalenga machoni ovyoovyo. Pale kituoni Kijutoni, sarakasi zilipamba moto. Makusudi alikuwa angali kwenye seli yake. Hayawi hayawi huwa. Siku yake kuenda mahakamani ilifika. Mlango wa seli yake ulifunguliwa na mlinzi aliyekuwa karibu.

Mwangaza ulipomfikia usoni mshukiwa Makusudi, alishukuru kuvuta tena hewa huru ilioingia humo chumbani. Punde si punde, askari wawili wakaingia mle ndani kwa tafarani na vishindo vya tembo. Walimtia pingu mkononi bila kuupoteza muda wao huku wakimweleza bayana kuwa atakalolitamka kiholela litamwandama kama jua na mwale hadi kwenye meza ya hakimu!

Kisa na maana, asijaribu kuuchonga ulimi wake kushinda ulivyo. La sivyo, kujiuma kwake chanda kinywani kutakuwa kwepesi mno. Yaani, angejitia kitanzi mwenyewe kwa kupayuka bila haja.

Alianza kuuona mlango mwingine wa maisha. Mlango huu hakuwa ameuzoea wala hakujua kama angeweza kukabiliana nao endapo ataruhusiwa kuingia ndani, kila alipojaribu kuujengea picha mlango huu, aliona upweke wa uvundo. Aliona hali ya kutojiamini.

'*Yeye ni nani wakati huu*?' Aliona kila doa la kosa lina mizani yake ya kulipwa na kulipiwa. Alijiona mdeni asiyejua alipe nini na kwa thamani gani. Haya yote yalimwonesha wazi kuwa *siku ya nyani kufa, miti yote huteleza*. Aligundua paruwanja kuwa amefikwa na ukiwa wa mashakafundo.

Ingawaje alitembea kwa mwendo wa polisi wale hakuwa nao kiulimwengu hadi pale waliposimama. Alipozinduka kutoka kwenye fikira zake za mbali, aliwaona askari wakimwashiria jambo la kufanywa huku wakiwa wamekosa subira naye. Nani asiyejua kuwa mvunja sheria

habembelezwi!

Askari wale walikuwa wamemwelekeza kwenye karadinga lao lingine. Ishara waliompa ilikuwa rahisi, ajipandishe aingie kwenye gari. Akafanya hivyo bila kusuasua. Akiwa pale garini, alianza kutanabahi jinsi mambo huwenda yakawa ya kifuu cha nazi kweye tanuri la moto mkali! Safari ya kwenda mahakamani ilikuwa karibu kung'oa nanga. Saa kama tatu hivi baadaye.

Huwenda yakawaka moto mkali au yakawa magumu sana kwake kuyavumilia ingawa matendo yalikuwa yake mwenyewe kujitakia. Yote haya yalikuwa kwake kama mwiba wa kujidunga. Akakumbuka kuwa ni kweli eti, '*mdharau mwiba huota tende*!'. Mawaidha ya nasaha aliyopewa bure pasi gharama, yamegeuka shubiri chungu. Maneno ya kumrudi yalianza kumwonyesha kijana mtu kuwa hayatoki kinywani bwerere pasi na maana kuwa.

Mathalani, alijua kuwa ni dhahiri na shahiri makosa aliyoyatekeleza yatamwamisha ulimwengu wa watu wengi walio huru na sauti zao. Katika mipigo ya moyo wake aliona ni vigumu kupata huruma ya hakimu kuhusu kesi yake ijapokuwa alishaizoea mahakama na mahakimuwake. Ilikuwa sawa na kumshawishi Firauni awaachilie wana wa Iziraeli warudi Kanani.

Kwa umbali wa mawazo yake, alijenga picha ya ujasiri wake namna ambavyo unaweweseka sawa na sumu kali inayopashwa moto. Hawezi kamwe kuyakubali makosa yake ingawa nafsi yake inamshutumu. Sumu ya kutenda makosa ilikuwa kali mithili ya mamba. Alijaribu kujiona atakavyokuwa baada ya hatima yake kuamuliwa mahakamani. Majuto yalimkodolea macho kwa hamu na huruma. Kwani yote haya yalikuwa mazao ya matendo yake tu. Akiyafikiria haya, gari lilimaliza safari yake. Lilikuwa limefika kwenye gereza la Shikadabu.

Kila mmoja aliye garini aliteremka na kuongozwa ndani ya

magengo ya gerezani. Sauti ya makuu na majuto ilianza kumwimbia wimbo uliomkera mno pindi tu alipofunguliwa mlango wa seli. Chumba alichoingia, kilivunda harufu kali ambayo kutokana na hali ya mawazo yake kwa sasa hakufaulu kujua inatokana na nini.

Vilevile, giza la kutisha lisilo na kivuli lilitawala viambaza vya chumba hicho. Mlango ulipojifumba nyuma yake. Hakupendezwa na chochote muda huo wote. Si chakula alicholetewa si mavazi ya gerezani aliyolazimishwa kuvaa pasi na hiari. Alikuwa na kiu ya ncha kali kutafuta uhuru uliomtoroka na kumteleza kwa bahati mbaya. Ama kweli, *maji yakimwagika hayazoleki*. Ajabu ni kwamba, alifahamu kuwa bado hafai kuwa mahaabusu kwani hajafikia daawa yake kortini. Walakini, mambo ndivyo sivyo. Ndivyo alivyo sasa. Askari alimfanya hivyo kwa utundu na ulaghaifu wake. Ama walitaka apate ladha ya adha za jela kabla ya kurudishwa dunia wa hewa safi. Apate fursa ya kuangazia ilani kwa watundu wenzake mitaani mathalani aisifu mvua iliyomnyea Shikadabu.

Alitingwatingwa na shauku ya kutafuta mawaidha na ushauri wa kujinusuri alakulihali. Ila kwa sasa amechelewa sana. Labda walio pamoja naye pale selini watamsaidia na kumfariji.

Ila, alikula ng‘o! Kila aliyemzingira pale korokoroni, alijitia hamsini zake seuze kutamani kupiga soga naye. Nani kwa hakika angempa mkono wa usaidizi iwapo wote ni mahabusu? Kumbe shida haina rafiki! Sio uwongo waliposema Waswahili kuwa *mwiba wakujidunga huambiwi pole*.

Kutia msumari moto msibani, hakuna yeyote wa mnasaba naye aliyefaulu kuwa na moyo wa kumtembelea wala kumjulia hali kule Shikadabu.Upweke ulimpakata na kukataa katakata kumwachilia mwanetu. Sasa, alijua wazi ya kuwa nasaha hazifai kupuuzwa hata chembe

Haya yote yalianza kujidhihirisha na kumwagika paruwanjani

pindi mkono wa sheria ulipoanza kuwarapua viboko mmoja baada ya mwingine. Kila mmoja alitumwa kwa mahakama iliomsubiria.

***

Tarehe kumi, mwezi wa aruba. Ni siku iliyompa wahaka na wasiwasi mkubwa. Akawa kama jongoo aliyetembea kwenye kijiti kilichoanguka motoni. Alitetemeka si haba.

Siku hii alichukuliwa na kubebwa yosayosa kutokana na ukaidi wake wa nzi. Askari aliyembeba kama gunia la robota za pamba, alimwelelekeza moja kwa moja hadi paliposimama karadinga la mahabusu sugu.

Gari hilo lilikuwa na jina maarufu. Liliitwa '*Binti Maria'*. Sijui mbona. Lakini wengi waliowahi kubebwa au kunaswa nalo, wamedai kuwa linakuombea dua na sala nyerezi za kukufikisha salama salmini gerezani!

Majibwa kadha wa kadha yalianza kubweka mibweko ya hamaki pindi tu alipopitishwa mbele yao. Ni bayana hayakupendezwa na harufu yake au jinsi alivyowatazama kwa hofu. Yalimtolea chengo zao tayari kumg'ata na kuugeuza mwili wake kuwa chinyango za buchari.

Yalimtamani kwa mate ya fisi awe midomoni mwao ili kumpa adabu na adhabu ya aina yake. Waskari walimpitisha hapo kwa harka. Nje ya seli, kikosi cha askari kilikuwa makini kikishika doria nyua nzima ya kituo cha polisi cha Kijutoni.Walipishana huku na kule sanjari chanjari sawa na akrabu za saa. Ulinzi wa Shikadabu ni kazi na kazi

haina mchezo.

Kwa dakika chache Makusudi alikuwa ameabirishwa lori la polisi tena. Kimya akatulia ndanimwe huku akishukuru zahama aliyojinusuru kupata selini.

Alipoketi kwenye kiti cha ‘*Binti Maria*’, alionja afueni kidogo. Alipata utulivu wa aina fulani uliomjia ghalfa. Utuvu huu haukuwa wa kawaida hata akadhania ni zile sala na dua za gari lile zimeanza kutimia! Moyo wake ulikuwa unadunda sambejambe kwa woga. Haukuwa na raha. Wasiwasi aliokuwa nao ulipunguza kasi ya siku hiyo. Siku ikawa na mwendo wa kobe na kasa.

Ukweli ni kuwa, afueni aliyoipata ni kuwa nje ya seli zile za harufu kali na giza totoro lenye ndoto za kutisha kando na wale mbwa wakali. Pale garini, alikaa sako kwa bako na maghulamu wengine asioweza kuwatambua kabisa. Kutokana na aibu ya makosa yake alishindwa kuwatazama jicho kwa jicho. Kwani nyuso zao zilikuwa kavu kuliko wake wa kujishukushuku.

Nyuso zao zilikauka aibu aliyokuwa nayo yeye na zilishiba shibe ya ukaini na utukutu kama juju wa majuju. Kwa kuwaangalia tu, Makusudi alibaini kuwa wapo watundu kuliko tandu mwenyewe! Akasikitika kwa kukosa muda wa kuwashauri wenzake wasirudie waliyoyatenda.

Lango kuu la kituo cha Shikadabu lilifunguliwa wazi na askari bawabu. ‘*Binti Maria’* likashika njia na barabara kwa kasi huku king‘ora kikisheni anga.Magari yalikuwa njiani yalitii amri na kujibari kando kando.Walipofika karibu na daraja la Mirambo,mahabusu na askari waliachwa vinywa wazi kama changu walionaswa na kutolewa majini.Ajali isio ya kumithilishwa ilikuwa imepiga kambi pale darajani. Ilihusisha lori la shehena ya makaa na tanka la mafuta ya Petroli.

Kijigari kidogo na bovu kama katara kiliponea kubanjwa ovyo kama mabamba wakati wa ajali hiyo. Kando na hayo, ng‘ambo ya pili,matwana moja ilikuwa imebingirika bingiribingiri nje ya barabara

hadi kwenye kingo za mto Mirambo.

Manusura na mansura pamwe na wapita njia walioshuhudia hali hiyo walisema kuwa matwana ilioanguka mtoni ilikuwa ikijaribu kukwepa kugongana ana kwa ana na lori bovu la makaa lililokuwa na ishara tosha ya kisirani hapo barabarani.

Makusudi na washukiwa wenzake walitazama nje kwenye dirisha vilivyokingwa na nyaya nyembamba za chuma, waliona yale yalikuwa yakijiri huko. Alikumbuka ajali waliowahi kuisababisha miezi mitano iliopita. Akameza mate machungu. Sauti za dereva na mteja wake wa benki kwenye taksi ile iliopata ajali siku ile, zikamsuta sana. Sauti hizo zilimkaripia kwa ukali hata akakosa pahali pa kuuficha uso wake. Alijaa hatia kupindukia. hata wendazao walimdhihaki.

Alikumbuka masihara waliowahi kuyatenda hapo nyuma na kujutia sana. Ushauri wa Mwalimu Kadiri ulinjia na kumtulia tena katika safari yake ya kuelekea kortini,

"*Pele haligeuzwi jupi, kila binadamu ana udhaifu wake kila mmoja wenu ajaribu kuujenga uduni wake kuwa bora. Najua mwaweza. Tafadhali maisha yasikuangushe kingalingali.*".

Maneno haya yalimchoma sana kwa kuwa aliangushwa chali na maisha yake. Maneno ya mawazo yake yalimwamidisha ukweli mchungu uliompita mishipani mwa mwili wake kwa spidi sawa na lori la Binti Maria lilivyotegemea njia. hana jipya wala geni, alisalia akiambizana na moyo wake mpaka mwisho wa safari.

## SURA YA KUMI NA MBILI

Sasa.Makusudi akiwa kizimbani mahakamani alitetema sana ijapo alijipigia moyo konde. Alikuwa tayari kujitetea kwa hali na mali angaa apate kuuonja uhuru wake kwa mara nyingine tena. Alisimama titsi akimsubiri jaji mwenye hatima yake afike.

Ubongoni mwake. Hapo kizimbani. Alijiona sawa na mangisi ijapokuwa hali zao zi tofauti. Walisubiria kifo ingawa mmoja wao ywafa kifo cha halali yake na mwengine ywakipokea kwa haki yake. Mmoja wao ndiye mhalifu na mwengine ni kitoweo tu.

Alijichukua kuwa kuku kwa sababu ya utawa wa shida ulioanza kumnogea utamu huku jibu lake la kujifanya msiri kwa watu likitishia kumchubukia kwenye kipini cha hukumu ya leo. Alikuwa kuku anayesubiri kuchinjwa kichikichi kwa hanjari ya chinjachinja! Hana bahati ya mtende.

Wingu la hisia za soni na simanzi lililovurugika, lilizidi kutambaa pale kortini pindi tu hakimu alipotia guu. Mimi, kina Chachania pamoja na wote wamjuaye Makusudi, tulitundika macho ya huruma tukisuburi kwa hofu na wahaka yatakayojiri kadamnasi yetu. Pasi na kujua la kutenda. Tungefanya nini jamani? Tumtetee vipi rafiki na ndugu yetu? Dua tu.

“Leo hii, tulijua eti *uwongo wa sikio si ukweli wa macho*! Ukweli huu ndio unaomchoma sana Makusudi.Aliyoyatenda, yalikuwa wazi kana kwamba ni doti jeusi tititi kwenye kitambaa cheupe pe cha Malkia.”

Hakimu wa kuikata daawa hii alifaa kuwa Siti Kaliamti.Mkazi wa Kichakamkwanju karibu na mtaa wa Mapona kaskazini. Jaji huyu alifahamika sana kwa ushupavu wake wa kudhibti masa sugu na yaliokuwa chege kama yake Makusudi.Alikuwa kama msumeno oto kwa wengi walio waasi waliomfahamu kila alipoivaa sura ya ujaji.

Hakuwa mwepesi wa kupinda shingo kwa jambo lolote lile. Hisia na sheria hazikumpiga chenga kwa wakati mmoja. Alizidhibiti vilivyo. Kupitia kwake, wengi wakutajika tu wameyaonja makali na matamu ya hukumu yake. Amewachuna na kuwachunua wengi wenye maovu wa kila rika na cheo seuze kwake Makusudi! Mara kadhaa, maamuzi yake yalichanga bia kwingi ufasaha na ufanisi wa usawa katika jamii yetu. Wenyeji walimpenda kwa hilo. Kesi ya Makusudi ilifika mezani mwake kutokana na haja ilimpata jaji Tanga, amabaye mara nyingi alishughulikia kesi na matatizo ya vijana. Lakini kutokana na dharura ya kufikiwa na ukiwa nyumbani alikolelewa ilimbidi amwachie Bi. kalimati kuendesha shughuli za mahakamani.

Mkondo wa daawa ya Makusudi ilitia nanga. Kwenye meza ya hukumu, Hakimu, Siti Kalimati akawa wima na ange kudhihirisha upanga wake ungali na makali yale yale ya toka zamani. Alisikiliza kwa umakini wa aina yake.

Macho yake yenye umbo la gololi, mara hii aliyafumbua kiasi cha haja mpaka yakawa madogo, yakawa sawa na njugu. Mara kwa mara, alionekana akikuna pua kisha anajituma kuandika chini mawili matatu yaliomfikia akilini.

Korti ilikubali kopo la ukimya. Tuli, kukatulika. Masikio yalitegeka ndi! Kila neno na kila kitendo hakikutupita. Tulijishuhudia wenyewe. Wakili wake Makusudi aling'ang'ana kwa udi na uvumba kumtetea. Kwa upande mwingine.

Waliomshutumu Makusudi mathalani hawakuikosa mishale ya kutuma na kufuma. Washtaki hawa walikuwa wamejiandaa vilivyo kwa mashtaka yasiopingika.

Pindi tu aliposimama kugangua yake (*Mwakilishi kesi wa askari waliomnasa Makusudi*) Bi. Nasagango.Mambo yalienda tenge. Mshtakiwa Makusudi hakuwa na pa kujificha wala kujisiteri. Matumaini yake ya kuwa huru yakakaidi kabisa kukaangika chungu

kimoja na kesi yake.

Bi. Nasagango –mkazi wa Mtemanyuki ambapo shule ya Kidoa huwa, alianza kufungua ushahidi wake. Alinukuu kwa uangalifu kila jambo lilowahi kutokea. Alirejelea makala mbalimbali ya ithibati pevu. Alimhoji hivyo huku akiutafuta ukiri wake Makusudi ambaye ukimtazama vyema, alikuwa mtu aliyegeuka maji. Tulio kando, tuliona wazi kuwa, hajiwezi kamwe.

Kucha zake Bi. Nasagango zilizidi kumshamiri kumrarua ngozi. Ushahidi wake ulimiminika kama maanguko mbele ya meza yake karani wa korti na hakimu Bi. Kalimati.Wakili wake pia alilemewa na hali kwani aligonga mwamba kupata njia za kumwokoa Makusudi.

Ingawa alijaribu awezavyo kumpigania Makusudi, jitihada hufika kikomo. Hali ilikuwa si hali tena. Ni wazi na bayana kama mwangaza wa mchana kuwa anayemtetea ana makosa chungu nzima. Hata yey, kama kaumu nzima, alisubiria huduma za huruma za Jaji. Angetoa uamuzi gani? Wapo watu wengi walijiuliza swali kama hilo.

Siti Kalimati aliipokea kesi baada ya mjadala mkali ulioibuka kati ya mawakili wale wawili. Alianza kwa kuugonga mpopota mezani kuashiria ukingo wa kuikata kesi. Sisi sote tulihohosa kwa muda. Wakati huo. Alirudia kuzitazama karatasi kadhaa zilikuwa mbele yake.

Akazikagua moja baada ya nyingine huku akizigawa kwa pande mbili. Kuna zile alizoziweka upande wake wa kulia. Nyingine alizitosa upande wa kushoto ilhali kulikuwa na chache alizozikusanya karibu kifuani. Alipokamilisha shughuli hiyo, aliirudia mahakama na kikao cha kesi.

Akatoa sauti, akasema; “Kulingana *na kesi hii, tuna mengi ya kujiuliza. Kwanza, wewe Makusudi, ulifikira nini ulipojizamisha katika mambo kama haya? Hujawahi kuonywa na yeyote kweli? Naona unajuta. Pili, umekubali mwenyewe kuyatenda yanayosemwa mbele*

*yetu leo hii*?”

“*Naam, mheshimiwa hakimu. Mimi kama mshtakiwa. Najuta sana. Najuta kuwa na nta sikioni. Nilionywa ila nilikuwa sikio la kufa wakati huo. Sikusikia dawa wala sikuhitaji kafara jamani. Nakiri kuwa bubu kiziwi muda huo wote. Ninakiri kuwa ni ukweli yote yanayosemwa mbele yetu. Ninawaomba radhi. Wewe unanifahamu vyema.*” Makusudi alizungumza huku ametutupia uso uliojaa shufaka na huzuni.

Bila shaka alihitaji msahaha wa mtu kwa njia moja au nyingine. Baada ya kukiri yake,aliushusha chini uso wake na kunyamaza kimya.

Kitete si kitete kilichotujia, kilikuja kutokana na kuwa tutatengana naye. Michezo tulioicheza uwanjani, tusingecheza naye. Hatutakuwa pamoja kwenye maisha ya kawaida. Pengine Bi. Kalimati kama jaji abadili mtazamo huu. Shuleni Chumio hatakuwa kielelezo chema. Si kwetu peke yetu. Walimu wetu Bi. Sonia na Bwana Kadiri watapoteza mmoja wetu. Wazazi wake watamkosa sana.

Bi. Kalimati alimtupia jicho pia. Aliendelea kuikata kesi yake. Macho yake ya mwewe yalipitia kwa haraka faili la kesi hii. Jalada hilo ilikuwa limewakilishwa na Mwendesha mashtaka alikaa bega kwa began a karani wa korti ile. Alisafisha tena koo yake na kuitazama mahakama.

“Ushahidi *uliopo hapa unadhibitisha kuwa umekuwa mhalifu na mwizi. Umeshiriki wizi wa kuku kwenye shamba la Mama Maimuna.Sheria haziruhusu wahalifu kuwa watundu wala huru. Hivyo, huna budi kukubali kurekebishwa tabia na hulka zako mapema. Wewebado una umri mchanga. Msichana mrembo wa haja. Nadhani wafahamu kuwa chuma kiwahi kingali moto. Chukua nafasi hii ujirudi. Kifungo chako kinaanza sasa. Utakuwa kwenye gereza la kurekebisha maadili la Shikadabu. Natumai ukitoka huko utanipa mimi tabasamu. Hamna dhamana wala haja ya kukata rufaa. Kesi imekwisha.*” Bi.

Kalimati aliizima kesi.

Umati wa watu ulibaki tuli. Sio wa ukimya sio wa ukelele. Wapo miongoni mwao waliokumbuka jinsi nyota yake ilivyometa na kung'ara miezi michache iliotangulia. Sasa amebaki si wa salamu si wa mitajo si wa kuigizwa si wa chotechote.

Wazazi wake walitoneshaneka si haba. Walimu na marafiki walimsikitikia. Aliibeba aibu na izara kichwani. Alisimama kizimbani asijue afanye nini. Askari wa korti alimwongoza kwengine baada ya Bi. Kalimati kuondoka mahakamani.

Nilipomtazama kwa mara ya mwisho. Sikuuona usodai na utadi waka kama alivyokuwa zamani. Amebadilika.Alikuwa mnyonge asiye na usono kwa lolote. Alilia kwa kite tu. Machozi yalijiundia vijia vyake kwenye uso wake wa ujana. Alibubuja na kusononona. Msiba huu alijitakia mwenyewe. Jamani hakujua, mwiba wa kujidunga…….

Kutoka hapo, hatakuwa Makusudi wa kucheka na mcheshi. Nilimwona akitumbua macho kama kibawanta. Mafuta ya kikaango chake yalikuwa yameiva. Mara hii, hakujiona kikaangoni bali kwenye moto wake. Hukumu ya Bi. Kaliamti ilidhihirsha hayo. Makusudi alibaki akimeza mate machungu, shubiri kando.

# SURA YA KUMI NA TATU

‘*Lipitalo, hupishwa*’. Makusudi aliyapishia njia yaliompata bila kinyongo. Siku nazo ziligandamana na kukataa kusonga kama alivyozitarajia mwenyewe. Zilijikokota polepole kama hatua za kobe jangwani. Licha ya hivyo, kuishi kwa Tashi jelani kulisalia tu kushikilia kamba ya subira huvuta heri. Tena, kujijutia na kujililia, kulibakia ada yake kuche kusiche.

Maadamu kifungo chake kilikuwa kingali kikaangoni, msururu wa ikabu na viboko vya kumkumbusha jana yake vilizidi kumpa uzinduzi kuwa mdharau mbiu hubiuka yeye. Fikira za laiti angalijua zilimsumbua na kumkengeza kila mara.

Kila alipoketi peke yake, alikumbuka bila kwenda chelele jinsi tulivyong`ang`ana kumpa nasaha. Alijitathimini kwa kina. Aliona hasara kubwa kujiunga na magenge yale ya wevi sugu na walanguzi yaliomwaribia sura na umbo la maisha yake.

Tama na ashiki yake ya kujitajirisha kwa mkono wa kushoto kumemrambisha garasa. Amejiingiza kwenye kisima cha jitimai bure bilashi. Ila sasa alielewa eti kupata si kwa werevu tu na kukosa si kwa ujinga pia. Kila kitu huja na muda wake na nafasi yake. Kwani, *Mungu hamnyimi ajitumaye*.

Hata hivyo, bado alihitajika kurithi maovu yake. Visa vya ukali wa hukumu yake vilimkubali na kumkumbatia. Mathalani vilimfika kooni bila yeye kupenda. Hakuwa na jingine bali kuvumilia tu. Minong`ono na vilio vya kite havikuyapunguza makali ya ufungwa wake.

Waama, alihitajika kufanya kazi za shokoa kama punda wa dobi. Shughuli hizo za gerezani, zilimvisha maadili mapya kabisa hata akawa zaidi ya mfano wa Makusudi tuliyemjua pale zamani.

Kwa kipindi cha miezi mitatu gerezani, alianza kunyenyekea

kwa uadilifu sawa na mtwana. Hakudhubutu kufuga pembe za sungura tena. Alijipiga msasa zaidi katika mienendo yake. Akajirudi sana na kujitenga na mavi ya kale ingawa hayanuki. Hakutaka kupiga darubini, kutazama wala kuangalia mambo ya zamani bali alitarajia kujiatua humo.

Naam, angali alikuwa mcheshi hata huko gerezani. Alibaki kuwa mstari wa mbele kuwatanabahisha mahabusu vijana kwa wakongwe kutorudia maosa yaliowavusha ng`ambo hiyo. Alitumia maigizo mbalimbali kupitisha ujumbe wake. Hakukosa kuwaambia kuwa *tabia ni kia la mwili*. Hivyo, mtu awe makini kutoteleza na kujipata mashakani na mashakafundo.

Kando na kuwa gerezani, hakusahau kuwa angali mwanafunzi. Aliyavulia nguo masomo kwa moyo usiodekadeka. Japo hali ilikuwa ngumu, hakukata tama ya kuirudia elimu. Alijitahidi na kujikaza kisabuni kumalizia kidato cha nne.

Nyota yake ya kuwa mhandisi, alitarajia kuwa itakuja kutimia. Marafiki na familia, tulimwombea dua salama ili amalize kifungo chake akiwa amebadilika. Kuwa kwake jela hatungeweza kukuzuia.

Mtaani, watu waliendelea kuishi maisha yao. Waliyaendeleza ima fa ima na kwa kawaida kama kuwapo kwa chumvi kwenye mapishi ya wali. Tuliokuwa tukisoma shuleni zama hizo, tulikuwa daima mbioni kukamilsha malengo yetu. Wapo wale waliohitimu vyuoni.

Wachache kama mimi na Chachania, tulifanikiwa kuzinyaka nyota zetu za jaha. Tulipenyeza kileleni na hatimaye dhamira zetu za maisha ziligonga ndipo. Kwa yakini, dhamira ni dira. Tulichokitaka tulikipata peupe pe!

Chachania aliangukiwa tuli na ruya yake ya uhasibu. Alifanikiwa kwa bahati na chudi kuwa afisa mkurugenzi wa benki kuu.

Banki hii ilijumuisha hazina kubwa ya nchi za madola. Ni Banki hii hii iliwahi kuporwa na wezi usiku mmoja siku za nyuma. Kwa sasa imeimarika na kupigiwa mfano na benki nyinginezo.

Isitoshe, umahiri na ustadi wake Chachania wa kuhesabuhesabu ulikuwa ungali naye sawa na lulu migodini. Aliboresha hisa za kampuni yake maradufu. Hali ya uwekezaji ilipamba moto kila siku. Wateja waliongezeka kuweka hazina na kuazimwa mikopo. Jina la banki lilimtegemea sana Chachania na weledi wake wa mambo.

'*Mtaka hupata'*, Chachania aliye mwana wa mifupani kwa familia yao, aliibuka kuwa kioo cha almasi kwa wazazi wake pamwe na jamii yetu. Si mtaa wa Mapona.Si Masazoni.Si kichakamkwajuni. Si Mtemanyuki.Si Chumio wala kule aliko kaka yake – Kijutoni.Alienzika kwote kwa juhudi zake za kuanzisha miradi mbalimbali ya kuinua hali ya maisha.

Kwa upande mwingine. Ni dhahiri shahiri ya kwamba, kapu langu la riziki lilijazwa tunu na tamasha hadidi na furifuri. Namshukuru Mungu daima. Nilipohitimu chuoni. Nilifaulu kuwa wakili. Niliajiriwa na korti kuu nchini. Niliipenda kazi yangu ya kuimarisha sheria ambayo nilithamini kuwa ngao ya jamii.

Kazini sikukosa kilemba cha waridi. Nilisifika mara kwa mara. Ushupavu wangu ulijengeka kila uchao. Jina langu halikuwa jina tena bali nembo ya usawa. Baada ya miaka mitatu hivi, nilipata cheo cha juu. Nilivishwa mbeleko kuwa hakimu mkuu.

Mamlaka haya yanilaki pamoja na udogo wangu. Jopo la majaji liliridhia mimi kuwa kwenye kiti cha hadhi ile. Muda huu, nilipiga taswira nyuma, niliwakumbuka kina Bi. Nasagango na Bi Kalimati.Nikadhamiria kwa uchu kuwa mfano wao.

Kila mara, nilijitoa mhanga kukabiliana na dhuluma zozote jino

kwa ukucha. Nilijaribu kwa kila njia kuzidhibiti. Wala sikufurahia wafisadi walipoponyaka hukumu zangu. Ingawa mara nyingi, dua ya kuku haimpati mwewe.

Sote. Mimi na Chachania –mnuna wa Makusudi, tulipenda kazi tulizojaaliwa kupata. Ingawa tulikuwa katika taaluma tofauti tulijitoa sabili kuijenga jamii yetu kwa hali na mali. Kila mmoja wetu alitoa mchango wake kwa njia na nia moja. Tulielewa wazi kwamba; kila mwashi na ujenziye.

Kamwe hatukusahau siku zetu za usogoni. Ndio maana, kila tulipopata nafasi ya kutoa mkono, tuliweza kuchangia anghalau kuimarisha hali za wenzetu.

Kwenye miradi yetu, tuliweza kuwa mamoja na wenzetu tuliosoma nao zamani. Walichanga bia mawazo faafu ya kuboresha majiji yetu. Tulifanikiwa kuunda chama na hata kamati ya kusimamia miradi hiyo. Azma yetu ikiwa ni kuwa na misingi bora kwa kila jambo. Si elimu si mahitaji yetu binafsi.

Kama wanachama wowote, tulijukumika kutoa michango kadiri ya uwezo tulinao huku tukihifadhi kwenye hazina moja. Kwa njia hii, tulifanikiwa tufadhilisha ujenzi wa madarasa ya shule kadhaa, kuundwa kwa barabara za lami, kusimamishwa kwa ndandalo za umeme na kuchimbwa kwa visima vilivyosafirisha maji kwa kila boma kwa njia ya mabomba na mifereji.

Juhudi zetu zilizokuwa mfano wa vichuguu vya mchwa, hazikuwa pachipachi wala wingi wa wasiwasi kati ya watu. Bidii ya kujituma huku ilipokelewa vyema na kwa moyo wa njiwa. Katu wenyeji hawakuchelea kutupa mikono ya shukrani na yenye pongezi kama si baraka. Kwa kuwa dari husitiri paa. Bila wao, hata sisi tuvumao tusingekuwa sisi.

Wengi kama mimi na Chachania ambao ni wanachama wa

chama cha *MAENDELEO NI MSINGI* tulizidi kuifaa na kuipagaa jamii yetu kwa mema kutoka kwa jasho letu wenyewe. Wazazi wetu kando na kuwa majungu makuu yasiokosa makoko, walizidi kutuchnja kwa maarifa yenye busara na hekima tele.

Walituafu na kutushauri kwa mawaidha mengi ya kito na thamani. Masikioni na ubongoni.upo wakati walitushauri tujaribu juu chini kuhamasisha vijana wenzetu kuhusu ushawishi wa marika, matumizi ya dawa za kulevya kando na baadhi ya madhara yanayojitokeza peupe kwenye mitandao ya teknolojia.

Hili lilikuwa ari na ombi la wazazi wetu. Kamwe hatukulipinga bali tulianza kulipangia mikakati. Alijikoleza nta na komango mara hii hakuwapo kati yetu. Kwa kushirikiana, sote pamoja na wanachama wenzetu waliokuwa uta na upote, tuliunda chama kingine. *CHAMA CHA MAADILI NA TALANTA*.Kupita chama hicho, tulifaulu kuwarudi na kuwaelekeza vijulanga wengi waliokuwa wamemezwa wazima.

Tulishirikiana bimithili ya kinu na mche kutwanga nafaka za kuwaelimisha vijana waliotoka kwenye aila za wasonacho na mayatima. Mnato wa jitihadi hizi zilivutia macho ya idara mbalimbali za Elimu.Wafadhili pia walituunga mkono kuwakuza wadogo wetu. Mashababi sufufu walifanikiwa na kunufaika kwa mradi huo wa pili.

Isitoshe, tuliweza kuwapa ilani na kuwatanabahisha wachanga wale kuhusu uja wao. Tulifurahi kuona kuwa wengi wao walikubali kutakaa ushawishi mbaya wa marika. Walikubali kuwa makini. Pengine walituiga –mimi na Chachania.

Tuliwaonya si kwa vidole bali kwa soga letu la kila mara kuwa, watambue sumu ya ugaidi na kutu ya kutopata elimu. Tulitahadhari nao. Wangepiga nasaha zetu, bila shaka njia ya marahaba na majuto ingewasubiri.

Tuliwaonya tukukumbuka kuwa kesho yetu ilitegemea leo yao. Kuwapatiliza wangali wadogo kulikuwa ada yetu. Waswahili husema, tikiti baya li shambani mwako. Haikuwa shere wala pigo la bakunja. Ukweli usiofichika.

Ipo siku, Bwana Koja – babaye Makusudi, alichukua nafasi na hatua ya kuwatembelea vijana wale wa mradi wa pili. Wadogo hao walimpenda sana Bwana Koja.Nakumbuka akiwaeleza maneno yalionigandamana ahadi wa leo. Aliwaambia.

"*Wanangu.Tahadhari kabla ya nini? Ni heri na afueni kujipa tahadhari mapema maishani. Tusifanye mambo kuwa mzaha kama popo. Hatimaye tukajipachika majuto makubwa. La sivyo, akweaye mchongoma hujutia wapi jamani?*" Baba yake Makusudi aliyasema haya akiligogota gazeti la zamani kidogo lenye maandishi makubwa yalikolezwa wino. Maandishi yenyewe yalinena hivi; ***"MAKUSUDI YA JANA YAMFUMA MAKUSUDI"***

Kila barobaro aliyekuwa pale alibakia na jibu kinywani. Walijipata wamempa jawabu kwa sauti moja ya kujihurumia. "*Akweaye mchangoma hujutia kileleni!*" Sisi wengine tuliokula na kuleleka naye Makusudi, majibu yetu yalibakia moyoni. Daima na dawamu, tulikubali kuwa tendo ovu ni kovu la milele…………..."

Muda wote huo, nilikuwa mawazoni nikiwazia ya zama zangu udogoni. Kila kiungo cha mwili wangu kilinong'onezana kwa siri pamoja na akili zangu. Mawazo yaliakisi kila kona ya jumba lile nililokuwa ndani kisha kurudi kwa vishindo vikuu ubongoni mwangu. Hata mara nyingine, nilijipata nimeshika kani na kugombana vikali ajabu na maisha.

"*Wewe maisha, mbona unakuwa lumbwi?"*

*"Hata! Tangu lini nikawa kinyonga? Mimi sigeuki wala sina rangi. Labda niwe mchana na usiku!"*

*“Sivyo, mbona unatugeukia sisi wengine? Wakubali tuwe vipofu wenye macho!”*

*“Jamani, mimi sina muda wa kugeukageuka. Ungalijua natamani sana kufanya hivyo ungaliona mengi. Usingeniuliza haya ila siwezi. Nyinyi wenyewe mna uwezo huo. Si nyinyi mwageuka na kupenduka mtakavyo kama nyoka?”*

*“Sisi! sisi kina nani?”*

*“Nyinyi binadamu! Nyinyi ndio lumbwi! Mwaigeuza mienendo yenu kisha mwanilaumu mimi! Mwone msena wako Makusudi.Si yeye mwenyewe kajigeuza vile ama ni mimi! Sitaki lawama zenu. Binadamu mnikome!*”

Maisha yalinijibu kwa madaha na kejeli. Sikuweza kuyapinga. Yaliniweka wazi kabisa. Sikuwa na budi, niliyawacha yaendelee na shughuli zake. Yalinikumbusha kuwa mkuki kwa nguruwe mtamu, kwa binadamu mchungu.

“*Kumbukumbu hizi za zama zile zingali mbichi akilini mwangu. Zimeniweka kwenye nguu ya tumaini. Zimenifungua macho kweli. Siku zijazo ni kama tumba. Hazijachanuka. Kwa hakika, ya kesho hayajulikani…….*” Niliwaza.

“Muda wa saa moja nimekuwa afisini mwangu nikiwaza haya. Ujana wangu ulikuwa umebeba mengi. Punde.Macho yalipepeseka. Malaika zikaimaima mwilini. Nilizinduka taratibu. Nilianza kuhisi baridi kwa umbali. Nilijihisi kama baridi imenigeuza tango kwenye ngoma za mikwiro, jambo ambalo haliwezikani. Kumbe sikufahamu, nimerudi tena kuwa na umakinifu. Nilikuwa mbali na ukawaida wangu.

# SURA YA KUMI NA NNE

"*Huu si muda wa kupumzika, mbona wasahau Bamkubwa? Zile kesi zatusubiri sisi. Ebu twende kaka*." Kwa utani mwingi – Wakili mwenzangu (Bwana Tandika) alininong'onezea kwa sauti ya chini alipoingia afisini pangu na kunipata kwenye lindi zito mawazoni.

Alikuwa amechukua wakati wake kuniangalia nilivyoganda kwenye kiti na meza yangu. Alisongea karibu meza yangu, akapanga nakala zake chache zilidai kumponyoka mkononi ndipo akanishauri tuondoke. Shughuli za siku zilinukia ubani, zilishamiri kasi kwa sasa. Bila shaka Bwana Tandika alikuwa na jakamoyo. Hakuweza kuniona maeneo fulani pale kortini ndiposa akachukua hatua ya kunitafuta hadi ofisini kwangu. Nilipenda sana kuwa kwenye mkahawa wa korti. Ila leo sikuweza kwenda huko. Nilijibanza chemba.

Nilijirudia ghafla. Huku nikitupatupa macho yangu kila pande za chumba kile, kwa hiari, nilishutukia nimesalimia Bwana Tandika.Nilikohoa kidogo, kisha nikazungumza.

"Hujambo *kaka Tandika? Nikusaidie vipi leo*?"

Maneno yalinitoka juu kwa juu huku akili zangu razini zikinitulia ubongoni kwa mara nyingine tena.

"*Ni mzima mwenzio. Sijui wewe. U mzima*?" Bwana Tandika alinijulia hali.

"Ah, *hofu kando. Nina siha na rihi kama majaaliwa ya Dayani*."

Nilimjibu huku nikivuta akili nyuma kukumbuka alivyonieleza hapo awali

. "*Hivi umesema…. umesema eti ile kesi ipo tayari*?"

Alinijibu huku akinionyesha sajili ya nambari za kesi zilizokuwa kwenye jalada alilolibeba kwa mkono wake wa shimali.

“Naam.Hakika *kesi nambari arubaine na ile ya nambari sabini, kama sijakosea, zimeiva!*”

“Zinaanza *saa ngapi*?”

Niliendelea kuuliza.

“Tumesalia *na robo saa kuanza hukumu za leo bwana Jaji*.”

Bwana Tandika alinijibu kwa heshima na taadhima.

Nilisadiki nikiitazama saa ya mkononi,

“*Aha! Niko tayari. Twende basi tukazitegee sikio*.” Nilishauri.

Kulingana na hali niliyokuwa hapo mwanzo, sikuweza kupata nafasi ya kupitia nakala za kesi zile ingawa nilijua hazitakuwa nyepesi kama zile zilizowahi kutangulia kwenye jukwaa la mahakama yetu.

Niliingia bila mwendo kasi huku waliohudhuria wakisimama kwa utulivu kuonyesha heshima kwa hadhi yangu. Nilikaa kwenye kiti cha mimbari na kuishika mizizi ya kesi. Moja baada ya nyingine.

Kesi ya kwanza, ilikuwa ya tarakimu aruba nne. Ilisomwa kwa kina na karani wa korti. Mshataka ya mhalifu yalihusiana na ununuzi wa bidhaa za biashara kwa njia ya kimagendo. Ilisemekana kuwa alipenda sana kutumia mlango wa nyuma kukamilisha malengo yake. Kwake, hongo ilikuwa kama salamu.

Sikutaka kupoteza wakati kwa waasi kama hawa. Mara moja. Nilimchinjia kesi kwa hanjari. Niliamua apate kifungo cha miaka mitano pamoja na kazi za sulubu. Hayo Niliyaambatanisha kwa faini ya hela zenye thamani sawa na tabia yake ya kuzunguka milango ile ya nyuma!

Hukumu yangu ilipomtua akilini mshukiwa huyu. Jasho la harara ilimpenya kwenye kunyanzi zake za uwongo na ukweli

zilizoashiria hali ya kuonewa huruma. Mwili ulimtetema nusura apepee pale mahakamani. Huwenda atakoma hulka hii akiponyoka au akijitenga kando na hukumu yangu. Jambo ambalo nilihakikisha halitawezekana. Sheria na haki ni lazima zizingatiwe. Mahakama hii ingali yafahamu ya kuwa, ukali wa Bi Kalimati nilikuwa nao maradufu.

Kesi ya pili iliibua hisia. Chaji ya kesi hio ilinichafua na kunivuruga akili na moyo. Ilinikumbusha niliyokuwa nikiyawaza saa zima pale ofisini mwangu bila kujua ni kwa nini. Nilishangaa na kubutaa. Kimako cha limbukeni kilikuwa ni afadhali. Kesi namba sabini na saba iliniigizia uzee na uzimbezimbe wa kuchechemea kwa mchecheto wake.Jina lililotajwa kuwa chanzo cha kesi hii,halikunikaa akilini kabisa.Sikulisadiki ingawa mwenyewe naitwa Sadiki!Sikuweza kusadiki kuwa nimelisikia jina la mtu fulani. mtu nilyemjua fasili na asili yake. Nilishusha pumzi tu na kungoza mtama umwagikie kuku wengi.

Mara hii, "*Makusudi amefanya nini*?" Nilijiuliza kwa hasira na simanzi. Miwani iliyoivaa ikanidondoka ijapokuwa nilikuwa nimeipelekea mikono yangu kuiondoa usoni. Sikuwa na moyo wangu hata kidogo kwa yatakayojiri. Si kwamba namwogopa mtu wa watu. Namfahamu yeye na vitimbi vyake kutoka zama za utotoni. Nilishindwa tu kuelewa ni kwanin hafunziki kwamatendo yake mwenyewe. Nimuda mirefu sasa akiwa nzi mkorofi wa chooni. Kwa kutikisa kichwa sauti iliniambia akilini,

'*Tabia ni kia la mwili*!'

Makusudi aligeuka gaidi sugu. Sugu kuliko weusi wa kaa. Sugu kuliko gaidi la ugaidi. Aligeuka chuma chenye kutu kali. Kali zaidi ya ncha za jambia. Makusudi sasa ni Kutu isiokubali makali ya msasa wala moto. Hasaidiki hatolewi kafara! Haina maana.

Chambilecho Waswahili; '*Kupotea njia ndiko kujua njia*'. Hayo yalikuwa kinyume sana. Kwa rafiki yangu wa zama zile. Nilikubali ya

kwamba amepotea na hana njia kamwe. Alipoteza mwelekeo kabisa. Hakujua njia ya kuridia wema wa maisha. Nilisadiki nilioambiwa na maisha hapo nyuma.

Huruma yangu kwake iligeuka kuwa tabia ya mbogo – mori na hamaki. Sikutaka awe mtihani wa hisia zangu kamwe. Uso uliniiva nusura kuungua kwa hasira na ghadhabu. Nilikasirika kwa sababu Makusudi amegeuka popo wa mchana. Asiyeona japo mwenye macho! Aliyarudia makosa yale yale aliwahi kujutia.

Ila ubinadamu ulinibembeleza kila nilipompia jicho. Jambo ambalo nililikemea sana kwa sasa. Nilijua nikimchelea haki sitakuwa mkweli daima. Nikimtelekeza kama rafiki kwenye kucha za haki, kazi yangu itakosa maana. Hukumu yangu itageuka dhuluma kwa wengi hata Bi Kalimati ataumia pale alipo.

Nilihitaji fimbo ya karibu. Kwani hakuna jambo gumu kama kumhukumu mwandani wako. Asa yule mlieleleka na kulia pahala pamoja. Ni sawa na kujichuna ngozi au kujing'oa jino legevu. Lakini, pasi na undugu wetu, Makusudi amekuwa chubuko lililokataa katakata maadili ya kutibiwa.

"*Nitafanya nini*?"

"*Mara hii Makusudi atamlaani Shetani*!" Niliuambia moyo wangu. Sikuwa na budi bali kutii naye amri ya sheria. Nilisubiri kesi ya Makusudi iwakilishe mezani pale mahakamani.

# SURA YA KUMI NA TANO

Hapa nilipo (kwenye kochi la hakimu) ninao uzoefu mkubwa katika uhakimu. Nimekumbana na washtakiwa waliuona mlango wa mahakama kwa mara ya kwanza pamwe na wahalifu sugu waliozoea vyumba vya jengo hilo hilo. Seuze msena wangu. Huyu aliyevia hulka ya kuishi maisha ya mema.

Nilisongeza kiti changu nyuma na kumtupia macho ya tungule, nilikuwa ninamdadisi na kumpekua huku kesi yake ikikolea kikaangoni mathalani ya iliki na dania mchuzini. Nilikata shauri kujua visanga alizuka navyo mara hii vilizalika wapi.

Miezi mingi ilikuwa imekomaa tangu ujana wetu utufikishe umri wa makamo. Ingawaje siku na miezi hizo zilisukuma miaka yetu mbele, Makusudi alibakia kuwa na hirimu ya kuwa mhuni mkaidi na mkaini kuliko mwanambuzi.

Tulifahamu na kufichua ya kwamba alifaulu kuwa mhandisi aliyetopea na kubobea. Sifa zake za ufundi ilizagaa kwingi kama uvmbi la chamchela. Alifanikisha kujenga majumba ya mayatima aliyafadhili mwenyewe kama mhisani.

Pongezi za dhati alizidaka kama hongera kutoka kwa watu wengi hadi leo anapokabiliwa na mchongeo mzito kuliko daawa ya ibilisi mwenyewe.

Jambo ambalo wakazi wema hawakulifahamu ni kwamba Makusudi si mjasiriamali wa biashara nyingi tu bali pia alishiriki usambazaji na kuuzaji wa dawa za kulevya ambazo zilikuwa mpya na tafauti kwa watu wengi. Tembe zenyewe ziliitwa "***kete***".

Dawa za kete ni za aina yake. Vijitembe vidogo vilivyohangaisha wateja. Kando na hamu kuu iliyowakaba wateja wa vijitembe hivi, waliozitumia walipata mahangaiko kadhaa mwilini. Wengi wao walitabawali damu kama wagonjwa wa kichocho. Mara

nyingine, washindwa kupumua ama kupata hamu ya kutia mlo tumboni. Ladha ilitoweka kabisa. Awe mume awe mke.

Vijitembe hivyo vikawa ndio kite cha kila familia iliojivunia mashababi na mabanati. Wengi wao wakiwa wanafunzi wa shule. Hasa shule zake Bwana Makusudi na mkewe Bi. Chingwena: shule ya akademia ya Chongani na shule ya upili ya Makusudi Senior. Shule hizi zilikuwa na viwango dhabiti vya masomo kuliko zile za serikali. Ilikuwa fahari kubwa kupata nafasi ya kushika elimu katika shule za kibinafsi kama hizo.

Wazazi waliofaulu kuwajumuisha watoto wao kwenye shule hizi za bweni, walipigwa na butwaa sana walipowatembelea. Vijana wao walibadilika hasi. Ni vigumu kujua yapi yanawageuza. Walimu wapo wazuri na heshima zao. Skuli zao zipo na miundo msingi bora na ya kuvutia. Tatizo la vijana walishukiwa kuwa waraibu likawa fumbo la kufumbiwa mjinga, mwerevu Makusudi alishalifumbua na ndiye mkadamu wa mambo hayo mwenyewe.

“Miezi kadhaa iliopita, Makusudi alituhumika kwamba ameshiriki kuwaambukiza baadhi ya wanafunzi wa shule yake ya Makusudi Senoir ugonjwa wa aina yake, asa kutokana na 'chanjo alizokuwa akiwaletea kama matibabu yao’. Aliwabariki uwele uliojuikana kote kuwa na idhini ya kuzingazinga na kugeuka ombwe wa maisha bila hiari yoyote. Wanagenzi hawa walitibiwa tafauti na magonjwa wengine. Walikuwa daktari wao spesheli, aliyekuja skuli siku tatu kwa juma. Waliozidiwa sana waliruhusiwa kwenda nyumbani kutafuta matibabu zaidi.

Lakini matokeo ya wengi wao ilikuwa wana ukosefu wa kinga mwilini. Ndio maana wanasedeka na kuseneneka kila siku zivyosonga. Wazazi wa wanafunzi kama hawa wakosa la kujiliwazia wala kuulizia. Ni pigo kubwa limeshawachapa mijeledi. Kando na uhawinde wao, ugonjwa huu uliwateka bakunja.

Kumbe nia yake Makusudi ya kuanzisha shule zake pamoja na majumba ya mayatima ilikuwa kama zama za zama kongwe – kueneza uraibu wa dawa za kulevya na kuwauza mayatima ughaibuni kama vijakazi. Walimu wasamaria wema katika shule zake walidokeza fununu za habari hizi kwa wenyeji walio Mashombo, Masazoni mpaka Mtemanyuki. Kilio chao kilisikika mbali. Vidonda vya nyoyoni mwao vikatoboka na kupasuka. Maswali yao mengi yakajibika. Wenyeji wenye hasira za mkizi, waliotoneshwa makovu ya zamani,wakapanga kumpa maro ya kupigiwa mfano wakati ujao.

Ni kijitambo kidogo, maeneo haya yalipoteza wana wao kwenye lindi hili lililoongozwa na kina Makusudi.Ilikuwa ajabu sana tena kumwona amerudi kuongeza mizoga kwenye maisha ya wasiojiweza na dhika zao. Wenyeji waliamua kumvamia kama nyuki katika maeneoya afisi yake. Walitaka kumpa adabu yake.

Inspekta Mzoa alimtambua Makusudi na madhila yake toka seezi za vidole hadi nyweleo za utosi wake! Alijua kwa busara kuwa Tashi hawezi kurekebika katu. Mara nyingine alimfananisha Makusudi na madini yenye matiko sugu yasiopindishwa hata kwa nari wa jehanamu! Alimlinganisha sana na ngozi ya kiatu kilichochomeka, hakiwezi kung’ang’anika na kunyeka daima!

Daima na dawamu, Makusudi aliukumbatia imara ujambazi na ulevi wa dawa zake kama kwamba ni sherisi kwenye mbao za seremala. Mawili hayo yalikuwa ngozi kwake kama si mavazi. Alikubali kunuka maovu. Hawezi kuwa mbali nayo. Pengine kwa muda mdogo ama mauti.

Si ajabu wala mauja kugundua eti mali yake sufufu aliojipigia ubwana, ilinawiri kuwa kutokana na mawili yale yale aliyoyaweka moyoni mwake toka zamani. Ukarimu wake uliwapumbaza wasiomjua kwa kina na asili. Ucheshi wake ulikuwa ungali mzima, hivyo kukupiga chenga kulikuwa kwepesi na rahisi kama nini!

Uraibu wa mihadarati ulimgeuza milki na kumtilia nishai bwerere. Kitendo hicho ni kizuizi kikubwa kwake Makusudi na maisha. Yuyu huyu aliyepoteza zaidi ya miaka minne ya ujana wake jelani kule Shikadabu.

Leo amebebwa marshimarshi na wenyeji waliowahi kumpaka sifa njema. Walimgeuka kama kinyonga kutokana na hulka zake mbovu. Wenyeji wa maeneo yote walitamani afunzwe adabu mikononi mwao mara hii.

Makusudi alipatikana kwake akiwa anajiburudisha kwa sharubati ya tikiti na machungwa ya kutoka Misri.Starehe zake za nyani kwenye shamba la migomba ziligeuka kuwa purukushani za mende motoni! Alokwepa kukamatwa na umati wa watu uliokuwa umevamia nyumbani kwake bila taarifa wala ilani.

Kwa bahati, siku hiyo alikuwa na mgeni mwenye mamlaka makuu. Gavana wa gatuzi lao alikuwa amemtembelea. Kuna miradi ya maendeleo ilisubiri kikao chao cha siku hiyo.

Kuvamia huku kulimwacha mtu hoi. Hakutarajia.Ababaika na kutetemeka. Walinzi wa boma lake tayari walikuwa wameshaingia mitini. Waliobaki pale ni mabondia wa gavana. Nao walimzingira Gavana Mwamba peke yake. Watu wenye ghadhabu zao wakamnyanyua juu na kumweka chini tayari kupokeza taabu ndipo afueni ikatokea. Gavana aliwatuliza hasira na kuwahimiza wampe sikio kidogo ana jambo.

Gavana Mwamba alimnusuru mwenyeji wake kwa hotuba yake iliomjengea sifa mwenyewe ijapokuwa alikuwa mwanasiasa aliyetupaka mafuta kwa mgongo wa chupa kila uchao. Hana maendeleo kabisa tangu awe kiongozi wetu. Siku hiyo, alidai bila kupalizia moto ugomvi ulioshika kasi kati ya wenyeji na Makusudi.

“Sabalnuri *Wananchi?”*

*"Aheri Mheshimiwa Mwamba"*

Wenyeji waliitikia utweshi wake huku wakiupunguza moto wa kumaliza Makusudi.

"*Hewala wenzangu. Kwanza nawashukuru kutoshindwa na hisia zenu. Si jambo rahisi wala si mzaha kufanya hivyo. Ahsanteni tena. Ningependa kuwaeleza kando na porojo ya kuwa kuna sheria jamani. Hakuna mkubwa kuliko sheria. Wasemavyo wenye ulimi wa hadhi, sheria ni msumeno, hukata mbele na nyuma. Mbona basi muwe na ari ya kujikata wenyewe baada ya kumkatia mwenzenu uhai? Mpelekeni kortini. Ahukumiwe kwa haki. Nimewasihi wananchi. Halafu makosa yake kama ni madogo tunaweza kuyamaliza hapa hapa tu. Atatoa kitu kidogo afadhili makosa yake. Nawasihi wananchi!*"

Aliwazungumzia akiwa mwingi ukweli na ujuvi. Wananchi walikataa hicho kitu kidogo. Walimtaka Makusudi mzima. Heri wafike mahakamani. Hakika siku hii, Bwana Mwamba alitambua kuwa hata yeye kando na kuwa mtu wa kupagaza maneno bure, siku hii alitoa kauli ya maana sana. Wapo wenyeji waliokuwa na msimamo wa kati kwa kati. Walitaka kuamini yalisemwa na Bwana Mwamba ingawa wanamfahamu kwa jambo mmoja tu, kuna mengi hajawahi kuyatimiza tangu ashike hatamu ya uongozi. Wakafoka.

"*Ndio!*

*Hapana!*

*Atoe kitu!*

*Kabisa!*

*Haiwezekani!*

*Twendeni mahakamani!*

*Hapana!*

*Atemwe hapa!*

*Ale kichapo cha mbwa!*

*Mtandikeni huyo kinyau!*

*Haki itendeke!*

*Polisi!*

*Polisi!*

*Khaaa!!*

*Waje upesi!*

Sauti za wenyeji zilitandika hewani matakwa yao. Muda mchache hivi, Inspekta Mzoa aliwasili na kufika kumnasa Makusudi. Alifika baada ya kupokea arafa kutoka kwa mtu aliyejitambulisha kama mlinzi wake wa nyumbani. Inspekta alipotua hapo. Alipokea kipaza sauti alichopewa na Bwana Mwamba.

"*Hamjambo tena wananchi? Hakika lililo na mwanzo halikosi mwisho. Aah, ninachukua fursa hii kuwashukuru tena kwa uvumilivu wenu na kwa wale waliopiga ripot, pokeeni shukrani zetu za dhati. Tunawadhamini sana. Hata hivyo, huu ndio wasaa na mkao aula kwetu sote kusimama kidete mathalani maboriti ya mashua, kusema kwa sauti moja juu ya mihadarati. Mihadarati hii ni dawa za kulevya. Sumu kali kati yetu na vijana wetu. Dawa hizi zinazorotesha maisha seuze afya ya halaki. Kama nguruwe ni haramu iweje mihadarati? Halali! Haramu ya halali! Hapana! Mihadarati sharti iwe batili ya haramu! Sote*

*tuukomeshe uraibu yeyote mwenye kushiriki nayo ni nduli wa maisha yetu. Msimfiche katu! Mwanikeni mlivyomwanika huyu Makusudi. Haki yao ipo kortini. Asanteni sana*.”

Polisi walimchukua na kunyakua kwenye mikoni ya wananchi walipungua subira ya haki kutimia. Tayari alikuwa amepapurwa kidogo na waliokosa kustahimili hasira zao. Wapo walimnyorosha kwa viboko. Wapo waliomkemea kwa maneno makali. Siku haikuwa siku kwake. Inspekta Mzee Mzoa na kikosi chake alimpeleka mbio kwenye kituo cha Kijutoni. Alikaa huko chini ya ulinzi mkali. kwake kulikuwa kama makazi ya zamani. Anakumbuka alijipataje hapo."History can repeat and regenerate itself.”

Sasa kipenga cha hatima yake kimepigwa mahakamani kwa mara nyingine tena. Taathira ya kesi hii sikuisawiri kwa uzuri machoni na akilini mwangu tena haikunipendeza hata kidogo jinsi ilivyosonga kwa mwendo wa kobe na ngisi! Kulingana na majibizano ya mawakili wa pande mbili, nilibaini chai ya kuhadaa kinywa imemwagwa upande fulani.

Wenyeji walijaa mahakamani siku hiyo. Walitaka haki itimie wakiona kwa macho yao. Walifika wote. Si wa Mapona si wa Masazoni si wa Kichakamkwanjuni si wa Mtemanyuki wala si wa Mashombo.Wote walikuwa pale wakitega masikio na kutundika macho kwenye meza yangu ya jaji.

“*Lazima nitamsenga vizuri ndugu huyu. Lazima ajue kuwa asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na Ulimwengu* pia. Hawezi kuwa kizingiti kwa wengine. Kwa nini?

*La, sitajilegeza wala sitalegeza kamba. Lazima nitampiga kibobwe cha kumzindua na kutimiza haki. Nitatoa hukumu yangu*.” Nilijizungumizia mwenyewe nikitilia jicho sarakasi za jukwaa la kesi.

Kesi ilipinda na kupinduka huku na kule kama joka

lililopondwa jichwa lake. Majalada yalifunguliwa na kufungwa. Sauti za mawakili zilipanda na kushuka. Tetesi ziliongezeka zikipungua. Bila kusahau mchemko wa hisia za watu, ziliiva na kuungua wakati mwingine. Mashtaka na makosa yalimiminika bila hesabu. Ushahidi wa kila aina na ainati ulithibitishwa. Wakupinga walipinga vikali. Wakuungama waliunga mikono yao dhabiti. Hatimaye mkono wa lawama ukamnyookea rafiki yangu – Makusudi.

Mambo yalipamba moto hadi pale hukumu yangu ilipochuka safu na kusitisha mkingamo huu wa Makusudi kwa mara moja na ya mwisho. Hata kidogo, sikushindwa kumtabikisha rafiki yangu Tashi na samaki aliyeoza mwili mzima. abadani hafai kuwa kitoweo. Hivyo, Makusudi hakufaa kuwa mtu wa maisha tuoishi. Hakuwa na utu kabisa.

Niliamua hukumu yake ni miaka thenini u ishirini gerezani kule Shikadabu.Miaka saba kwa kila kosa. Alikuwa na makosa matatu mazito; kushiriki wivi sugu kwa siri, kuwalaghai watu na kusambaza dawa za kulevya ovyo ovyo. Hasa kwa watoto wa shule.

Kando na hayo, nilmwongeza kiboko cha mwisho kwa kumpa miaka kenda ya kusambaza gonjwa hatari kwa kutumia dawa za kulevya. Ni watoto wengi waliokuwa mateka wa ugonjwa aliowatakia kwa hiari yake. Mathalani, sheria ya korti ilitoa kiwango fulani cha mali yake yakidhi matibabu yao.

Mahakama ya Mashombo ilimpa kifungo cha miaka dhahari ya sulubu na shokoa gerezani baada ya kupatikana na hatia zinazosadifu makosa ya jinai. Mkewe naye akapata pigo lingine zaidi. Alitozwa faini ya nusu milioni kwa kuwa mhusika mshiriki wa tuhuma zilifika kortini. Hapa ndipo Makusudi alipopasuliwa ukweli na maisha yake. Alikua ameyachezea shere sasa yamempasua jibu. Hakuwa na kufutia machozi. Kila kitu kilimnyooshea kidole cha lawama. Hana tena hatua ya kupofusha watu na uzuri wake uliokuwa mkakasi. Matendo yake yalimzima mwenyewe.

Tukiwa nje ya korti. Wenyeji na mahakama nzima ilishangila kwa shangwe hekima ya hukumu yangu. Walishangilia kuondolewa kwa mzigo mzito kati ya vijana wao. Waliona mwanzo mpya nilouona hata mimi mwenyewe hapo awali.

Nakumbuka Bwana Koja na mkewe Bi. Tumaini wakinipongeza (wazazi wake Makusudi). Wazazi wangu, Bwana Mlafani na Bi. Rehema walizipata habari hizo rungani. Walichukua muda wao pia kunipungia mkono wa kutenda haki.

Chachania – nduguye Makusudi alinipiga pamabaja kama rafiki. Alifurahia hatua yangu ya mwisho. Jambo ambalo sikulitarajia kwake kama ndugu ya mtu. Kushukuru kwake, kulinirudisha nyuma kwenye mawazo yangu ya zamani. Nilikumbuka maneno aliowahi kumwambia Inspekta Mzoa tulipokuwa tungali shuleni, kule Chumio.

Yalikuwa maneno yenye uzito na uzalendo aliyoyasema pale Kijutoni siku alipotekwa nyara Makusudi. Kwa hakika, amenifundisha kuwa mzalendo kindakindaki. Si kwa nchi yangu tu bali pia kwa jamii yangu.

Kila mmoja aliridhika. Kila mtu alitambua ya kwamba mzaha aliouweka mbele mwenzetu ni kisima cha kujichimbia. Sote – wenyeji kwa wapita-njia kule Mashombo, tuliungana mkono kufuta maovu yaliomea kwenye jamii yetu. Kila mmoja aliamidi kwamba maisha hayana mzaha na *ukichezea zuri na baya hufika*.

baada ya hekaheka za kortini kuisha, nilirudi afisini mwangu. Nilirudi kukikalia kiti changu na kuiwasha tena redio. Nikawaza kwa kina iwapo nimeambulia hekima au nilitenda shombo. Nakumbuka bado yale maneno ya sauti ilionijia asubuhi. Naikumbuka sauti ile ikisema,

*" Nakuona haupo makini. siwezi kukuita bundi, bado ukomavu haujakushika mkono vizuri. kuna hatua zinakungoja uzipige imara ili*

*uwe sawa na shwari.'*

*"Nimepiga hatua ipasavyo. Sasa, nimekuwa bundi. Naona ukomavu na busara hazijanigea."*

Nilijitania mwenyewe. Halafu nilipata fahamu kuwa, maneno ya mtu ni amali. Maneno hugunaguna na nafsi nayo nafsi hubembeleza azma. Lazima mtu ajisukume na ajisikilize. Na zaidi, ishi ukijua kuwa, duniani kuna watu. Sauti yako haikosei jambo. Nafasi ya kusaidia ikigonga hodi, ifungulie bila wasiwasi. Daima msaada ni kikoa, utakikanapo jitahidi. Kuwa mhimili. Kesho ya mtu ni fumbo.... Nimejufunza mengi. uso wa maisha ujengwa kuanzia jana na juzi si leo na kesho pekee. kuteleza mara nyingi si kuanguka. ukiteleza simama, jipanguse na uimarishe mwendo. Kamwe usirudie yalio kuweka chini. Kwani yana karaha na majuto. Ndivyo yalivyo hayo makusudi ya jana!

Nilijirudi kutoka mawazoni. Nikainuka kitini taratibu. Nikasimama kwenda zangu. Mlango wa afisi hiyo nikaufunga nyuma yangu.Ndi!

# SHEREHE

**A**

**Albadiri:** kisomo cha kuapiza jambo baya au kinga

**Alifu kwa kijiti:** anza upya**.**

**Aruba: Nne**

**Afu**: shauri

**Afueni:** afadhali

**B**

**Batili: -isio halali**

**Bingirika:** kugeuka upande upande

**C**

**Chakachaka:** kwa haraka

**Chaji:** shtaki

**Chelea:** susia

**Chege: -**isioiva

**Chinjachinja:** mchinjaji

**D**

**Danga:** kijana, kijulanga, kinda.

**Dhihaka:** kejeli, shere goya.

**Dede:** wima

**F**

**Fauwa:** mamoja

Furufu: furahifu; ya kukufarisha.

**H**

**Hadhari:** kuwa macho, kuwa makini,kijichunga

**Hangahanga:**

**Hatihati:** wasiwasi

**Hawafu:** woga, mtu mwoga

**Hohosa:** tamka maneno yasiofahamika; kuweweseka

**Harubu;** taabu, adha

**Himila:** ujauzito, mimba

**I**

**Ijara:** malipo ya kazi iliyofanywa.

**Ijaza:** ruhusa ya kutenda jambo katika dini, kibali cha mahafali

**J**

**Jitu tambo:** mtu mwenye mwili mkubwa; misuli tinginya

**K**

**Kitende:** makao, hashuo, maskani makazi.

**Kichea:** kwa ghafla

**Kidimu:** kuku mwenye manyoa yaliosimama.

**Kingwangwa:** jambo lililozidi uzito unaokadiriwa kutoka mwanzo

**Kicho:** hofu kikuli, kitete

**Kiwe:** ugonjwa wa kutoona vizuri

**Kitete:** uoga, hofu, ukunguru

**Kikakakaka**: kwa haraka

**Kusapasapa:** kusitasita

**Kukurukakara:** hekaheka

**kuzingazinga na ombwe:** kuchezesha na jambo la hatari; kufanyia mchezo hatari.

**Kokomokwa:** bubujuikwa

**L**

**Maro**: pigo la watu wengi.

**Marisau**: risasi, marisawa.

**Mburu matari:** masikini wasiojiweza.

**Matete**: aina ya nyasi. (*Umoja ni **tete***)

**Mrimo**: kazi ya uganga

**Mterehemeshi**: mcheshi

**Mangazimbwe**: sarabi, mangati au mazigazi

**Masa**: makosa, mambo mabaya

**Mkimwa**: mtu anayechoshwa na jambo kwa haraka, mkinaifu

**Nishai:** poteza fahamu kutokana na ulevi wa pombe au dawa za

kulevya.

**Noa:** kwama

**Ndege mbaya**: nuksi, bahati mbaya.

**P**

**Pua nguo: tupilia mbali nguo, toa.**

**Piga selo:** kutoa milio mikali, piga nduru**.**

**Piga ubwana:** kuwa na raha mustarehe**.**

**Piga goe:** tegemea**.**

**S**

**Sawiri:** unda picha kwa kalamu

**Selea:** ishi mahali kwa muda mrefu**.**

**Seezi:** mkato au mistari kwenye vidole**.**

**Shufaka:** hofu

**T**

**Tabikisha:** linganisha, fanya kuwa sawa na

**Tadi:** maringo

**Thenini u ishirini:** ishirini na mbili

**Tosa**: zama, tumbukia

**Tumba**: robota,

**Tango**: muziki wa mtindo wa kilatino.

**Tabasuri**: hekima

**Tema**: acha kitu

**Tunuku**: bariki, faidi

**Tojatoja:** kuweka alama, chanja, vuaza

**U**

**Ugono:** usiku, wakati wa giza.

**Ulimbwende: uzuri**

**Ukiri**: hali ya kukubali ukweli wa jambo.

**Ukaini**: utukutu, ukaidi, ujeuri.

**Uchapasi wa majengo:** mvuto wa nyumba

**Unazi**: uraibu

**Usodai:** madaha, maringo, kiburi

**W**

**Welekevu**: busara, utaratibu wa kuelewa.

**Z**

**Zingazinga; enda** huku na huko, zunguka